# OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## NUKUU ZA SOMO LA KISWAHILI

## DARASA LA SITA

## M

# KUWASILIANA KATIKA MIKTADHA MBALIMBALI

**Kuanzisha na kuendeleza mazungumzo katika miktadha mbalimbali**

**Kuimba wimbo wa kizalendo kwa ufasaha**

Wimbo ni tungo zenye kufuata mapigo ya kimuziki yenye mahadhi ya kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti na yenye mpangilio maalumu wa maneno.
Nyimbo hutumia lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi na hupangwa kwa utaratibu au muwala wenye mapigo ya kimuziki au mizani.
Wahusika wa nyimbo huwa mtu mmoja mmoja au kikundi cha watu. Nyimbo aghalabu huambatana na ala za muziki kama vile ngoma, zeze, marimba, makofi, vigelegele, kinanda, gitaa n k

Nyimbo huimbwa popote kulingana na tukio au muktadha unaofungamana na wimbo huo. Hivyo basi kuna nyimbo za:-

i. Dini
ii. Harusi
iii. Siasa
iv. Jando/unyago
v. Kilimo
vi. Nyimbo za kuwindia wanyama n.k.

**Kazi/faida za nyimbo**

1. Kuburudisha - nyimbo huburudisha hasa pale mtu anapokua amechoka na majukumu mfano shughuli za kilimo.
2. Kuelimisha-nyimbo hutumika kuelimisha jamii juu ya masuala mbalimbali mfano:- jinsi ya kujikinga na ugonjwa wa UKIMWI.
3. Kuhamasisha - nyimbo hutumika kuhamasisha jamii mfano kwenye masuala ya kisiasa juu ya kujiandikisha kupiga kura pia kwenye shughuli za afya
4. huwahamasısha watu kufuata kanuni za afya ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu.
5. Kuliwaza - nyimbo hutumika kuliwaza pale jamii inapopatwa na tukio kama la kifo. Takribani shughuli zote za maisha ya binadamu huambatana na uimbajı wa nyimbo.

**Uzalendo**
Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda, kuithamini na kujitoa mhanga kwa ajili ya nchi yake.
Mzalendo wa kweli daima anaweka maslahi ya nchi mbele.

**Sifa za mzalendo**


Ili mtu aitwe mzalendo ni lazima awe na sifa hizi;

i. Kuzaliwa nchi husika na angalau mzazi mmoja au wote wawili wawe ni wazawa.
ii. Awe mwaminifu wa kulipa kodi, kutoibia nchi yake kwa njia yeyote
iii. Kutokua mharibifu au mfujaji wa mali na rasilimali za nchi.
iv. Kuwapenda watu wote hasa viongozi wanaoijenga nchi bila kujali chama, udini, ukabila wala rangi yake.
v. Kuweka juhudi kubwa katika kuitangaza nchi yake vizuri ndani na nje ya mipaka
vi. Kuwahamasisha watu wa karibu yake kama familia, ndugu majirani na marafiki kuipenda nchi na kujitoa muhanga kwa ajili ya nchi yao

Hapa Tanzania wapo baadhi ya viongozi ambao kweli ni wazalendo

i. Mwl Juliasi Kambarage Nyerere ni mfano mzuri wa kuigwa, ni mtanzania mzalendo na anazo sifa zote za uzalendo. Pale alipopigania uhuru wa Taifa Letu kutoka kwa wakoloni, pia alipopigana vita na Iddi Amini alipotaka kuchukua ardhi ya watanzania. Mwalimu Nyerere alijitoa muhanga

ii. Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa waziri mkuu wa Tanzania nae alikuwa mzalendo kwa kupambaba na watu waliokuwa wanahujumu uchumi wa Tanzania



iii. Raisi John P. pia ni mzalendo kwa jinsi anavyopambana na wala rushwa, kulinda na kutetea rasilimali za nchi



**Sifa za watu wasio wazalendo**

- Watu wanaotumia rasilımali za nchi vibaya
- Kuharibu miundo mbinu
- Watu wanaohifadhi fedha zao nje ya nchi
- Wezi wa malı za umma
- Kuisema nchi vibaya
- Mafisadı
- Kuthamini vitu na mambo kutoka nje ya nchi

**Wimbo wa kizalendo**



**Tazama ramani**

Tazama ramanı utaona nchi nzuI1,
Yenye mito na mabonde mengi ya nafaka
Nasema kwa kinywa halafu kwa kufikiri
Nchi hiyo mashuhuri huitwa Tanzania
Kitikio: Majira yetu haya yangekuaje sasa
Utumwa wan chi Nyerere ameukomesha

Chemichemi ya furaha ama nipe tumaini
Kila mara kwako niwe niliburudika
Nakupenda sana hata nikakufasiri
Nitalalamika kukuacha Tanzania
Kitikio: Majira yetu haya yangekuaje sasa
Utumwa wa nchi Karume ameukomesha

Nchi yenye azimio lenye fumaini.

Naliwe peke yako mwanga wa kitanzania
Ninakuthamini hadharani na moyoni
Unilinde nami nikulinde hata kufa
Kiitikio: Majira yetu haya yangekuaje
sasa Utumwa wa nchi Kawawa
ameukomesha

**Faida za nyimbo za kizalendo**

Nyimbo za kizalendo husifia Taifa, mfano mzuri wa nyimbo za kizalendo ni kama vile nyimbo za Taifa (Mungu ibariki Tanzania), Tanzania Tanzania, Tazama ramani n k. Nyimbo za kizalendo huzindua moyo wa uzalendo kwa nchi na chuki kwa maadui wa nchi husika. Pia nyimbo za kizalendo huelezea na kusifia uzuri wa nchi na watu wake.

**Kutaja na kueleza mawazo makuu yaliyomo katika wimbo wa kizalendo**
**Jibu maswali yafuatayo kutokana na wimbo wa kizalendo hapo juu**

1. Taja nchi iliyotajwa katika wimbo Tazama Ramani
    - ❖ Nchi iliyotajwa ni Tanzania
2. Eleza kwa kifupi uzuri uliotajwa katika wimbo Tazama Ramani
    - ❖ Nchi ya Tanzania ina miti na mabonde mengi ya nafaka ni nchi yenye amani na furaha hakuna vita ni nchi huru inayo uhuru wake haitawaliwi na nchi nyingine.

3. Taja watu waliokomesha utumwa katika nchi hiyo
    - ❖ Nyerere, Karume, Kawawa

4. Katika wimbo mwandishi anaahidi nini?
    - ❖ Mwandishi anaahidi kuithamini nchi na kuilinda
5. Umejifunza nini kutokana na wimbo huu
    - ❖ Nimejifunza kuwa mzalendo kwa kuipenda nchi yangu, kuithamini na kuilinda. Hii ni pamoja na kulinda rasilimali zote za nchi na kuzitunza.

**Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya;**

**1. Ramani**
- ❖ Mwalimu alitufundisha jinsi ya kusoma ramani

**2. Nafaka**
- ❖ Bwana shamba alituelimisha jinsi ya kuhifadhi vyakula vya nafaka

**3. Moyo**
- ❖ Mwalimu Nyerere aliwatia vijana moyo ili kupambana na nduli Idd Amin

**4. Utumwa**

- Hayati Mwalimu Nyerere alipigania Taifa la Tanzania na kulitoa kwenye utumwa dhidi ya wakoloni.

**Kughani shairi kwa kuzingatia kanuni za mashairi, vina, mizani na kituo**
Shairi/mashairi ni tungo zenye kutumia mapigo ya silabi kwa utaratibu maalumu wa kimuziki kwa kutumia lugha ya mkato, lugha ya picha na tamathali za semi.

**Aina za mashairi**

i. **Mashairi ya kimapokeo**

- Haya ni mashairi yanayozingatia kanuni za urari (ulinganifu) wa mizani, vina, idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi. Vilevile haya huitwa mashairi funge

ii. **Mashairi huru**

- Haya ni mashairi yasiyozingatia kanuni za kimapokeo yaani hayazingatii kanuni za urari (ulinganifu) wa mizani, vina, idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi, mashairi haya huitwa mashairi ya kisasa.

**Vina**
Vina ni silabi zenye sauti ya namna moja zinazotokea katikati au mwishoni mwa kila mshororo wa kila ubeti wa shairi. Hivyo shairi lina vina vya kati na vina vya mwisho. Ili shairi lako lihesabike kama limetimia vina ni lazima herufi za kati na herufi za mwisho za ubeti ziwe zinafanana.

**Mfano;**
Tulopeleka bungeni, wamegeuka nyang'au
Mafisadı kama nini, baladhuli mabahau
Wanavunja mpini, konde wamelisahau
Zamani za siku hizi, mambo siyo yavyokua
Vina vya katı ni ni na vina vya mwisho ni u

**Mizani**
Mizani ni ulinganifu wa idadi ya silabi katika kila kipande au mistari ya ubeti wa shairi. Mara nyingi mashairi ya kımapokeo huwa na mizani nane (8) kwa kila kipande na mizani kumi na sita (16) kwa kila mstari (mshororo)

**Mfano,**
Kiswahili ni kitamu, kuongea na kusoma
Daima hakishi hamu, kama mtoto na mama
Jifunze ukifahamu, ukizungumze vyema
Kiswahili lugha yangu, sikuachi asilani

**Kituo**
Huu ni mstari wa mwisho katika kila ubeti wa shairi, kituo pia huitwa kimalizio au kiini mara nyingi hujirudia rudia katika kila ubeti

**Mfano;**
Yamezidi mitaani, madawa kuenea
Si bangi si heroini, nani ametuletea
Nipigapo darubini, vijana ndo meumia
Nani alotuingiza, kwenye janga la kulevya

Afya zimezorota, miili medhoofika
Uraibu ni-matata, ndoa kusambaratika
Mirungi wakishapata, watoto watairuka,
Nani alotuingiza kwenye janga la
kulevya,

Kweli inasikitisha, hali iliyotufikia,
Serikali hakikisha, vituo mmeviweka,
Madawa kuyapotosha, ukarabati
kunyooka, Nani alotuingiza kwenye janga
la kulevya

Joka lilokati yetu, mola tampa adhabu,
Asambazae kwetu, wana wetu kuharibu
Mali na cheo si kitu, ipo siku utajibu
Nani alotuingiza kwenye janga la
kulevya

Hivyo kituo ni; Nani alotuingiza kwenye janga la kulevya.
**Jibu maswali yafuatayo**
1. Shairi hili lina beti ngapi?
    - Shairi hili lina beti (4) nne
2. Kila ubeti una mishororo mingapi?
    - Kila ubeti una mishororo minne (4)
3. Shairi hili lina mizani ngapi kwa kila mstari (mshororo)
    - Shairi hili lina mizani kumi na sita (16) kwa kila mstari

4. Taja kituo cha shairi hili
    - Kituo cha shairi hili ni; Nani alotuingiza kwenye janga la kulevya.
5. Taja vina vya kati vya ubeti wa pili
    - Vina vya kati vya ubeti wa pili ni ta
6. Unafikiri kichwa cha shairi ni nini?

- Kichwa cha shairi ni madawa ya kulevya

7. Kwenye ubeti wa nne (4) mshairi anazungumzia joka ni kitu gani
- ❖ Joka ni mtu anayesambaza madawa ya kulevya

8. Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya

i. Janga
- ❖ Wananchi wa Songambele walipokata miti hovyo walikumbwa na janga la ukame

ii. Ukarabati
- ❖ Nyumba yetu ilipochakaa tuliifanyia ukarabati

iii. Dawa
- ❖ Mwalimu alituambia vijana tujiepushe na dawa za kulevya

iv. Mali
- ❖ Mzee Juma alikamatwa na mali va wIzı

**Kazi ya kikundi**

Kwa kushirikiana na mwenzako tunga shairi la beti tano kuhusu shule yako.

**Kuigiza igizo dhima kuhusu elimu ya biashara na kueleza umuhimu wake.**

Igizo ni mpangılio wa maneno unaoambatana na utendaji wa wahusika, wahusika huwa wanaiga mambo ambayo yanafanywa na jamii husika na kuyaonesha mbele ya hadhira. Pia maneno yanayosemwa na wahusika yanalingana na yale ya jamii husika. Hivyo basi uigizaji hautagemei sauti tu bali pia vitendo mijongeo ya mwili pia matendo yasiyoandamana na sauti kama ilivyo kwa uigizaji bubu. Wakati mwingine maigizo huambatana na nyimbo. Uigizaji hujumuisha vitendo kama vile michezo (ya watoto), majigambo, vichekesho, ngonjera na mazungumzo.

**Igizo**

Siku moja Sakina na Asha walikua wamekaa upenuni mwa nyumba yao na kuzungumza mambo mbalimbali. Pia walizungumzia juu ya ujasiriamali, mazungumzo yao yalikuwa hivi:

**SAKINA:** Mambo Asha, mzıma wewe?
**ASHA:** Poa tuu, mimi mzima sijui wewe
**SAKINA:** Nami nipo poa tuu
**ASHA:** Mh! Hivi Sakina unaelewa nini kuhusu elimu ya ujasiriamali
**SAKINA:** Elimu ya ujasiriamali! Kwani wewe huelewi ndo umeanza kuisikia leo au?
**ASHA:** Hapana Sakina nimeisikia siku nyingi ila siielewi rafiki yangu, samahani naomba unisaidie kunieleweshe.
**SAKINA**: Ujasıriamali hii inajumuisha kununua na kuuza bidhaa kwa kiasi kidogo.
**ASHA:** Ina maana kununua na kuuza bidhaa kwa kiasi kikubwa sio biashara?

**SAKINA:** Hapana sio kwamba sio biashara la hasha! ila kwa wafanya biashara wakubwa hao hawaitwi wajasiriamali. Mfano Bakhresa huyu ni mfanyabiashara mkubwa anauza bidhaa zake hadi nje ya nchi na pia ameajiri wafanyakazi wengi, na uzalishaji wake ni mkubwa tofauti na mjasiriamali yeye biashara yake ni kwa kiasi kidogo.
**ASHA:** Sasa nimekuelewa je, kuna umuhimu wowote wa kupata elimu ya ujasiriamali wakati biashara yenyewe huwa ni kwa kiası kidogo?
**SAKINA:** Kwanza kabisa, elimu ya ujasiriamali itakusaidia kujua mahitaji ya jamii inayokuzunguka na soko la bidhaa. Pia elimu inasaidia kujua kama biashara yako inakupa faida au hasara. Vilevile kujua kama biashara yako inakua au la. Pia kwa kuwa unakua na ujuzi hii inasaidia kujiajiri mwenyewe na kuepuka suala la kutokua na ajira. Mwisho humsaidia mhusika kuchangamana na watu mbalimbali katıka shughuli za biashara
**ASHA:** Oh! asante sana, sasa nimeelewa kuhusu elimu ya ujasiriamali.

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Igizo hili linahusu nini?
   - ❖ Igizo hili linahusu elimu ya ujasiriamalı

2. Wahusika wakuu katıka igizo hili ni akina nanı
   - ❖ Wahusika wakuu katika igizo hili ni Sakina na Asha

3. Kwa mujibu wa igizo hili ujasiriamali unajihusisha na nini
   - ❖ Ujasiriamali unajihusisha ununuzi na uuzaji wa bidhaa kwa kiasi kidogo

4. Taja faida za elimu ya ujasiriamalı
   - ❖ Husaidia kujua mahitaji ya jamu inayokuzunguka na soko la bidhaa.
   - ❖ Husaidia kujua kama biashara yako ina faida au hasara
   - ❖ Pia husaidia kujua kama biashara yako inakua
   - ❖ Husaidia mtu aweze kujiajiri
   - ❖ Husaidia mfanyabiashara aweze kuchangamana na watu mbalimbali katika biashara yake.

**2. Andika maneno yenye maana sawa na maneno yafuatayo**

i. Soko – gulio
ii. Ridhaa - idhini
iii. Ujuzi - mararifa-
iv. Mnadi – dalali
v. Karaha - kero
vi. Shujaa - jasırı
vii. Bakiza – saza
viii. Siha - afya

ix. Kaditama - tamati,kikomo
x. Nyati- mbogo
xi. Rushwa - hongo
xii. Ndondi - masumbwi
xiii. Majira - wakati
xiv. Lisani- ulimi
xv. Korongo - gema
xvi. Soka - kandanda
xvii. Mvuli – mvulana
xviii. xviii. Wakala – ajenti
xix. Nina –mama

**3. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika wingi**

i. Mwanafunzi mzuri husoma kwa bidii
- ❖ Wanafunzi wazuri husoma kwa bidiu

ii Kisima changu kimejaa chura
- ❖ Visima vyangu vimejaa vyura

iii. Kicheche kimekamata kuku wangu
- ❖ Vicheche vimekamata kuku wangu

iv. Sare ya shule yetu ni shatı la rangi nyeupe
- ❖ Sare za shule zetu ni mashatı ya rangı nyeupe

v. Shona nguo hu kwa ustadi
- ❖ Shona nguo hızı kwa ustadi

vi. Kijana huyu ni mjasiriamali
- ❖ Vijana hawa ni wajasiriamali

vii. Ukuta huu umeanguka
- ❖ Kuta hizi zimeanguka

viii. Mkungu wa ndizi umeanguka
- ❖ Mikungu ya ndizi imeanguka

ix. Sentensi hii ipo katika wakati uliopo
- ❖ Sentensi hizi zıpo katika nyakati zilizopo

x. Tamka neno hili kwa ufasaha
- ❖ Tamka maneno haya kwa ufasaha

xi Mto huu ndio uliofurika

- Mito hii ndiyo iliyofurika

**4. Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya**

i. Elimu

- Mwalimu alituambia tusome kwa bidii kwani elimu ni ufunguo wa 1

ii. Biashara

- Mama yangu anajıshughulisha na biashr

iv. Faida

- Mama alipouza mazao yake alipata faida kubwa

iv. Rafiki

- Mama aliniambia ni vizuri kuwa na rafiki mwaminifu

v. Mtaji

- Shangazi alianza biashara yake ya kuuza nguo za watoto kwa mtaji wa shilingi lakı moja.

**5. Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali ya kutendewa**

i. Timu yetu ilicheza mechi vizuri

- Timu yetu ilichezewa mechi vizuri

ii. Panya alisumbua ghalani

- Panya alisumbuliwa ghalani

iii. Juma anakaanga mandazi kwa ajili ya kuuza

- Juma anakaangiwa mandazi kwa ajili ya kuuza

iv. Tumefua nguo zetu

- Tumefuliwa nguo zetu

v. Walipanga kukutana na uongozi wa kijiji

- Walipangiwa kukutana na uongozi wa kijiji

vi. Anacheza muziki kwa ustadi mkubwa

- Anachezewa muziki kwa ustadi mkubwa

vii. Mama alipiga simu usiku

- ❖ Mama alipigiwa simu usiku

**6. Bainisha kauli za utendaji katika.sentensi zifuatazo**

i. Jordani alishinda mbio za maratoni na kurudi na medali

- ❖ Kauli za kutenda

ii. Kokoto na simenti zimechanganyika vizuri

- ❖ Kauli ya kutendeka

iii. Suruali iliendana na shati

- ❖ Kauli ya kutendana

iv. Dada anamsomesha mdogo wake

- ❖ Kauli ya kutend

v. Mbwa na paka wanapigana

- ❖ Kauli ya kutendana

vi Shangazı na mjomba hutembeleana mara kwa mara

- ❖ Kauli ya kutendeana

vii. Mlima unamiminika theluji mithili ya mto

- ❖ Kauli ya kutenda

viii. Mwalimu wetu ana utaratibu wa kuandikiwa majina ya wasumbufu darasani

- ❖ Kauli ya kutendewa

ix. Ubwabwa ulipikwa vizuri na mama

- ❖ Kauli ya kutendwa

**Kusimulia hadithi yenye methali na kuelezea maana ya mafunzo yaliyopatikana katika methali.**

Hadithi ni masımulizi ambayo yanatumia lugha ya mjazo au lugha ya nathari na mtiririko wake ni mwepesi au sahili. Kuna hadithi za kubuni na hadithi za kihistoria,

Methali ni vsemi mfupi wa mapokeo wenye mpangilio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jamii husika.
Ni kauli fupi yenye pande mbili za fikra ambazo upande wa kwanza huanza na upande wa pili humalizia mfano "akili nyingi huondoa maarifa".

**Maana** – mtu mwenye kuonesha uhodari mwingi katika jambo aghalabu hutokea kuharibu
**Mafunzo** – mtū asijifanye anajua kila kitu-kwa RUna Vingne hajui

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata; Maisha ya Jamal**

Katika kijiji cha Lawate kulikua na babu mmoja aitwae Hamisi. Babu huyu alikua akiishi na mjukuu wake aitwae Jamali. Waliishi katika nyumba nzuri, walikula na kuvaa vizuri. Kwa ujumla maisha yao yalikuwa mazuri. Malezi ya babu hayakua mazuri sana kwani alikuwa akimwachia uhuru sana na wahenga walisema "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo". Wazee wenzake na Hamisi walijitahidi kumwambia asimdekeze mjukuu wake, lakini hakuwasikiliza. Wazee wenzake walimwambia "samaki mkunje angali mbichi".

Jamali alivyozidi kukua ndivyo alivyozidi kuwa mtoto mbaya kwani aliacha shule na kuanza tabia ya wizi. Mzee Hamisi alipoona mjuku wake ameacha shule alisikitika sana. Akakumbuka maneno ya wazee wenzake akajisemea moyoni "Mchelea mwana kulia hulia yeye" Babu alianza kumkanya mjukuu wake lakini alikuwa amechelewa Jamali nae hakumsikiliza babu yake, babu alimwambia "Mwana mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idd". Ama kweli "mchuma janga hula na wa kwao" siku moja Jamali alikwapua mkoba wa dada mmoja. Alikimbizwa na wananchi wenye hasira na alipokamatwa alipigwa vibaya sana.



Aliporudi nyumbani kwa babu yake damu zilikua zinamvuja mwili mzima. Loo! babu yake alishangaa na pia alisikitika sana na kumwambia Jamali "Asiyesikia la mkuu

huvunjika guu". Jamali mjukuu wangu nilikwambia achana na tabia ya wizi hukunisikia ona sasa yaliyokupata lakini damu ni nzito kuliko maji. Babu yake Jamali alimtibu majeraha yake na kumpa dawa za miti shamba hadi akapona. Baada ya kupona Jamali na wenzake walikwenda kuiba kwenye duka la mchina mmoja. Lahaula! kumbe lile duka lilikua na ulinzi mkali Jamali na wenzake walipoanza kuvunja mlango wa duka walizingirwa na wamizi na kUkamatwa na kupelekwa kiuo cha polisi kešho yake walipelekwa mahakamai da KUSomewa iasme., WaluuKumiwa kifungo cha miaka mitano. Ama kweli mchimba kisima huingia mwenyewe na mkamia maji hayanywi.

Babu yake alipopata taarifa ile alisikitika sana na aliamua kufunga safari kwenda kumtembelea mjukuu wake gerezani kule alikofungwa. Alipofika huko alimkuta mjukuu wake na walisalimiana Alimtazama mjukuu wake usoni na kumwambia Jamali mjukuu wangu, mara zote nilikua nikikuasa kuwa dunia hadaa ulimwengu shujaa lakini hukunisikiliza.

Jamali alimsikiliza tu babu yake huku akibubujikwa na machozi. Babu yake alimtazama tena usoni na kumwambia "Asiyefunzwa na wazazi wake hufunzwa na ulimwengu na ndege mjanja hunaswa na tundu bovu sasa ulimwengu utakufunza. Sina budi kurudi nyumbani kwa heri" babu aliinuka na kuondoka.

Jamali alibaki amekodoa macho huku akiwaza na kujisemea moyoni, mdharau mwiba mguu huota tende. Laiti kama ningemsikiliza babu yangu wakati ule, yote haya yasingenikuta kweli mwenye pupa hadiriki kula tamu.

**1. Jibu maswali yafuatayo**

i. Jamali alikuwa akiishi na nani?

- ❖ Jamali-alikuwa akiishi na babu yake

ii. Mzee Hamisi alikua akiishi katika kijiji gani?

- ❖ Mzee Hamisi alıkuwa akiishi katika kijiji cha Lawate

iii. Kwanini Jamali alipigwa na wananchi wenye hasira?

- ❖ Kwa sababu alikwapua mkoba wa dada mmoja

iv. Jamali na wenzake walifungwa kifungo cha miaka mingapi?

- ❖ Walifungwa miaka mitano

v. Jamali na wenzake walikua na tabia gani

- ❖ Jamali na wenzake walikuwa na tabia ya wizi

2. Tunga sentensi kwa kutumia maneno haya

i. Kwapua

- ❖ Tulipokua sokoni Kariakoo mwizi alikwapua mkoba wa dada yang

ii. Damu

- ❖ Mgojwa alipopelekwa hospital aliongezewa dam

iii. Mjukuu

- ❖ Mjukuu wa mama yangu anapenda sana kunywa maziwa

iv. Mlinzi

- ❖ Nyumbani kwetu kuna mlinzi mkali sana

v. Mahakamani

- ❖ Jirani yetu alipokamatwa na kuku wa wizi alipelekwa mahakamani

3. Orodhesha methali zote zilizotumiwa katika hadithi hii

i. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
ii. Samaki mkunje angali mbicihi
iii. Mcheleamwana kulia hulia
iv. Mkaidi hafaidi mpaka siku
v. Mchuma janga hula na wa kwao
vi. Asiyeisikia la mkuu huvunjika guu
vii. Damu nzito kuliko maji
viii. Mchimba kisima huingia mwenyewe
ix. Mkamia maji hayanywi
x. Dunia hadaa ulimwengu shujaa
xi. Asiyefunzwa na wazazi wake hufunzwa na ulimwengu
xii. Ndege mjanja hunasa kwenye tundu bovu
xiii. Mdharau mwiba yeye ya huota tende
xiv. Mwenye pupa hadiriki kula tamu

4. Eleza maana na mafunzo yanayopatikana katika methali zifuatazo

1. Samaki mkunje angali mbichi

Maana - mtoto mfunze adabu akiwa bado mdogo akiwa mkubwa hatofundishika

**4. Eleza maana na manunzo yanayopatikana katika menal ziuatazo**

i. Samaki mkunje angali mbichi

- ❖ Maana - mtoto mfunze adabu akiwa bado mdogo akiwa mkubwa hatofundishika
- ❖ Funzo- Methali hii inawasihi wazazi wawafunze adabu watoto wao wangali bado wadogo ili wakue katika maadili mema kwani wazazi/walezi wasipowafundisha wangalı wadogo wakiwa wakubwa hatawasikiliza tena

ii. Damu nzito kuliko maji

- ❖ Maana: Ndugu yako wa damu ndiye anayeweza kukusaidia katika shida kuliko wengine.
- ❖ Funzo: Undugu baina ya watu si jambo rahisi kulitupilia mbali ama kulipuuza hivyo huwezi mwacha ndugu yako aangamie ni lazima kujitahidi kumwokoa hata kama mmegombana.

iii. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

- ❖ Maana: Mtoto huwa mwema au mtukutu kulingana na malezi anayopatiwa.
- ❖ Funzo: Tujitahidi kuwalea watoto katika malezi mema ili wasije kua na tabia mbaya na baadae wakapata matatizo mfano kufungwa jela, kuchomwa moto n.k

iv. Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe

- ❖ Maana - mzazi aogopaye mtoto wake kuumia kwa kumwadhibu akoseapo huishia kuumia mtoto anapopotoka na kuwa na tabia mbovu.
- ❖ Funzo Wazazi wanaonywa kutoogopa kuwaadhibu watoto kwani akiharibikiwa na kuwa na tabia mbaya ni aibu ya mzazi.

v. Mkaidi hafaidi mpaka siku ya Idd

- ❖ Maana - mtu asiye na utii au usikivu hujikosesha mengi mazuri kwa tabia yake.
- ❖ Funzo- tunapaswa kuwa watii na wasikivu ili tupate yalıiyo mema/mazuri

vi. Mchuma janga hula na wa kwao

- ❖ Maana- majanga asababishayo mtu katika kazi au maisha yake huishia kumdhuru yeye na watu wa karibu yake.
- ❖ Funzo - methali hii inawaasa watu kutofanya matendo mabaya kwani wakipata shida shida hiyo itagharimu na watu wa karibu yao. Mfano ukiiba ukapigwa ukaumia italazımu watu wa karibu kukuhudumia hadi upone.

vii. Mchimba kisima huingia mwenyewe

- ❖ Maana - anayepangia wengine ubaya, si ajabu akajikuta yeye mwenyewe akidhuriwa nao
- ❖ Funzo- si vizuri kuwafanyia watu mabaya kwani yanaweza kukugeuka ukadhurika, mfano ukiiba kwa mtu unaweza kukamatwa na kupigwa sana hadi ukapata ulemavu.

MWL

viii. Mwenye pupa hadiriki kula tamu

- ❖ Maana- Mwenye papara za kupata matokeo ya ghafla, huishia kupata matokeo duni kwani hakipi kitu muda wa kukomaa na kupendeza
- ❖ Funzo- Tusipendelee kufanya kazi za mkato bali tufanye kazi zenye tija ili kupata matokeo mazuri. Mfano – kutaka kupata mali au utajiri wa haraka unaamua kuhujumu uchumi au kula rushwa utaishia kufungwa jela.

**5. Kwa kila vifungu vya maneno vifuatavyo unda methali moja tu ambayo inawiana na maelezo husika**

i. Pale mtu anapopuuzia hatari au tatizo na kuona kuwa halina madhara ndipo panapoweza kumdhuru.
- ❖ Ndege mjanja hunasa kwenye tundu bovu

ii. Anayefurahishwa na kitu chochote au mtu yeyote, huweza kuona tuu uzuri wa hicho kitu au huyo mtu. Mtu akipenda kitu hukitetea hata kwa kukipa sıfa kisicho nazo
- ❖ Ukipenda chongo huita kengeza

iii. Mtu mwenye kuonesha uhodari mwingi katika jambo aghalabu hutokea kuliharibu.
- ❖ Akili nyingi huondoa maarifa

iv. Anayekataa kukanywa au mafundisho apewayo na wakubwa zake huishia kufikwa na mabaya ambayo angesikiliza pengine angeyaepuka
- ❖ Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

v. Kuwa tayari kuuliza pale usipoelewa kwani ukiona aibu kuuliza hutaweza kjifunza
- ❖ Kuuliza si ujinga

vi. Mambo ya ulimwengu si ya kutumainiwa sana lazima tuwe waangalifu na kutumia hekima ili kufanikiwa na kuwa salama.
- ❖ Dunia hadaa ulimwengu shujaa

vii. Usipuuze tatizo hata kama ni dogo laweza kuishia kukupa hasara au janga kubwa baadae
- ❖ Mdharau mwiba mguu huota tende

**6. Malizia methali zifuatazo**

i. Mfa maji__________________________________________
- ❖ Haachi kutapatapa

ii. Biashara__________________________________________
- ❖ Haigombi

iii. Bora nusu kitumbua mkononi____________________________
- ❖ Kuliko kitumbua kizima kilichopo dukani

iv. Nazi mbovu__________________________________________

❖ Harabu ya nzima

v. Ndovu /tembo hashindwi______________________________

❖ Na mkonga wake

vi. Chema chajiuza______________________________________

❖ Kibaya chajitembeza

vii. Heri nusu shari__________________________________________

❖ Kuliko shari kamili

**7. Andika methali zenye maana sawa na methali zıfuatazo**

i. Ng'ombe wa maskini hazai_____________________________________

❖ Asiye na bahati habahatiki

ii. Ngoja ngoja huumiza matumbo_________________________________

❖ Chelewa chelewa utamkuta mwana si wako

iii. Nguo ya kuazima haisitiri matako_________________________________________

❖ Wimbo wa kuazima haukeshi ngoma

iv. Limbukeni hana siri____________________________________________________

❖ Maskini akipata matako hulia mbwata

v. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti___________________________________________

❖ Aibu ya maiti aijuaye

vi. Baada ya kisa mkasa____________________________________________

❖ Baada ya chanzo kitendo

vii. Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi____________________________________

❖ Kisicho riziki hakiliki

viii. Bandubandu humaliza gogo______________________________________

❖ Haba na haba hujaza kibaba

**Andika neno moja linalojumuisha maneno yote**

**i.** Sato, sangara, changu, tasi, perege- **samaki**

**ii.** Chai, soda, juisi, maziwa – **vinywaji**

**iii.** Ugali, chapatti, pilau, nyama - **vyakula**

iv. Kanga, gauni, suruali , shati, sketi - **mavazi**
v. Visu, mshale, mapanga, mikuki-**silaha**
vi. Mtama, mahindi, uwele, mpunga - **nafaka**
vii. Malaria, kipindupindu, kikohozi, homa – **magonjwa**

**Kubainisha na kueleza taswira za kimawazo zilizo katika nahau kutoka katika hadithi**

Taswira ni mkusanyiko wa picha mbalimbali ziundwazo kupitia maelezo ya waandishi katika kazi ya fasihi. Picha hizi hujengwa kwa matumizi ya lugha au maelezo fulani ili kuufanya ujumbe kujitokeza kwa msisitizo mkubwa. Tamathali za semi husaidia katika kujenga taswira ya maandishi ya kifasihi mfano;

- Chumba kilikua kimepambwa kikapambika
- Mkabala wa kitanda palikua na meza iliyowekelewa redio iliyocheza kwa sauti ya juu.

**Nahau**

Ni semi fupifupi ambazo hutumia lugha/maneno ya kawaida lakini maneno hayo hutoa maana tofauti na ile iliyo kwenye maneno ya awali. Japokuwa nahau hutumia maneno ya kawaida lakini kauli yake ina undani kiasi kwamba kwa wageni wasioifahamu lugha hiyo hawawezi kuelewa maana.

**Mfano;**

- Ana mkono mrefu- mwizi
- Kuzunguka mbuyu – kutoa rushwa/mlungula
- Ana mkono wa birika - mtu bahili

Nahau kama zilivyo methali nazo zina
maana
Maana ya nahau hujengwa na taswira za kimawazo zilizomo ndani yake

**Ufahamu**

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yafuatayo**

Katika kijiji cha Songambele palitokea baa la njaa, baada ya wanakijiji hao kuharıbu mazingira, waliyaharibu mazingira kwa kukata miti ovyo na kulima kwenye vyanzo vya maji Mifugo mingi ilikufa kwasababu ya kukosa malisho, watu wengi afya zao zilidhoofika sana kwa kuwa wengi wao walikula mlo mmoja tu. Hii ilipelekea na baadhi ya watu kuaga dunia.

Mwenyekiti wa kijiji cha Songambele aitwae Juma aliamua kujitoa muhanga kushughulikia tatizo hilo. Alikata shauri kumualika bwana shamba aishie kijiji cha jirani ili aje awaelimishe wanakijiji wenzake. Mwenyekiti alifunga safari mpaka kijiji cha pili

na kumuomba bwana shamba aje awaelimishe juu ya utunzaji mazingira. Bwana shamba alikubalı ombi lile alımuahidi kuwa atakuja siku inayofuata, kwani vijiji hivyo ni pua na mdomo. Bwana Juma aliporudi aliwataarifu wanakijiji kwamba kesho yake kutakua na mkutano. Wananchi walikubali na walimwahidi mwenyekiti wa kijiji kwamba watawahi.

Kulipokucha asubuhi wanakijiji walifika kwa wingi kwenye mkutano, baada ya wanakijiji kujikusanya punde si punde nae bwana shamba aliwasili. Alipigwa na butwaa kuona kijiji cha Songambele kilivyogeuka kuwa jangwa.

Alianza kwa kuwasilimu wanakijiji na kisha kuwauliza kwanini kijiji chao kimekua na ukame hivyo? Mzee Hamisi alinyosha kidole kisha akajibu, vijiji vingine vimewaonea gere hivyo wakaamua kukipiga kipapai kijiji chao ndio maana kimenatwa.na janoa hilo.

Bwana shamba aliangua kicheko kisha akawaambia, hizo imani zenu zimepitwa na wakati. Mmeharibu mazingira wenyewe mmekata miti ovyo kwa ajili ya kuni na mmechoma mkaa na kulima na kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji. Hivyo kupelekea mvua kutokunyesha kwa wingi. Ili kuepukana na janga hili hamna budi kutunza mazingira ili mazıngira nayo yawatunze, Hivyo kila mtu asimame kidete kuhakikisha miti inapandwa upya

Mwenyekiti wa kijiji alimshukuru bwana shamba kwa kuwaelimisha, aliwauliza wanakijiji wenzake kama wana swali waulize kabla bwana shamba hajaondoka. Mzee Mkude alisimama kisha alianza kwa kumshukuru bwana shamba kwa kuwaelimisha. Mzee Mkude alimwambia bwana shamba kwamba wao wamekata miti wakauza na kuchoma mkaa. Hata pesa walizozipata hawakufanyia mambo ya maendeleo. Hawakuwapeleka watoto wao shule wala kuwanunulia sare na madaftari. Kwani waliishia kupiga maji tu, hivyo sasa wameelimika na atakua bega kwa bega na wanakijiji wenzake kutunza mazingira. Wanakijiji nao kwa pamoja walikata shauri kutunza mazingira ya kijiji chao ili kiwe kama kilivyokua hapo awali.

**1. Jibu maswali yafuatayo**

i. Ni kijiji gani kilipatwa na baa la njaa?
  - ❖ Kijiji kilichopatwa na baa la njaa ni kijiji cha Songambele

ii. Mwenyekiti wa kijiji hieho aliitwa nani?
  - ❖ Mwenyekiti wa kijiji hicho aliitwa Mzee Juma

iii. Ni shughuli zipi wanakijiji walizozifanya na kusababisha ukame?
  - ❖ Shughuli walizozifanya na kusababisha ukame katika kijiji chao ni kukata miti, kufuga na kulima kwenye vyanzo vya maji.

iv. Unafikiri ni kwanini bwanashamba aliangua kicheko
   - ❖ Bwanashamba aliangua kicheko kwa sababu mzee Hamisi alisema kijiji kimepigwa kipapai na vijiji vingine kwa kuwa waliwaonea gere.

v. Kwa nini mwenyekiti wa kijiji alimua kumualika bwana shamba aje kijijini kwao?
   - ❖ Alimwalika ili aje awaelimishe wanakijiji wenzake juu ya utunzaji wa mazingira

**1. Msamiati**

**Tunga sentensi kwa kila neno**

**a. Ukame**

❖ Mwalimu alitufundisha kwamba ukame husababishwa na mvua kutokunyesha kwa muda mrefu

**b. Njaa**

❖ Mdogo wangu alipohisi njaa alilia sana

**c. Alika**

❖ Mama alialika wageni wengi kwenye harusi ya dada vang

**d. Mazingira**

❖ Mwalimu alituambia tusicheze kwenye maZingira hatarıshi

**e. Kidete**

❖ Mjomba aliposingiziwa kaiba kuku mama yangu alisimama kidete kumtetea

**2. Nahau**

**Orodhesha nahau zote katika habari uliyoisoma**

- Kata shauri
- Aga dunia
- Pua na mdomo
- Punde si punde
- Pigwa butwaa
- Ona gere
- Pigwa kipapai
- Piga maji
- Bega kwa bega
- Kata shauri

MWL.

**Eleza taswira ya nahau zifuatazo**

i. Juta kuzaliwa

- Juta sana hasa baada ya kufanya jambo lililokuletea athari mbay

ii. Kaa chonjo
- Chukua tahadhari jiepushe na jambo

iii. Maji kuzidi unga
- Mambo kuwa mabaya, mambo kuharibika

iv. Maji kuzidi unga
- Mambo kuwa mabaya, mambo kuharibika

v. Shika usukani
- Ongoza, kuwa kiongozi

vi. Pua na mdomo
- Jirani sana, karibiana sana

vii. Pigwa kipapai
- Fanyiwa mambo ya kishirikina, chawiwa ama rogwa ili kukuondoa mahali ulipo katika nafasi fulani

viii. Piga chenga
- Kwepa mtu au majukumu

ix. Chapa kazi
- Kufanya kazi kwa bidii

**Chagua herufi ya jibu sahihi**

1. Fatuma na Asha hawapikiki katika chungu kimoja msemo huu una maana;
   a) Hawaishi1 pamoja
   b) Hawapendani
   c) Hawaelewani
   d) Hawazungumzi

Jibu C

2. Nikipata nafasi nitakuja kukutupia jicho maneno yaliyopigiwa mstari yana maana;
   a) Kukupa miwani
   b) Kukuona
   c) Kukutibu
   d) Kukupa zawadi

MWL

Jibu B

3. "Usinivike kilemba cha ukoka" ina maana gani?
   a) Usinisumbue
   b) Usinidanganye
   c) Usinishauri
   d) Usinidharau

Jibu B

4. Ashura alimezea mate kalamu ya Asha maneno kumezea mate yana maana gani
   a) Kutamani
   b) Kumeza mate mengi
   c) C. Kuona wivu
   d) Kuiga

Jibu A

5. Bakari ni mwingi wa habari maana yake ni
   a. Mwanahabari
   b. Mwongo
   c. Mmbea
   d. Mwenye maneno mengi

Jibu D

**3. Miundo**

**Tunga sentensi kwa kila muundo**

i. ………………….katikati ya…………………………..
   Mtoto amesimama katikati ya msitu

ii. ………………..juu ya…………………………………
   Kalamu ipo juu ya meza

iii. ……………………..chini ya…………………………….
   Mwajuma ameficha viatu chini ya kitanda

iv. ………………..ndani ya………………………………….
   Mdudu ameingia ndani ya embe

v. ………………..mbele ya……………………………………….
   Mwalimu amesimama mbele ya darasa

**4. Mazoezi ya lugha**

**Andika sentensi zifuatazo katika wakati uliopita**

i. Mwalimu Hamisi anafundisha somo la kuhesabu
   - Mwalimu Hamısı alıfundisha somo la kuhesabu

ii. Fatuma anauliza swali darasani
   - Fatuma aliuliza swali darasani

iii. Mwajuma amefika salama
   - Mwajuma alifika salama

iv. Wanafunzi wanaimba nyimbo nzuri
   - Wanafunzi waliimba nyimbo nzuri

v. Mwalimu anatoa zawadi
   - Mwalimu alitoa zawadi

**Badıli sentensi zifuatazo ziwe katika kauli kutendwa**

i. Dada amepika chakula
   - Chakula kimepikwa na dada

ii. Fatuma amesoma vitabu vingi
   - Vitabu vingi vimesomwa na Fatuma

iii. Mtoto amechana kitabu changu
   - Kitabu changu kimechanwa na mtoto

iv. Mgeni rasmi aliwasalimia wageni
   - Wageni walisalımıwa na mgeni rasmi

v. Dereva ataendesha basi la shule
   - Basi la shule litaendeshwa na dereva

vi. Mama alikua ananalilia bustani
   - Bustani ilipaliliwa na mama

vii. Baba alifunga mlango
   - Mlango ulifungwa na baba

**Kusimulia mambo yaliyoonekana baada ya kuranya ziara Tupr kauka mazngira ya jiramna shule.**

Ziara ni safari ya kujifurahisha au ya mafunzo ambayo mtu hutembelea maeneo fulani mashuhuri.Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka binadamu mfano miti, nyumba, milima, nk.

**Ufahamu**

**Soma habari ifuatayo kisha jibu**

Mwalimu Bakari anafundisha katika shule ya msingi Mawenzi, anafundisha somo la Kiswahili na pia ni mtaalamu wa somo la hisabati, shule ya mawenzi ipo mjini.

Siku moja mwalimu Bakari na wanafunzi wa darasa la sita walishauriana waandae ziara fupi. Walishauriana waende kituo cha usalama barabarani ili wapate elimu ya usalama barabarani.


Mwalimu Bakari aliandika barua kwa mkuu wa kituo cha usalama barabarani kuomba kwenda kujifunza elimu ya usalama barabarani. Mkuu wa kituo cha usalama barabarani alikubali ombi lao, na aliwaambia waende siku ya ijumaa. Mkuu huyo wa kituo cha usalama barabarani aliwaahidi kuwapa ushirikiano wa hali ya juu.

Mwalimu bakari aliwasisitiza wanafunzi kufua nguo zao na kuzipiga pasi ili siku ya ziara wawe nadhifu, pia mwalimu Bakari aliwaambia wanafunzi waandae maswali ya kuuliza siku ya ziara.

Siku ya ziara ilipofika wanafunzi wote waliwahi kufika shuleni, mwalimu Bakari aliwapa maelekezo kabla ya kuzuru kituo cha usalama barabarani, ilipofika saa tatu asubuhi mwalimu Bakari na wanafunzi wa darasa la sita walianza kutembea kuelekea kituo cha usalama barabarani. Punde si punde walifika kituo cha usalama barabarani, walimkuta mkuu wa kituo hicho akiwasubiri. Aliwapokea wanafunzi na mwalimu kwa ukarimu wa hali ya juu. Mkuu wa kituo cha usalama barabarani aliwatambulisha wanafunzi na mwalimu Bakari kwa wafanyakazi wenzake kituoni hapo.

Baada ya hapo mkuu wa kituo aliwakabidhi wanafunzi na mwalimu Bakari kwa askari wa usalama barabarani ili awafundishe. Askari huyo wa usalama barabarani aliwafundisha jinsi ya kuvuka barabara. Aliwaambia ni vema kuvuka barabara kwenye kivuko chenye alama za pundamilia, pia sehemu zenye taa wanatakiwa kuvuka taa nyekundu zinapowaka kwani wakati huo magarı huwa yamesimama.

Pia aliwaambia kuwa waangalifu wanapovuka sehemu zisizo na kivuko. Kwanza waangalie upande wa kulia kısha waangalie upande wa kushoto na kisha warudi kuangalia upande wa kulia tena pakiwa salama hakuna magari au magari yapo mbali ndipo wavuke. Asha alımuuliza askari wa usalama barabarani taa za kijani zina maana gani? askari huyo alimjibu taa hizo huruhusu magari kupita, mtembea kwa miguu haruhusiwi kuvuka muda huo.




Pia aliwasisitiza wanafunzi wanapokua barabarani wawe na nidhamu, wasicheze barabarani ni hatari kwani wanaweza kugongwa na magari. Baada ya kuwafundisha askari wa usalama barabarani aliwapeleka mwalimu Bakari na wanafunzi barabarani ili kujifunza kwa vitendo.

Walipomaliza kufundishwa mwalimu Bakari na wanafunzi walimshukuru sana mkuu wa kituo cha usalama barabarani pamoja na askari wa usalama barabarani aliyewafundisha, waliagana kwa furaha na wanafunzi na mwalimu Bakari.walirudi shuleni saa saba mchana.

**1. Ufahamu**

1. Mwalimu Bakari anafundisha shule gani?
    - ❖ Mwalimu Bakari anafundisha shule ya msingi Mawenzi

2. Mwalimu Bakari ni mtaalamu wa somo gani?

- ❖ Mwalimu Bakari ni mtaalamu wa somo la hisabati

3. Mwalimu Bakari alimuandikia nani barua?
   - ❖ Mwalimu bakari alimuandikia barua mkuu wa kituo cha usalama barabarani.

4. Kwenye ziara yao walijifunza nini?
   - ❖ Kwenye ziara yao walijifunza elimu ya usalama barabarani.

5. Askari wa usatama barabarani aliwaambia wavuke barabara kwenye alama gani?
   - ❖ Wavuke kwenye alama ya pundamilia

6. Askari aliwaambia taa nyekundu zina maana gani?
   - ❖ Askari alıwaambia taa nyekundu zikiwaka magari yanasimama hivyo waenda kwa miguu wanaruhusiwa kupita

7. Mwalimu Bakari na wanafunzi walirudi shuleni saa ngapi?
   - ❖ Mwalimu Bakari na wanafunzi walirudi shuleni saa saba mchana.

8. Ni wanafunzi wa darasa la ngapi walikwenda ziara?
   - ❖ Wanafunzi waliokwenda ziara ni wa darasa la sita.

**2. Msamiati**

**Oanısha maneno ya safu A na maana zake safu B**

| SAFU A | | SAFU B | |
|---|---|---|---|
| 1 | Kumbusha | A | Hali ya kuungana na kusaidiana katıka jambo |
| 2 | Zuru | B | Tabia njema aliyo nayo mtu katika jamii anayoishi |
| 3 | Ukarimu | C | Fanya mtu afanye jambo Fulani alilolisahau |
| 4 | Nidhamu | D | Enda mahali fulani kwa madhumui ya kutembea na kujifunza jambo au kuonana na mtu |
| 5 | Ushirikiano | E | Weka dhamira ya kutekeleza jambo fulani |
| 6 | Ahidi | F | Enye kupendeza au kuwa safi |
| 7 | Nadhifu | G | Hali ya mtu kuwa mwema |
| | | | |

**Majibu**

| | |
|---|---|
| 1 | C |
| 2 | D |
| 3 | G |
| 4 | B |
| 5 | A |

| | |
|---|---|
| 6 | E |
| 7 | F |

**3. Vitendawili**

**Tegua vitendawili vifuatavyo kwa kuandika jibu kwenye nafasi wazi**

1. Ajenga ingawa hana mikono - ndege
2. Akila yeye na mimi hushiba
3. Akiongea kila mtu hubabaika- radi
4. Finyanga vyungu vya dona – matonge ya chakula
5. Fimbo ya babu ina mafundo – muwa mama na mtoto tumboni
6. Fundi kimya haneni lolote – babu
7. Gari hili la ajabu hata lofa analo – miguu
8. Ghala lake limejaa punje za mahindi – kinywa
9. Gololi mbili zaenda mbio – macho
10. Hakikamatiki hakieleweki – moshi na kivuli
11. Hana haja ya kukaribishwa - nzi
12. Hata mzungu amezishindwa- kifo
13. Hausimami, hausimikwi - mkufu, kamba, uzi
14. Inama nikwambie – mwiba
15. Kaa hapa, name nikae pale tumfinye mchawi - kula ugali

4. Toa maana ya methali zifuatazo;

1. Adui wa mtu ni mtu______________________________

- Mtu hudhuriwa na wale walio karibu naye mabaya atendewayo mtu hufanywa na walewale anaoishi nao.

2. Akiba haiozi______________________________________

- Ni vizuri/muhimu kuweka akiba kwa faida ya baadaye ipo siku itakuja kukusaidia

3. Boriti ya nyumba ifupishie nyumbani_______________________

- Ufanyapo jambo hakikisha unachukua tahadhari kuepuka kukosea
- Kasoro za nyumbani zitatuliwe nyumbani wala si kuzisema nje

4. Cha kupewa hakishibishi___________________________________________

- Jambo unalopangiwa, kuahidiwa au kupewa haliwezi kukutosheleza kwani utapewa kulingana na kipimo cha mpaji.

5. Dawa si chungu, chungu ni maradhi____________________________________________

- Uwe tayari kuumia ili kupata ufumbuzi wa tatizo kwani madhara ya tatizo ni mabaya kuliko ugumu uupatao katika kulitatua.

6. Dawa ya moto ni moto_________________________________________

- Njia ya kukabiliana na mambo magumu ama mtu mkorofi ni kwa kusim-

**5 Mazoezi ya lugha**

**Bainisha neno ambalo ni tofauti na mengine katika orodha ifuatayo**

a) Kiti, meza, chakula, dawati, sora
b) Tembo, pundamilia, simba, faru, kuku
c) Soksi, bangili, hereni, mkufu,
d) Chungwa, parachichi, papai, nazi, nanası
e) Gari, pikipiki, baiskeli, meli, treni
f) Chaki, kitabu, mwalimu, kalamu, daftari
g) Mchicha, mahindi, kabichi, majani ya kunde, kisamvu
h) Mpera, mpapai, mpira, mchungwa, mchenza, mfenesi
i) Simu, gazeti, kikokotozi, televisheni, redio
j) Kuona, kupima, kunusa, kuonja

Andika wingi wa sentensi zifuatazo

i. Mwalimu aliniandalia
ziara Walimu walituandalia
ziara

ii. Mimi ninapenda kusoma hadithi
Sisi tunapenda kusoma hadithi

iii. Mwalimu alisoma risala
Walimu walisoma risala

iv. Mtoto anaimba wimbo mzuri
Watoto wanaimba nyimbo
nzuri

v. Mwanakijiji amejenga darasa la kusomea
Wanakijiji wamejenga madarasa ya
kusomea

vi. Ndugu yangu alisafiri jana

Ndugu zangu walisafiri jana

**Oanisha maneno yanayokaribiana kimaana kutoka safu A na E**

| | SAFU A | | SAFU B | | MAJIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| **1** | Jogoo | **A** | Mwisho | **1** | Q |
| **2** | Jokofu | **B** | Kasi | **2** | S |
| **3** | Hatimae | **C** | Treni | **3** | A |
| **4** | Ghasia | **D** | Hongo | **4** | P |
| **5** | Gari moshi | **E** | Ruhusa | **5** | C |
| **6** | Fukara | **F** | Mabaki | **6** | R |
| **7** | Hodari | **G** | Masumbwi | **7** | N |
| **8** | Idhini | **H** | Pombe | **8** | E |
| **9** | Samani | **I** | Kapteni | **9** | T |
| **10** | Rushwa | **J** | Kiongozi | **10** | D |
| **11** | Masalia | **K** | Maziwa mgado | **11** | F |
| **12** | Mbio | **L** | Jasiri | **12** | B |
| **13** | Ndondi | **M** | Gemo | **13** | G |
| **14** | Nahodha | **N** | Bingwa/gwiji | **14** | I |
| **15** | Mtindi | **O** | Danganya | **15** | K |
| **16** | Shujaa | **P** | Fujo | **16** | L |
| **17** | Laghai | **Q** | Jimbi | **17** | O |
| **18** | Korongo | **R** | Maskini | **18** | M |
| **19** | Kileo | **S** | Friji | **19** | H |
| **20** | Kiranja | **T** | Fanicha | **20** | J |

**Kushiriki katika mjadala kuhusu matumizi ya simu ya mdomo**
Simu za mdomo hufikisha ujumbe haraka kwa njia ya mazungumzo. Ujumbe wa simu za mdomo haupotei kwa sababu ni mawasiliano ya moja kwa moja.

**Ufahamu**
**Soma mjadala ufuatao kisha jibu maswali**
MUSA: Habari yako Juma
JUMA: Ni nzuri kabisa
MUSA: Nina swali ninataka kukuuliza
JUMA: Uliza tu Musa usiwe na wasiwasi kwani kuuliza si ujinga
MUSA: Mh! Hivi matumizi ya simu yana umuhimu gani katika jamii

JUMA: Matumizi ya simu yana umuhimu, kwanza husaidia watu wa sehemu mbalimbali kuwasiliana kwa muda mfupi tofauti na zamani, ilikuwa ni vigumu kuwasiliana na mfu wa mbali. Ilimlazimu mtu kufunga safari, pili matumizi ya simu hukuza uhusiano kwa watumiaji. Uhusiano huo waweza kuwa baina ya mtu na mtu au kikundi na kikundi. Vilevile simu hukuza uhusiano wa kimataifa kwa kupashana habari za kimataifa.

MUSA: Mh! asante rafiki yangu sasa nimeanza kuelewa Je, kwa upande wa elimu matumizi ya simu nayo yana umuhimu?

JUMA: Haswaa! Kwenye elimu pia husaidia kukuza ujuzi kupitia program za simu za video, makala mbalimbali na vitabu vinaweza kupakuliwa mtandaoni.

Mh! Musa sio kwenye elimu tu hata kwenye biashara wafanyabiashara huweza kutangaza bidhaa zao kupitia mitandao ya kijamii

MUSA: Kweli matumizi ya simu yana umuhimu sana

JUMA: Ni kweli kabisa katika nyanja mbalimbali matumizi ya simu ni muhimu. Hata kwenye huduma za kibenki watu hutuma na kutoa fedha na pia kuhifadhi katika simu. Pia simu huweka kumbukumbu na hii huwasaidia sana wafanyabiashara hata wasiokuwa wafanyabiashara waweze kuhifadhi kumbukumbu. Vilevile simu huburudisha zipo program za muziki na michezo mbalimbali ambayo humfanya mtu aburudike.

MUSA: Kweli faida zipo nyingi lakini kuna baadhi ya vitu huwa na faida na hasara. Je, matumizi ya simu yana hasara?

JUMA: Swali zuri, Musa hasara zipo kama mtu atatumia simu vibaya. Kwanza hupoteza muda wa kufanya kazi iwapo mtu atatumia muda mwingi kwenye simu kuwasiliana na kuangalia program mbalimbali zilizopo kwenye simu. Pia unaweza kuharibu macho pale unapotumia simu kwa muda mrefu na hasa kwenye giza, simu huwa na miale ya umeme inayotokana na mwanga wa simu. Vilevile matumizi ya simu ni gharama kwani bila kuweka fedha huwezi kupata huduma unayohitaji katika simu. Vilevile matumizi mabaya ya simu husababisha mmomonyoko wa maadili hasa kwa watoto na vijana. Watoto na vijana wanaharıbika kıtabıa kupitia matumızı ya simu, hasa kwa kuangalia program hatarishi zinazowekwa au zunazotumwa mtandaoni. Program hizo ni kama vile picha na video mbaya. Program hizi ni kinyume na maadili yetu.

MUSA: Mh ama kweli kizuri hakikosi kasoro ila jambo la msingi ni kutumia simu kwa matumizi sahihı. Kwanı simu ni muhimu hasa katika zama hizi za sayansi na teknolojia, kila mtu awe na nidhamu katika kutumia simu hizi.

JUMA: Ni kweli kabisa

MUSA: Asante Juma kwa kunielimisha

MWL.

**1. Ufahamu**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Majibizano uliyoyasoma yanahusu nini2

   Majibizano yanahusu umuhimu wa matumizı ya simu katıka jami

2. Wahusika katika majibizano hayo ni akina nani?

Wahusika ni Juma na Musa

3. Taja faida za simu kama zilivyoelezwa katika majadiliano hayo
- Husaidia kuwasiliana
- Hukuza uhusiano kwa watumiaji
- Husaidia kukupa ujuzi katika masuala mazima
- Husaidia kutangaza biashara na masoko kwa wafanya biashara.
- Husaidia kutunza kumbukumbu
- Huburudisha kupitia program za muziki na michezo mbalimbali katika simu
- Husaidia kuhifadhi, kutuma na kutoa fedha

4. Taja hasara za simu zikitumika vibaya
- Simu hupoteza muda mwingi wa kufanya shughuli za maendeleo
- Huharibu macho ukitumia kwa muda mrefu hasa kwenye giza kwani mwanga wake una miale ya umeme
- Hutumia gharama kubwa kwani ni lazima kuweka fedha ndipo upate huduma unayohitaji katika simu
- Pia husababisha mmomonyoko wa maadili hasa kwa watoto na vijana pale wanapoangalia program hatarishi.

**2. Msamiati**

**Tunga sentensi kwa kutumia msamiati ufuatao**

i. Mawasiliano
- ❖ Baba alıwaambia watoto wake ni vizuri wawe na mawasiliano mazuri ili waishi kwa upendo.

ii. Mtandao
- ❖ Simu ya mama yangu mtandao wake ni wa Tigo

iii. Program
- ❖ Mwalimu wa somo la kompyuta alıtufundısha program ya uchapaji matangazo

iv. Simu
- ❖ Dada yangu alipomaliza eimu ya juu mama alimnunulia simu

v. Nidhamu
- ❖ Mwalimu alītuambia mwanafunzi mwertye midhamu bolanya

**3. Miundo**

Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo

i)......................... kinagaubaga………………………………

- ❖ Juma aliongea na Musa kinagaubaga kuhusu umuhimuwa matumizi ya simu katika jamii

ii) ……………………baada ya …………………………………….

- ❖ Juma aliamka baada ya kuamshwa na mama yake

iii)........................... ..kimoyomoyo…………………………………

- ❖ Mwalimu aliwaambia wanafunzi wasome kimoyomoyo hadithi

iv)……………………..ili mradi………………………………...

- ❖ Manka alikwvenda shule ilimradi tu amfurahishe baba yake

v) ……………………ingawa……………………………..

- ❖ Hakushinda mchezo ule ingawa ni mzoefu.

**4. Methali**

**Malizia methali zifuatazo**

1. Akunyimae tonge - hakunyimi neno
2. Akufaaye kwa dhiki – ndiye rafiki
3. Baharia mvivu - huishia pondo mbovu
4. Baniani mbaya - kiatu chake dawa
5. Cha kuzama - hakina rubani
6. Cha mjinga - huliwa na mwerevu
7. Chururu - si ndo! ndo! ndo!
8. Dunia mtego wa panya - ukicheza utanasa
9. Dunia tambara bovu - ukivuta utalichana

5. Mazoezi ya Lugha

Andika umoja na wingi wa maneno yafuatayo

| | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| 1 | Chakula | Vyakula |
| 2 | Jiko | Meko |
| 3 | Mnazi | Minazi |
| 4 | Sukari | Sukari |
| 5 | Mto | Mito |
| 6 | Uzi | Nyuzi |
| 7 | Maji | Maji |
| 8 | Yai | Mayai |
| 9 | Mlima | Milima |
| 10 | kitabu | Vitabu |

**b. Kanusha sentensi zifuatazo**

1. Tutaandika Kiswahili
    - Hatutaandika Kiswahili.
2. Bibi ana duka la nguo
    - Bibi hana duka la nguo
3. Tutatoka hapa mapema
    - Hatutatoka hapa mapema
4. Ugonjwa huo ulimdhoofisha
    - Ugonjwa huo haukumdhoofisha
5. Manka atanunua simu
    - Manka hatanunua simu
6. Juma ni mfupi sana
    - Juma mfupi sana
7. Utafiti utakamilika mwakani
    - Utafiti hautakamilika mwakani
8. Daktari anatibu
    - Daktari hatıbu

**c. Andika neno moja linalojumuisha maneno uliyopewa**

1. Simba, chui, kifaru, tembo- **wanyama**
2. Mtama, mahindi, mchele, ngano - **nafaka**
3. Kware, kunguru, njiwa, bata, kuku – **ndege**
4. Kabati, meza, kiti - **samani**
5. Nanasi, chungwa, papai, parachichi - **matunda**
6. Jumatatu, jumanne, jumatano, alhamisi- **siku**

7. Kipindupindu, malaria, ebola, surua - **magonjwa**
8. Nanasi, cnungwa, papai, paracnicni - **matunda**
9. Jumatatu, jumanne, jumatano, alhamisi - **siku**
10. Kipindupindu, malaria, ebola, surua - **magonjwa**
11. Kaptula, shati, kanga, suruali – **mavazi**
12. Ôngea, zungumza, ujumbe, taarifa - **mawasiliano**
13. Arusha, Dodoma, Shinyanga, Mbeya - **mikoa**

**d. Andika kweli au sikweli**

1. Simu ni chombo cha mawasiliano - **kweli**
2. Simu ikitumika vibaya yaweza kusababisha mmomonyoko wa maadili – **kweli**
3. 11i. Simu hazina faida yoyote katika jamii **- si kweli**
4. Simu inaweza kutumika kwa kupiga picha - **kweli**
5. V. Mwanafunzi mwenye nidhamu hawezi kufaulu - **sı kweli**
6. Mtumiaji wa simu hapaswi kuweka fedha kwenye simu yake ili kupata huduma anayohitaji katika simu - **si kweli**
7. Mwanafunzi mwema hufanya kazi kwa kusimamiwa **– si kweli**
8. Simu hutumika baina ya watu walio karibu tu – **si kweli**
9. 1X. Matumizı ya simu yana faida na hasara - **kweli**

**e. Andika umoja wa sentensi zifuatazo**

1. Watete wanejua
kucheza Mtoto anajua
kucheza
2. Ng'ombe wamekamuliwa
maziwa Ngombe amekamuliwa
maziwa
3. Sisi ni wanafunzi wa darasa la sita'
Mimi ni mwanafunzi wa darasa la
sita
4. Sisi ni mafundi wa kutengeneza
meko Mimi ni fundi wa kutengeneza
jiko
5. Tunasoma shule ya msingi Fuka
Ninasoma shule ya msingi Fuka
6. Walimu wetu hawapendi kelele
Mwalimu wangu hapendi
kelele
7. Kuta zimeanguka
Ukuta
umeanguka
8. Wale watanunua
matunda Yule atanunua

MWL

tunda

9. Kakakuona ni wanyama wa ajabu Kakakuona ni mnyama wa ajabu.

**f. Onanisha maneno ya safu A na safu B.**

| | Safu A | | Safu B |
|---|---|---|---|
| 1 | Simu | A | Kiwango cha juu cha uvumbuzi wa kisayansi |
| 2 | Kimoyomoyo | B | Kituo maalumu na rasmi kinachojihusisha na shughuli za kijamii |
| 3 | Teknolojia | C | Kuongea na nafsi yako bila kutoa sauti |
| 4 | Taasisi | D | Kifaa kinachotumika kuchapa na kuhifadhi kumbukumbu kwenye nakala laini |
| 5 | Kompyuta | E | Kifaa kitumwacho na watu walio katika maeneo tofauti kupashana habari. |

WA

Majibu:
1. E
2. C
3. A
4 B
5. D

**g. Andika ujumbe mfupi wa simu wenye maneno yasiyozidi kumi na sita kuhusu kuomba nauli ya kurudi nyumbani likizo.**

Shikamoo baba mimi ni mzima tutafunga shule mwezi wa sita nitumie nauli Sauda.

**Kutumia msamiati katika kuzungumza kwa kuwasilisha hoja kulingana na miktadha mbalimbali**

**Kubaini aia saba za maneno katika sentensi (Nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kiwakilishi, kiunganishi na kihisishi)**

Neno/maneno ni mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa ambazo huwa na maana mfano mwa- li-mu- mwalimu.
Sentensi ni kıpashio cha juu kabisa katika tungo yenye muundo wa kiima na kiarifu na pia huwa na maana Mfano: Baba analima na mama anafua

**1. Nomino (N)**
Nomino ni maneno yanayotaja watu, vitu, hali na mahali, nomiito hutokea kwenye umbo la umoja au wingi. Mfano: Mtoto anacheza. Neno mtoto ni nomino

**Aina za nomino**

**1. Nomino za pekee**

Nomino za pekee hutaja na kutambulisha nomino mahsusi na za kipekee. Yaani kuwa kitu ni hicho na wala si kingine chochote. Hizi ni nomino zinazohusisha majina ya watu, nchi, miji, milima, maziwa na bahari. Herufi za mwanzo za nomino za pekee huwa ni kubwa hata kama nomino hiyo inapatikana katikati ya sentensi.

**2. Nomino za kawaida**

Hizi kwa jina jingine huitwa nomino za jumla. Nomino za kawaida ni majina ya viumbe kama vile wanyama, miti, watu, ndege, wadudu n.k. Ni majina ya vitu vyenye umbo la namna moja mfano; Baba, dada, shangazi, nyoka, simba, kiti, n.k nomino hizo si maalumu kwa vitu fulani tu bali ni za vitu mbalimbali vya aina hiyo kama nomino "baba" linatumiwa na watu wengi na wala sio maalum kwa mtu mmoja tu, kwa hali hii twaweza kuona baba wengi. Nomino zote za aina hii huanza kuandikwa kwa herufi ndogo, isipokuwa kama neno linakua mwanzoni mwa sentensi.

**3. Nomino za jamii**

Hizi ni nomino zinazowakilisha vitu vingi katika jina moja yaani nomino zinazotaja jumla ya vitu vingi mfano; Jeshi, bunge, kamati, halaiki, n.k.

**4. Nomino za dhahania**

Hizi ni nomino za dhana zinazofikiriwa tu pasipo kuonekana mfano Mungu, malaika, zimwi, shetani.

**5. Nomino za kitenzi jina**

Hizi ni nomino zinazohusu vitenzi huundwa kwa kuongezwa kiambishi (Ku) cha unominishaji kwenye mzizi wa kitenzi cha kitendo halisi ili kukifanya kiwe nomino, mfano kitenzi soma nomino kusoma.

**Zoezi**

**Bainisha nomino katika sentensi zifuatazo**

1. Mwalimu anafundisha
    - ❖ Nomino ni mwalimu

2. Kuimba kwake kumetufurahisha
    - ❖ Nomino ni kuimba

3. Baba amenunua shamba
    - ❖ Nomino ni baba na shamba
4. Ngoma ilipigwa usiku kucha
    - ❖ Nomino ni ngoma

5. Mjomba alinunua mkate, machungwa na malimao
    - Nomino ni mjomba, mkate, machungwa na malimao

6. Jeshi linapigana
    - Nomino ni jeshi

7. Bustani ina matunda mengi
    - Nomino ni bustani na matunda

8. Bibi anafua nguo
    - Nomino ni bibi na nguo

9. Mungu ni mzuri
    - Nomino ni Mungu

10. Darasa lina wanafunzi wengi
    - Nomino ni darasa na wanafunzi

**2. Vivumishi (V)**

- Vivumishi ni maneno yanayoelezea zaidi nomino aghalabu vivumishi hutanguliwa na nomino. Mfano; Mtoto mzuri analia neno mzuri ni kivumishi

**Aina za vivumishi**

**1. Vivumishi vya sifa**

Vivumishi hivi hutoa sifa za nomino au kiwakilishi cha nomino sifa hizi huweza kuwa nzuri au mbaya

Mfano: Mwanafunzi **mtiifu** amefaulu

Mti **mrefu** umeanguka

**2. Vivumishi vya idadi**

Vivumishi vya aina hii hutoa taarifa kuhusu idadi ya nomino

Mfano: Watoto **watatu** wamefaulu

Watu **wachache** tu wamepewa msaada

**3. Vivumishi vya kumiliki**

Ni vivumishi vinavyoonesha kuwa kitu fulani kinamilikiwa na mtu aidha huonesha umiliki wanomino.

Mfano: Mtoto **wangu** ni mrembo
Nyumba **yetu** imejengwa kwa matofali ya kuchoma

**4. Vivumishi vioneshi**

Vivumishi hivi huonesha mahali au upande kitu kilipo vivumishi hivi hutegemea umbali na ukaribu.

Mfano: Kijana **yule** ni mkorofi
Nazi **zile** zimeharibika
Mtoto **huyu** ni mtulivu

**5. Vivumishi vya kuuliza**

Hivi ni vivumishi ambavyo hufafanua nomino kwa kuuliza habari zake. Hujibu swali gani? Ipi? Ngapi?

Mfano: Watu **wangapi** wamefarıki
Mwanfunzi **gani** anaandika vizuri
Mwanafunzi **yupi** hakufanya usafi

**6. Vivumishi vya a- unganifu**

Haya ni maneno yanayotumika kueleza hali au matumizi ya kitu ili kutofautisha kitu kinachozungumzwa na vitu vingine vya aina hiyo

Mfano: Nguo ya baba
Chakula cha mgonjwa
Jeshi la polisi

**7. Vivumishi jina kwa jina**

Hızi ni nomino zinazotumika kama vivumishi ambazo hutumika kufafanua nomino. Au hizi ni nomino zinazovumisha nomino nyingine.

Mfano: Askari **polisi** ameanguka
Mwalimu **Juma** amepewa zawadi
Kijana **mlemavu** amekwenda hospitatin

**8. Vivumishi vya pekee**

Haya ni maneno yanayoonesha ziada au msisitizo uliowekwa katika nomino iliyovumishwa

Mfano: Majani **yote** yamekauka
Mtu **yeyote** asiingie
Kiasi **chochote** cha fedha kitanitosha

**Zoezi**

**Bainisha vivumishi katika sentensi zifuatazo**

1. Panya **wengi** wameingia shimoni
2. Watoto **wazuri** wanapanda ngazi

3. Wanafunzi **watano** wamefaulu mitihani
4. Mtote **wangu**-amemaliza shule
5. Ndege **mzuri** alituburudisha kwa nyimbo **zake**
6. Mlima **mrefu** ni Kilimanjaro
7. Chungwa **kubwa** limeoza
8. Duka la dawa **ndilo** linalotakiwa katika kijiji chetu
9. Askari polisi amemkamata jambazi mmoja juzi usiku
10. Musa amekula chakula **chote**
11. Kuku **wawili** wameatamia
12. Kijiji **chetu** kina zahanati **nzuri** sana
13. Mwanafunzi **mtiifu** amepata zawadi
14. Mama ni **hodari** wa kupika chapatti
15. Wanafunzi **wengine** wafagie uwanja
16. Mwenge wa **uhuru** umefika Kinondoni
17. Yeye **mwenyewe** amefaulu

**3. Viwakilishi (W)**

Ni maneno yanayotumiwa baada ya nomino, viwakilishi huwakilisha nomino, hivyo huweza kutokea katika sentensi pale tu ambapo nomino haipo

Mfano: **Yule** anaumwa tumbo

**Huyu** anadeka

**A: Aina za viwakilishi**

**Viwakilishi vioneshi au viwakilishi vya kuonesha**

Viwakilishi hivi hutumika badala ya nomino kwa kutumia kuonesha nomino inayorejelewa bila kuitaja mfano huyu, yule, hapo, humo.

**Huyu** si mwenzetu kabisa

**Kule** kunafuka moshi

**Wale** ni watoto

**Huu** ni mti wa kivuli

**B. Viwakilishi vya nafsi**

Hivi husimama badala ya nomino zinazotaja nafsi za watu katika Kiswahili nafsi hugawanyika katika makundi matatu

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| Nafsi I | Mimi | Sisi |
| Nafsi II | Wewe | Ninyi |
| Nafsi III | Yeye | Wao |

**Mfano:**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Wewe unasemaje? | Ninyi mnasemaje? |
| Mimi nafua | Sisi tunafua |
| Yeye ataandika | Wao wataandika |

**C. Viwakilishi vya kuuliza**

Hivi ni viwakilishi vinavyouliza maswali

Mfano: **Wangapi** wamefika leo
**Yupi** ameanguka
**Wapi** wamekwenda
**Kipi** kimevunjika

**D. Viwakilisbhi vya urejeshi**

Hivi ni viwakilishi vinavyojengwa na shina amba pamoja na viambishi ngeli vyenye O-rejeshi.

Pia hujengwa na vipande vidogovidogo - ye- cho - vyo- lo-

Mfano: **Aliyeondoka** hatapewa chake
**Ambacho** kimevunjika ni hiki
**Ambaye** ameokota arudishe

**E. Viwakilishi vya idadi**

Viwakilishi hivi hutuarifu kuhusu idadi ya nomino huweza kuwa kamili au ya jumla

Mfano: **Watano** wameondoka
**Kidogo** kihifadhiwe
**Lukuki** wamehudhuria

**F. Viwakilishi vya pekee/vimilikishi**

Hivi ni viwakılishi vya pekee kuwakilisha nomino hufuata sheria za upatanisho za nomino zinazowakilishwa mfano - angu - ako - etu - enu – ao

Mfano: Kwangu haingii mdudu
**Chetu** kimekamilika
**Chenu** kimeoza
**Chako** hakina thamani

**G. Viwakilishi vya a-unganifu**

Haya ni maneno ya sifa yanayohusisha sifa na nomino inayosifiwa kwa kutumia a-unganifu. Nomino yenye sifa hiyo haitajwi katika sentensi hiyo

Mfano: **Wa** kwanza aje hapa
**La** saba wamefungwa
**Wa** mwisho kaondoka

**H. Viwakilishi vya sifa**

Hivi huonesha sifa fulani ya nomino zinazowakilisha

Mfano: **Weupe** waje mbele
**Wajanja** waondoke
**Wafupi** wasimame

**Zoezi**

**Bainisha viwakilishi katika sentensi zifuatazo**

1. Wawili zaidi wamekamatwa
2. Mwenyewe kaondoka
3. Wao wameamua kupigana
4. Sisi tunakabiliwa na uhaba wa chakula
5. Ambaye hajaondoka aje mbele
6. Lukuki wamekuja mkutanoni
7. La saba wamemaliza mitihani yao
8. Yeye ameamua kuja
9. Ambalo limeandikwa halibadilishwi
10. Yupiameanguka?
11. Ninyi mmeondoka
12. Chake kimeharibika kabisa
13. Wafupi wasimame
14. Wa mwisho aje mbele

MWL

**1. Vitenzi**

Vitenzi ni aina ya maneno yanayotumika katika sentensi kuarifu na kueleza jambo ili sentensi ikamilike. Mfano cheza, lima, andika, n k.

Mfano: Baba **analima** bustani

**Aina za vitenzi**

**A. Kitenzi kikuu (T)**

Vitenzi vikuu ni vile ambavyo hubeba ujumbe muhimu wa kiarifu cha sentensi. Au hueleza tendo lililofanywa na mtenda au alilofanyiwa mtendwa, wakati wa tendo hilo lilipofanyika, hali ya tendon a tendo na kauli ya tendo.

Mfano: Baba **anafua** nguo
Wanafunzi **watasoma** hadithi
Fatuma **anacheza** mpira

**B. Kitenzi kisaidizi (Ts)**

Vitenzi hivi hutoa taarifa ya kusaidia vitenzi vikuu hutoa taarifa kama vile uwezekano, wakati, hali n.k. Vitenzi visaidizi daima hutumika na vitenzi vikuu ndivyo vinavyobeba viambishi vya wakati.

Mfano: Baba **alikuwa** anakunywa.chai.
Mtoto **aliyekuwa** anapika ameondoka Juma **ataweza** kuchota maji

**C. Vitenzi vishirikishi (t)**

Vitenzi vishirikishi (t) haya ni maneno yanayoonesha hali fulani iliyopo au isiyokuwepo katika mazingira ya aina moja.

Mfano: Asha **ni** mtoto mtiifu
Huyu **si** mwimbaji

**Zoezi**

**Bainisha vitenzi katika sentensi zifuatazo**

1. Mama **anasoma** gazeti
**T.**

**2.** Baba **anafua** na mama **anapika**
**T.** **T.**

3. Mzee **uliyemwona akitembea** kwa madaha ni mjomba wangu Ts

4. Ebola **ni** ugonjwa hatari sana
**t**

5. Huyu **si** mwindaji haramu
**t**

6. Ugali **ni** mtamu
**t**

7. Juma **anacheza** mpira wa kikapu
**T**

8. **Kucheza** kwao kulituburudisha
**T**

9 **Aliyeweza kucheza** vizuri alipewa zawadi
**Ts.** **T**

10. Chakula hicho **si** kitamu
**t**

12. Baba **anampikia** mama ugali
**T**

13. Mtoto mpole **anacheza** vizuri
**T**

14. Mama **amewasili** kutoka Moshi
**T**

**2. VIelezi (E)**

Haya ni maneno yanayofafanua vitenzi, vivumishi au vielezi vingine. Huweza kuarifu kitendo kilichotendeka, kilitendeka wapi namna gani na hata mara ngapi.

Mfano: Mtoto anacheza **vizuri**
Mtoto anacheza **sana**
Juma alikuwa mrefu **sana**
Kijana aliruka mbali **sana**
Aliona mvulana mfupi **sana**

**Aina za-vielezi**

**A. Vielezi vya mahali**

Vielezi vya mahali hutoa habari kuhusu mahali ambapo kitendo kilifanyika aghalabu vielezi hivi huundwa kwa kutumia jina la mahali au kwa kuongeza kiungo ni mwishoni mwa neno linaloashiria mahali mfano shuleni, shambani n.k

Mfano: Mama amekwenda **shambani**
Watoto wanaimba **darasani**
Shati lipo **kabatini**
Msipite **sokoni** mkienda **kanisani**

***B. Vielezi vya wakati***

Vielezi hivi huelezea zaidi kuhusu wakati kitendo kinapofanyika mfano; jioni, jana, asubuhi, saa sita, mwaka ujao.

Mfano: Musa na Juma watakutana **kesho**
Ndege itaondoka **saa sita usiku**
Nitafua nguo **mwaka ujao**

**C. Vielezi vya idadi**

Vielezi hivi huelezea kitendo kilifanyika mara ngapi, vielezi hivi navyo vimegawanyika katika makundi mawili

**i) Idadi kamili Vielezi**

idadi kamili hutaja idadi kamili ya mara ngapi kitendo kilifanyika mfano mara mbili, siku tatu, kwa juma n.k

Mfano: Mtoto anaoga **mara mbili**
Daktarı alımwagiza mama anywe dawa **mara tatu kwa siku** na arudi kliniki **mara moja kwa mwezi**.

**ii) Idadi isiyodhihirika**

Vielezi hivi huelezea kiasi ambacho kitendo kilifanyika bila kutaja kiasi kamili mfano; chache, nyingi, kadhaa, wastanı, n.k

Mfano: Alianguka **mara kadhaa** kabla ya kufika
Dada hunipigia simu **mara kwa mara**
Tuligombana **mara nyingi**

**D. Vielezi vya maana au jinsi**

Vielezi hivi huelezea jinsi au namna tendo linavyofanyika

Mfano Juma anatembea **haraka haraka**
Wanacheza **kihuni**
Anaandika **vizuri**

MWL

**E.Vielezi viulizi**

Hivi ni vielezi ambavyo huuliza juu ya tendo lilifanyika lini, wapi namna gani n k.

Mfano: Juma anasoma shule **gani?**
Asha atarudi **lini?**
Watoto wanasoma **wapi?**
Mtoto alishinda **vipi?**
Mama amenunua **nini?**

**Zoezi**

**Bainisha vielezi vyote katika sentensi zifuatazo**

1. Asha anatembea kizembe

2. Watoto wanaimba vizuri sana
3. Babu yako anauza nini?
4. Mteja huyu hununua nguo mara nyingi
5. Mtoto anaoga mara mbili
6. Mshauri mzuri huwashauri wateja wake vyema
7. Baba amekwenda shambani
8. Ataondoka mwezi ujao
9. Daktari atafika kesho kutwa
10. Takataka zimetupwa jalalani
11. Kinyonga hutembea polepole
12. Kaa anakwenda upande upande
13. Alicheza na kuimba vizuri
14. Gari lilitumbukia mtoni taratibu
15. Panya mdogo ameingia shimoni
16. Dereva alimkwepa mlevi darajani
17. Simba ananguruma sana
18. Maji yamejaa pomoni
19. Vitabu vyote vilionekana vizuri
20. Lugha za kigeni hufundishwa sana shuleni

**6. Viunganishi (U)**

Kiunganishi ni neno au kikundi cha maneno chenye kuunganisha maneno katıka sentensi kama vile nomino na nomino, kitenzi na kitenzi n k

Mfano: Kitenzi **na** kitenzi

Kula **na** kunywa

Cheza **na** rukaruka

Nomino **na** nomino

Baba **na** mama

Uji **na** mgonjwa

Kalamu **na** daftari

Sentensi **na** sentensi

Baba analima **na** mama anapika

Mtoto analia **lakini** manma anafua

MWL

**Aina za viunganishi**

**A. Viunganishi huru**

Viunganishi hivi ni viunganishi vinavyosimama pekee katika tungo (sentensi) katikati ya vipashio vinavyoungwa.

Mfano: Baba na mama wamekwenda shambani

Alifua nguo kisha akazianika
Alikwenda ingawa hakupenda

**B. Viunganishi tegemezi**

Hivi ni viunganishi ambavyo huundwa kwa viambishi vya 0-rejeshi vinavyowekwa katikati ya kishazi huru kwa pamoja huunda sentensi changamano. Viambishi hivyo ni po- ye- cho-

Mfano: Mama anayepika **ni** msusi

**Zoezi**

**Bainisha viunganishi katika sentensi zifu atazo**

1. Kitabu chake kimepotea **lakini** cha Juma hakijapotea
2. Nitachelewa **kwasababu** nina kazi
3. Alimpiga Asha **tena** akampiga na Zaria
4. Yeye **ni** mtukutu **tena** mkorofi
5. Baba huyo **na** watoto wake
6. Mama atafua **kisha** atapiga pasi
7. Amekuja **ingawa** anaumwa
8. Aliyeondoka **ni** mwalimu
9. Sitakuja **kwa vile** sikualikwa
10. Anaimba **na** kucheza
11. Mkumbatie **lakini** usimbusu
12. Mwalimu aliuliza swali **wakati** yeye amesinzia
13. Huruhusiwi kuingia ofisini **hadi** saa sita
14. Fausta alikuwa **miongon**i mwa wanafunzi kumi bora
15. Naweza kwenda nyumbani **au** shuleni

**7. Vihisishi (1)**

Haya ni maneno ambayo hutumiwa kuwaklioha

Mfano**: Loo!** Maji yamemwagika
**Uwii!** Nimechelewa kanisani
**Ahaaa!** Ameumia mguu
**Eboo!** Huna macho

**Zoezi**

**Jaza nafasi wazi kwa kutumia vihisishi vifuatavyo: Loo! Uuwi! Kumbe! Ahaa!**

1. ____________________Nimechelewa kanisa
2. ____________________Nimekuona ukiiba
3. ____________________hivi nae alikuwepo

4. ____________________Hana hata aibu
5. ____________________ndio waliokunywa uji wa mtoto

**Majibu-**

1. Uwii!
2. Ahaa!
3. Ahaa!
4. Loo!
5. Kumbe!

**8. Vihusishi (II)**

Haya ni maneno yanayoonesha uhusiano baina ya neno moja na jingine au baina ya kıkundi cha maneno na kıngıne, vihusishi aghalabu huonesha uhusiano katı ya nomno na maneno mengine.

Mfano: Amekuja **kwa** miguu
Watacheza **katikati** ya uwanja

Dhima ya vihusishi inaingiliana na ile ya viunganishi kwani baadhi ya maneno yana dhima zote mbili katika sentens.

Mfano: Amepigwa **na** baba
Mtakwenda **kwa** miguu
Nitafika **kwa** Juma
Amekula **kwa** kijiko

Neno "kwa" katika sentensi hizi haliungi maneno bali huonesha uhu8iano uliopo kati ya kwenda na miguu na kati ya kufika kwa Juma

Mambo yanayoweza kuoneshwa kwa vihusishi (H)

i) Huonesha uhusiano wa kiwakati

❖ Mfano: Ni vizuri kupiga mswaki **baada ya** kula

ii) Huonesha uhusiano wa mahali

❖ Mfano: Ninaishi **karibu na** kanisa

iii) Huonesha uhusiano wa kulinganisha

❖ Amekula **zaidi ya** uwezo wake

iv) Huonesha uhusiano wa umilikaji

❖ Kitabu hiki ni **cha kwangu**

v) Huonesha uhusiano wa sababu

- ❖ Nimerudi kwa **ajili ya** kuonana na daktari

**Zoezi**

**Jaza nafasi zilizowazi kwa kutumia neno kwa au "na"**

1. Alipanda basi__________ rafiki yake
2. Anatembea___________miguu kuelekea mjini
3. Darasani kuna meza_____________madawati
4. Tulichinja kuku______________kuwa tulipata wageni
5. Juma anakula wali_________________kijiko

**Majibu**

1. Na
2. Kwa
3. Na
4. Kwa
5. Kwa

**Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali**

Wazazi wangu ni wakulima. Walianza kulima shamba dogo karibu na nyumba yetu. Shamba hilo lilitoa mazao kidogo sana na ambayo hayakutosha kwa chakula Baadaye walipata shamba kubwa bondeni. Wakalima mpunga na mahindi wakavuna kiasi kikuhwa.cha nafaka hizi.

**Maswali**

Kutokana na kifungu cha habari uliyosoma andika maneno mawili kwa kila kundi la maneno lililoorodheshwa

1) Nomino - Wazazi, wakulima, nyumba, shamba, chakula
2) Vitenzi – kulima, wakalima, wakavuna
3) Vielezi - bondeni, sana
4) Vivumishi – wangu, dogo, yetu.

**Tunga sentensi yenye vipashio vifuatavyo**

i) W+ Ts+ T+ E
Huyo uliyemwona alicheza vizuri

ii) N+ V+ V+ T+ N+ E
Kijana mfupi mweusi anacheza mpira vizuri

iii) N+ V+ E+ T+ N+ V+ E
Mtoto mzuri sana analima shamba lake
vizuri

iv) N+ V+ T+ E
Kijana mrefu anacheza mpira
vizuri

**Onesha aina za maneno yanayounda sentensi zifuatazo**

1. Viti vyetu vimetengenezwa
vizuri N V T
E

2. Mama amekwenda shambani
N. T E

3. Mzee uliyemwona akicheza na kuimba ni mjomba
wangu N Ts T U T t N
N

4. Mtoto mpole
ameanguka N T E

5. Juma anakula kwa
kijiko N T H
N

6. Aisee!
Umeanguka I
T

7. Mtoto mzuri anaimba
vizuri N V T
E

8. Yupi
ameondoka W
T

9. Alicheza na kuimba
vizuri T U T
E

10. Uji ulimwagika
mwaa! N T
I

11. Juma anakula chakula kwa
kijiko N T N H
N

**Kueleza na kubaini maneno mapya katika risala iliyowasilishwa**

**Risala** ni taarifa fupi inayosomwa mbele ya kiongozi mgeni rasmi kwa niaba ya kundi fulani la watu ili kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi. Ni aina ya taarifa ambayo hupelekwa na mtu au watu fulani inayoelezea haja inayotakiwa. Risala imegawanyika katika sehemu kuu tatu nazo ni:

1. Mwanzo; hapa panahusu sana salamu, ukaribisho na lengo la risala
2. Kati, hapa ndio kiini cha risala ambacho huonesha mafanikio matatizo manendekezo n.k.
3. Mwisho; hapa husisitiza maudhui ya risala pamoja na shukrani

**Risala ya wahitimu wa darasa la saba kwa mgeni rasmi**

Ndugu mgeni rasmi, walimu, wazazi, wanafunzi wenzetu, wageni waalikwa, mabibi na mabwana, tunayo furaha kukualika leo katika shule yetu ya msingi Ivaeni, ili usheherekee pamoja nasi katika mahafalı haya ya darasa la saba.

Ndugu mgenı rasmi, awalı ya yote tunapenda kutoa shukrani kwa uongozi mzima wa shule yetu Ivaeni, kwani wamekua wazazi bora waliotuongoza katika misingi imara. Misingi ambayo itatusaidia hata baada ya kumaliza elimu yetu ya msingi.

Ndugu mgeni rasmi tulianza darasa la kwanza tukiwa wanafunzi hamsini na tano. Lakini kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo utoro na vifo tumebaki wanafunzi arobaini na tano wasichana wakiwa thelathini na wavulana kumi na tano.

Ndugu mgeni rasmi miongoni mwa mafanikio tuliyonayo katika shule yetu ni umiliki wa mradi wa miti ya matunda. Mradi huu umetusaidia kuweza kupata matunda katika mlo tuupatao hapa shuleni na hivyo kupelekea kuwa na afya bora.

Ndugu mgeni rasmi mafanikio mengine ni uwezo wetu mkubwa kitaaluma, ni kweli kwamba uwepo wa walimu bora ndiyo imekua sababu ya shule yetu kushika nafası ya kwanza katika mitihani yote ya kujipima tunayoifanya katika mkoa wetu wa Kilimanjaro. Achilia mbali kuwa wa kwanza tumepata maarifa stahiki ambayo yatatusaidia kupambana na changamoto mbalimbali zilizopo kwenye jamii yetu.

Ndugu mgeni rasmi mbalı na mafanikio hayo kuna changamoto kadhaa ambazo zimekua zikitusumbua. Miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa maktaba kwa ajili ya wanafunzi kujipatia maarifa zaidi. Tatizo hili limetufanya tushindwe kupata maarifa zaidi ambayo hupatikana katika vitabu na makala mbalımbali nje ya vile vya darasani. Hivyo inatulazimu kutegemea maarifa kutoka kwenye vitabu vya darasani tuu. Vilevile ukosefu wa vitabu vya kutosha kwani kitabu kimoja huchangiwa na wanafunzi watano, na kutufanyva tusome kwa shida.

Ndugu mgeni rasmi ni matumaini yetu kuwa mafanikio yetu na changamoto zetu umezisıkia na utazıfanyia kazi kadrı ya uwezo wako ili shule yetu ya Ivaeni iendelee kung'aa na kushika nafasi za juu kimkoa na hatimae kitaifa.

Ndugu mgeni rasmi tunashukuru sana kwa kufika hapa kujumuika pamoja nasi japo una majukumu mengi, asante na karibu sana.

Jibu maswali yafuatayo

1. Risala hii ilitolewa na wanafunzi wa darasa la ngapi kwenda kwa mgeni rasmi?
   - Risala hii ilitolewa na wanafunzi wa darasa la saba kwenda kwa mgeni rasmi.

2. Risala hii ilitolewa na wanafunzi wa shule gani?
   - Risala hii ilitolewa na wanafunzi wa shule ya msingiivaenr

3. Shule ina mradi gani?
   - Shule ina mradi wa miti ya matunda

4. Ni changamoto zipi shule inakabiliana nazo?
   - Shule ina changamoto ya maktaba kwa ajili ya wanafunzi kujisomea ili kupata maarifa zaidi.
   - Pia shule ina changamoto ya vitabu kwani kitabu kimoja kinachangiwa na wanafunzi watano.
5. Tatizo la uhaba wa vitabu na maktaba vinaathiri vipi ujifunzaji wao?
   - Uhaba wa vitabu unapelekea wanafunzi kusoma kwa shida na pia ukosefu wa maktaba hufanya wanafunzi wakose maarifa zaidi.

**Toa maana ya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi**

**1. Mheshimiwa**
   - Neno la heshima linalotamkwa kabla ya kutaja jina la mtu maarufu mfano mtu mwenye wadhifa
   - Sentenst Mheshimiwa waziri alihutubia mkutano katika kijiji chetu

2. Mradi
   - Shughuli au biashara fulani inayomuingizia mtu kipato, jambo au hoja inayotakiwa kupatikana au mpango fulani wa maendeleo.
   - Sentensi: Baba na mama walinzisha mradi wa kulima mboga mboga

3. Maktaba
   - Nyumba au chumba mnamohifadhiwa machapisho ambamo watu huruhusiwa kuyatumia au kuyaazıma kwa muda au mkusanyiko wa machapisho kama vitabu, kanda, n k. yaliyohifadhiwa na ambayo huweza kuazimwa.

- Sentensi: Mwalimu wa somo la Kiswahili alitupeleka kuzuru maktaba

**4. Mahafali**
- Mkusanyiko mkubwa kwa ajili ya sherehe ya kutunuku vyeti kama vile shahada au stashahada n k.
- Sentensi: Jirani yetu alitualika kwenye mahafali ya mtoto wake aliyetunukiwa shahada ya uzamili.

**5. Taaluma**
- Ni elimu inayopatikana kwa kujifunza au kufundishwa
- Sentensi: Dada yangu ana taaluma ya udaktari

**6. Miliki**
- Jumla ya mali aliyonayo mtu au shirika fulani
- Sentensi: Mama yangu anamiliki ekari tano za miti ya mbao

**7. Uhaba**
- Halı ya kutopatikana kwa wingi au kwa idadi ya kutosha, uchache
- Sentensi. Kijiji chetu kina uhaba wa maji

**Mazoezi ya lugha**
**Andika kinyume cha maneno yafuatayo**
1. Tema - meza
2. Haribu – tengeneza
3. Kataza - ruhusu
4. Furaha - huzuni
5. Faida - hasara
6. Nuru – giza
7. Mwalimu – mwanafunzi
8. Mchana – usiku
9. Kumbuka- sahau
10. Ezeka - ezua
11. Kusanya – tawanya
12. Shibe - njaa
13. Chungu – tamu
14. Injika – epua

MWL

**Panga sentensi zifuatazo ili zilete mtiririko sahihi**
1. Alijibanza kwenye kona ya ofisi akivizia mwalimu atoke darasani
2. Kidasharı alichelewa kuamka, jambo lililomfanya achelewe kufika shuleni

3. Alipotoka tu kidashari akaingia
4. Na kweli alinofika muvalmu wa Kiswahili alikua ameshaanza kufundısha
5. Alianza safari ya kwenda shuleni akijua wazi kwamba atamkuta mwalimu darasani

**Majibu**

1. Kidashari alichelewa kuamka, jambo lililomfanya achelewe kufika shuleni
2. Alianza safari ya kwenda shuleni akijua wazi kwamba atamkuta mwalimu darasani
3. Na kweli alipofika mwalimu wa Kiswahili alikua ameshaanza kufundisha
4. Alijibanza kwenye kona ya ofisi akivizia mwalimu atoke darasani
5. Alipotoka tu kidashari akaingia

**Andika maneno mengine yenye maana zinazofanana**

1. Chumvi – Munyu
2. Bure - bwerere
3. Geza - 1ga
4. Mvulana – mvuli
5. Msichana – binti
6. Mtima - moyo
7. Barua - waraka
8. Waza - fikiri
9. Jela - gereza
10. Dhiki – shida
11. Idhini – ruhusa
12. Maringo - madaha
13. Magonjwa – maradhi
14. Ajuza – kikongwe
15. Nyanya - bibi
16. Kenda - tisa
17. Mama - nina
18. Soka - kandanda
19. Ugali - sima

**Bainisha neno lisiloendana na maneno mengine katika kila kifungu cha maneno**

1. Embe, ndizi, **mtama,** tikiti
2. **Rambirambi,** kibarua, kazi, ajira
3. Mwalimu, **runinga,** shule, kitabu
4. Dawa, **posta,** tabibu, hospital, mkunga
5. Msururu, **duara,** mstari, foleni
6. Ugali, wali, mihogo, **maharage**

7. Januari, machi, disemba, **alhamisi**
8. ***Kiti***, sahani, kijiko, sufuria, mwiko
9. Nyeupe, kijani, manjano **katani,** bluu
10. Tembo, chui, **kuku,** pundamilia

**Andika neno moja lenye maana sawa na tungo zifuatazo**

Mfano: Leta akilini fikira ya jambo lililotokea au lililopata kumbuka

1. Kitu anachopewa mtu baada ya kuhitimu elimu au mafunzo fulani cheti
2. Ondoa ngozi ya mnyama aliyekufa – chuna
3. Mahali wanapotibiwa watu – hospitali
4. Mahali ambapo sheria za nchi hutungwa - bungeni
5. Mahali ambapo watu huenda kuuza na kununua bidhaa – sokoni
6. Nenda kutoka mahali fulani hadi pengine kwa miguu au kwa basi, ndege, baiskeli safiri
7. Mtu anayetengeneza kabati, viti, meza - seremala

**Kusoma habari na kubainisha maneno mapya na kueleza maana zake kwa kutumia kamusi.**

Maneno mapya, ni maneno ambayo mzungumzaji yeyote wa lugha anakutana nayo kwa mara ya kwanza katıka lugha yake. Maneno hayo yanakua mapya kwake na ili apate maana ni lazima atumie kamusi.

Kamusi ni kitabu ambacho kinaorodhesha maneno ya lugha yaliyokusanywa kutoka kwa mzungumzaji wa lugha Fulani kwa mfano Kiswahili, maneno hupangwa kwa mtindo wa alfabeti. hutoa maana, asili na ufafanuzi wa matumizi ya maneno na jinsi yanavyotumika au yanavyotamkwa.

**Aina za Kamusi**

i. Kamusi wahidiya

- ❖ Hii ni kamusi ya lugha moja ambako maneno yanapangwa na kuelezwa kwa lugha ile ile mfano Kiswahili- Kiswahili.

ii. Kamusi thania

- ❖ Hii ni kamusi ya lugha mbili ambako maneno ya lugha moja yanaorodheshwa halafu maana huoneshwa kwa lugha tofauti. Mfano ni Kiswahili - Kiingereza au Kiingereza - Kiswahili.

**Muundo wa Kamusi**

**Kimuundo kamusi imegawanyika katika senemu kuu tatu**

1. UTANGULIZI WA KAMUSI
    - Hii ni sehemu ya kwanza ya kamusi, sehemu hii hujumuisha muhtasari wa sarufi ya lugha yenyewe pamoja na maelezo ya namna ya kutumia kamusi.

2. MATINI YA KAMUSI
    - Hii ni sehemu yenye vidahizo vyote vya kamusi husika kuanzia alfabeti a-z, vidahizo vyote huorodheshwa hapa na kufafanuliwa.

3. SHEREHE YA KAMUSI
    - Ni taarifa zinazoingia mwishoni mwa kamusi

**Faida za Kamusi**

- Husaidia kujua misamiati mipya
- Husaidia kujua ni aina za maneno kwa mfano nomino, kitenzi
- Husaidia hata kwa wale watu ambao hawajui lugha
- Kamusi huelezea zaidi kuhusu maneno mfano tembo - kisawe chake ni ndovu
- Kamusi hutusaidia kujua lugha ya kigeni mfano kifaransa
- Kamusi hutusaidia kusoma hata kwa wale wasiojua kusoma kwa sababu huwa na michoro au picha
- Kamusi huonesha matamshi sahihi ya maneno
- Kamusi huonesha asili ya neno mfano kutoka kiarabu, kiingereza, kireno au lahaja Fulani
- Kamusi hutusaidia kujua alama na vifupisho mbalimbali vinavyotumiwa katika lugha husika
- Kamusi huongeza maarifa zaidi kuhusu lugha ya mzungumzaji

**JINSI YA KUTUMIA KAMUSI**

Maneno ya kwenye kamusi hupangwa kwa utaratibu wa alfabeti A hadi Z

Kwa hiyo tunapotafuta neno katika kamusi tunaangalia limeanza na herufi gani. Maneno mengi yako katika umoja na wingi

**Mfano**

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kiti | Viti |

Mti Miti

**Chakula Vyakula**

Ili upate neno katika kamusi inabidi kuangalia herufi inayoanzia neno hilo katika umoja. Maneno megine yana viambishi awali mfano amekula viambishi awali ni a na me. Ili upate neno lenye viambishi awali katika kamusi angalia shina la neno linaanzia na herufi gani

**Mfano**

| Neno lenye viambishi awali | Shina | Herufi |
|---|---|---|
| Wanacheza | Cheza | -ch- |
| Amekula | Kula | -k- |
| Vizuri | Zuri | **-z-** |

Kwa maneno mengine kama vile vielezi, vihisishi, viunganishi angalia vinaanzia na herufi gani. Mfano katıka maneno haya koleo, kiazi, kichomi, kitendawili, kichaa, katika, kuku, kelele. Katika kamusi angalia herufi 'K' baada ya hapo angalia herufi inayofuata 'k' kama ni a, e,i,o,u kama mfuatano hufuata alfabeti kwa jinsi hiyo maneno hayo hapo juu yatakua na mfuatano ufuatao katika, kelele, kiazi, kichaa, kichomi, kitendawili, koleo, kuku. Maneno yalıyopangwa katıka kamusi kuanzia herufi "A" hadi "Z" huitwa vidahizo hivyo, kidahizo ni neno lolote linaloingizwa katika kamusi kwa kuandikwa kwa wino mzito na kutolewa ufafanuzi wake.

**Mfano**

Mama (n) - Mzazi wa jinsia ya kike

Kidahizo pamoja na fasili yake katika kamusi huitwa kitomeo. Hivyo kitomeo ni kidahizo pamoja na ufafanuzi wake.

Mfano

Kitomeo = Dada (n) ndugu wa uzao mmoja wa jinsia ya kike

Kamusi ni muhimu sana kwa mwanalugha yeyote yule. Bila kuwa na kamusi huwezi kujifunza lugha kikamilifu.

Kamusi pia husaidia sana kufahamisha mnyambuliko wa vitenzi katika kauli mbalimbali kama vile kutenda, kutendwa, kutendewa, kutendeka, kutendesha au kutendana. Minyambuliko hii huoneshwa katika kamusi kwa kutumia.

-ea- wa - ewa eka- esha- na -nk.

**Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali**

Mwalimu Mushi anafundisha katika shule ya msingi Oshara. Mwalimu mushi anafundisha somo la Kiswahili darasa la sita.

Siku moja mwalimu Mushi na wanafunzi wa darasa la sita walijadiliana kwa pamoja kuhusu kutembelea maktaba kuu ya mkoa. Walikubaliana kwa pamoja kwamba watakwenda sıku ya Alhamisi.

Mwalimu Mushi aliwasisitiza kuwa wasafi na kuonesha nidhamu ya hali ya juu, pindi watakapofika huko maktaba. Aliwatahadharisha kutokuiba vitabu kwani humo ndani kuna kamera za ulinzi.

Siku ilipowadia wanafunzi waliwahi mapema. Walipanda basi la shule kuanza safari ya kuelekea maktaba ya mkoa. Walipofika waliingia sehemu ya mapokezi walimkuta dada mmoja aliwakaribisha kwa furaha. Kisha aliwapa utaratibu na sheria za maktaba. Aliwambia mtu awapo maktaba haruhusiwi kula chakula, kulala, wala kupiga kelele Na ukichukua kitabu kwa ajilı ya kusoma ni lazima ukirudishe palepale ulipokichukua. Kisha aliwaruhusu kuingia ndani kwa ajili ya kujisomea.

Wanafunzi pamoja na mwalimu Mushi waliingia ndani ya maktaba na kila mtu alıchukua kitabu akipendacho na kuanza kujisomea kimya kimya.

Mwanafunzi mmoja aitwae Hadija aliona kitabu kikubwa kimeandikwa kamusi. Alivutiwa nacho akakichukua ili akisome. Alipofungua ndani alistaajabu kuona maneno mengi yakiwa yamepangwa kwa alfabeti pamoja na tafsiri zake.

Muda ulipokwisha mwalimu na wanafunzi walirudi shuleni. Walipofika shuleni mwalimu Mushi aliwauliza juu ya safari ya maktaba. Wanafunzi walimwambia mwalımu kuwa wanmefirahi sana kwani wamesoma vitabu vingi hivyo wamepata maarifa zaidı. Hadıja alımwambia mwalımu yeye amesoma kıtabu kimeandikwa kamusi Na ndani ya kitabu hıcho kulikuwa na maneno mengi tafsiri zake Na maneno hayo yamepangwa kwa alfabeti kuanzia A hadi Z.

Mwalimu aliwaambia maneno yaliyopangwa kwa mpangilio wa alfabeti yanaitwa vidahizo. Na kidahizo pamoja na fasili yake huitwa kitomeo. Wanafunzi wote walifurahı sana kupata Maarifa hayo.

**UFAHAMU**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Mwalimu Mushi anafundisha shule gani?
   - Mwalimu Mushi anafundisha shule ya msingi Oshara

2. Mwalimu Mushi anafundisha somo gani?
   - Mwalimu Mushi anafundisha somo la Kiswahili

3. Mwalimu Mushi alijadiliana na wanafunzi kwenda wapi?
   - Mwalimu Mushi alijadiliana na wanafunzi kwenda kutembelea maktaba ya Mkoa

4. Walikwenda siku gani?
   - Walikwenda siku ya Alhamisi

5. Wanafunzi walikwenda maktaba kwa usafiri gani?
   - Wanafunzi walıkwenda maktaba kwa kutumia basi la shule

6. Ni vitu gani haviruhusiwi maktaba
   - Vitu visivyoruhusiwa maktaba ni kulala, kula chakula na kupiga kelele.

7. Mwalimu aliwaambia maneno yaliyopangwa kwa mpangilio wa alfabeti yanaitwaje?
   - Maneno yaliyopangwa kwa mpangilio wa alfabeti yanaitwa vidahizo.

8. Nini maana ya kitomeo
   - Kitomeo ni kidahizo pamoja na fasili yake

**Msamiati**

**Tumia kamusi kuandika maana ya maneno haya kisha tunga sentensi moja kwa kila neno**

**1. Alfabeti**
- Ni herufi za lugha zilizopangwa kwa utaratibu maalum ambazo hutumiwa katika maandishi. Mfano a, b, ch, d, e, nk

**SENTENSI**
- Mwalimu alipanga majina ya wanafunzi darasanı kwa alfabeti

**2. Kamusi**
- Ni kitabu cha maneno yaliyopangwa kwa utaratibu wa alfabeti au mwingine na kutolewa maana na maelezo mengine.

**SENTENSI**
- Baba yangu alinunulia kamusi

**3. Kidahizo**

- Ni neno linaloingizwa katika kamusi kwa chapa iliyokoza mara nyingine rangi, neno kuu katika kamusi

**SENTENSI**

- Mwalimu wetu alitufundisha namna ya kutafuta kidahizo katika kamusi

**4. Kitomeo**

- Kidahizo pamoja na maelezo yake yote

**SENTENSI**

- Mwalimu wetu alituambia maana ya kitomeo

**5. Maktaba**

- Nyumba au chumba mnamohifadhiwa machapisho ambamo watu huruhusiwa kuyatumia au kuyaazima kwa muda
- Mkusanyiko wa machapisho kama yitabu, kanda n.k. yaliyohifadhiwa na ambayo huweza kuazimwa na kutumwa.

**SENTENSI**

- Tulipokwenda tulisoma vitabu vingi vya hadithi

**6. Mwalimu**

- Mtu anayesomesha wengine elimu na maarifa fulani

**SENTENSI**

- Dada yangu ni mwalimu wa sekondari

**7. Maarifa**

- Njia inayotumiwa kujitoa katika shida ama kuweza kupata kitu
- Elimu, ujuzı

**SENTENSI**

- Baba alituambia tusome kwa bidii ili tuweze kupata maarifa.

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Oanisha sehemu A na B ili kupata methali sahihi**

| | SEHEMU A | | SEHEMU B |
|---|---|---|---|
| 1 | Simba mwenda pole | A | Hutunzwa |
| 2 | Mchelea mwana kulia | B | Havitangamani |
| 3 | Kipenda roho | C | Harabu ya nzima |
| 4 | Mpenda chongo | D | Si maungwana |
| 5 | Aibu ya maiti | E | Hula ovyo |
| 6 | Kiburi | F | Huona kengeza |
| 7 | Nazi mbovu | G | Hula nyama mbichi |
| 8 | Lila na fila | H | Hulia mwenyewe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Mcheza kwao | I | Ndiye mla nyama |
| 10 | Mpanda ovyo | J | Aijuaye mwosha |
| | | K | Aijuaye kata |

**MAJIBU**

1. **I**
2. **H**
3. **G**
4. **F**
5. **J**
6. **D**
7. **C**
8. **B**
9. **A**
10. **E**

**Kamilisha sentensi kwa miundo ifuatayo**
**Kuwa, japokua, afadhali, tangu, sharti**

1. Imetangazwa kesho ni sikukuu
   - ❖ Imetangazwa kuwa kesho ni sikukuu

2. Kupanda mlima mkali wakati wa mvua ni_____________kuliko kuteremka
   - ❖ Kupanda mlima mkali wakati wa mvua ni afadhali kuliko kuteremka

3. Mkitaka kula_________________mnawe mikono
   - ❖ Mkitaka kula sharti mnawe mikono

4. Alijitahidi kubeba mzigo ule_________________ulikua unamwelemea
   - ❖ Alijitahidi kubeba mzigo ule japokua ulikuwa unamwelemea

5 Nimeacha kula nyama_________________nilipokua mdogo
   - ❖ Nimeacha kula nyama tangu nilipokua mdogo

**Badili sentensi hizi katika hali ya kutendeka**

1. Mboga imechumwa kwa urahisi
   - ❖ Mboga imechumika kwa urahisi

2. Ukili umesukwa vizuri

- ❖ Ukili umesukika vizuri

3. Panya amekamatwa bila kutarajia
   - ❖ Panya amekamatika bila kutarajia

4. Wahalifu wameadhibiwa barabara
   - ❖ Wahalifu wameadhibika barabara

5 Gari linaendeshwa bila wasiwasi
   - ❖ Gari linaendesheka bila wasiwasi

**Panga maneno yafuatayo kialfabeti**
Kidani, kidato, kidevu, kideri, kidahizo
Mpangilio
Kidahizo, kidani, kidato, kideri, kidevu

**Andika visawe vya maneno yafuatayo**

1. Mtindo – staili
2. Nia – lengo
3. Ongea - sema/zungumza
4. Nakshi – urembo
5. Mtu-bimadamu
6. Shika - kamata
7. Rafiki – swahiba
8. Sala - dua
9. Rushwa - hongo
10. Waza - fikıri
11. Vifijo - vigelegele
12. Ukaidi - ujeuri
13. Vyema - vizuri
14. Wiki- juma
15. Mbwa- kelbu
16. Baba - abu
17. Bibi - nyanya
18. Daktari - tabibu
19. Treni - gari moshi
20. Mwana - mtoto
21. Keti - kaa
22. Nderemo – vifijo
23. Wivu- husda

MWL

24. Ugonjwa - maradhi
25. Tafrija - sherehe
26. Ukwasi - utajiri

**Kutumia maandishi katika kuwasiliana kulingana na miktadha mbalimbali**

**a. Kuandika matangazo mbalimbali kuzingatia taratibu za uandishi**

Matangazo ni habari inayotolewa hadharanı ilı ipate kuwafikia wanaohusika na habari hiyo. Matangazo kuhusu jambo muhimu kama vile Mkutano, nafası za kujunga kidato cha kwanza semina, nafası za kazi, biashara n.k.

**Aina za Matangazo**

1. Matangazo ya biashara - hudhamiria kuVuta wateja
2. Matangazo ya dini - shughuli za kidini
3. Matangazo ya shughuli za kiserikali
4. Matangazo ya tahadhari – Maonyo, ilani
5. Matangazo ya vifo
6. Matangazo ya nafasi za kazi

**Misingi ya uandishi wa matangazo**

a) Mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa matangazo
b) Kutaja kıchwa cha habarı – kiandike kwa herufi kubwa
c) Kutaja aina ya biashara (matangazo ya biashara)
d) Kutaja mahali inapopatikana hiyo bidhaa au huduma
e) Kutaja njia za mawasiliano.

**Sifa za matangazo**

a) Yawe na muundo sahihi
b) Yatumie lugha fasaha na pia inayoeleweka
c) Yatumie lugha yenye kuhusiana na ujumbe wa tangazo
d) Yawe na ukubwa wa kiasi tuu
e) Yatumie picha au mchoro

**Faida za matangazo katika jamii**

a) Kutangaza ni njia ya kuwasiliana na kupeana taarifa mapema kabla ya tukio linalokusudiwa
b) Kuelimisha jamii – matangazo hutumika kama vitanabaishi vyenye kutoa tahadhari, ujuzi, maarifa na stadi mbalimbali. Mfano chanjo ya pepopunda, wizi wa maji n.k.
c) Kutangaza husaidia kuboresha shughuli za kiuchumi kama vile kufahamisha jamii juu ya bidhaa mpya zilizotoka, mahali wanapoweza kupata bidhaa hizo

**Njia za kutolea matangazo**

**1. Matangazo ya redioni**

- Haya ni matangazo yanayotolewa kwa kusomwa na mtu redioni. Matangazo haya hutakiwa kutolewa kwa kutumia sauti inayosikika vizuri na maelezo yanayowezesha kueleweka kwa taarifa kamili inayotolewa.

**11. Matangazo kwenye televisheni (luninga)**

- Matangazo ya aina hii mbali na kutumia maelezo ili yaweze kueleweka kuhalisika na kuvutia yanatakiwa kuambatana na picha pamoja na wimbo au mlio Fulani unaovutia

**111. Matangazo ya magazetini**

- Matangazo haya hutakiwa kuandikwa kwa ubunifu ili yapate kueleweka na kuvutia. Mambo ambayo mwandishi anatakiwa kuyazingatia katika uandishi wa matangazo haya ni
  a. Kutumia fugha inayoeleweka
  b. Kutumia hati inayosomeka vizuri
  c. Kutoa maelezo yanayojitosheleza ili tangazo lake lipate kueleweka
  d. Kutumia picha au michoro inapoweżekana. Mfano picha za sabuni, mabatink.

**IV. Matangazo ya kwenye mabango**

Haya ni matangazo yanayoandikwa kwenye vitambaa vikubwa au mbao na kuwekwa mahali pa wazi. Mfano kando ya barabara au kwenye majengo. Matangazo hutakiwa kuwa na maandishi makubwa ili kumwezesha kila mtu kuyasoma bila tatizo. Vilevile matangazo haya huwekwa picha au michoro ili liweze kueleweka na kuvutia wasomaji wake.

TANGAZO LA BIASHARA
GARI LINAUZWA, WAHI
SASA
Gari aina ya TOYOTA PASSO
Lililotengenezwa mwaka 2001 rangi nyeusi
Liko katika hali nzuri, bei ni maelewano.
Wasiliana nasi kupitia
Simu 0783 -000040
Nukshi +22278286109
Barua pepe: pimbi@yahoo.gmail

Tovuti: www.Pimbi.go.tz

**Msamiati**

Eleza maana ya msamiati ufuatao kisha tunga sentensi kwa kila msamiati

**i) Tovuti**

- Nafasi katika mtandao wa kompyuta zinazopatikana taarifa mbalimbali. Mfano kazi, Wafanyakazi, biashara n k.

**Sentensi**

- Dada yangu aliona tangazo la kazi kwenye tovuti

**ii) Tangazo**

- Jambo lililotangazwa, ilani, notisi, taarifa la serikali au biashara

**Sentensi**

- Mimi nilisikia tangazo la wizara ya Afya kwamba watoto wenye umri chini ya Miaka mitano wakapate chanjo ya pepopunda.

**iii) Biashara**

- Ununuzi na uuzaji (uchuzi) ya jumla au

rejareja Sentensi

- Baba yangu anafanya biashara ya kuuza mbao

**iv) Barua pepe**

- Ujumbe unaotumwa kwa njia ya elektroniki kupitia kompyuta au simu iliyounganishwa kwenye mfumo wa mtandao wa intaneti

**Sentensi**

- Dada yangu alipokea ujumbe.toka kwa shangezi la

**v) Nukushi**

- Mashine ya kutuma nakala za matini kwa njia ya simu. (faksi)

**Sentensi**

- Baba yangu alikwenda mjini kununua nukushi ndogo kwa ajili ya kufanyia biashara zake.

**vi) Gazeti**

- Karatasi zilizochapwa kwa ajili ya kutoa habari

**Sentensi**

- Baba yangu aliona tangazo la nafasi za shule kwenye gazeti la majira

**METHALI**

**Toa maana ya methali zifuatazo**

i) Abadi abadi kumba hukata jiwe

- Juhudi ama bidii katika jambo hata uwe na uwezo mdogo namna gani hatimae litazaa matunda.

ii) Maji ukiyavulia nguo huna budi kuyaoga

- Ukiamua kufanya jambo yakupasa ulifanye kama linavyopaswa ikiwa ni pamoja na kukabiliana na changamoto atakazopata hadi limekamilika.

iii) Mbiu ya mgambo ikilia ina jambo

- Ukipata tahadhari ya jambo lolote huna budi kuchukua hatua za kujilinda usije kupata matatizo.

iv) Mchumia juani hulia kivulini

- Anayekubali kujishughulisha mwishowe atapata riziki au ahueni.

v) La kuvunda halina ubani

- Jambo ambalo tayari limekwisha haribika ama kwenda vibaya halina namna ya kuliokoa

vi) Samaki mmoja akioza huoza wote

- Kosa atendalo mtu huweza kuathiri ama kuchafua sifa hata za ambao awakuhusika nalo

vii) Siku za mwizi ni arobaini

- Huwezi kushamiri katika uovu milele, ipo siku utafahamika na kuumbuka

viii) Tahadhari kabla ya

- Jikinge na janga kabla halijatokea kwani likishatokea hutaweza kulitatua tena hatari

1x) Fuata nyuki ule asali

- Ukitaka mambo mazuri basi huna budi kukubali gharama za kulipata

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Tumia herufi za maneno yafuatayo kuunda maneno mengine mapya**

**Mfano Bakia – akiba**

i. Ua - au
ii. Oza - zao
iii. 111. Mila - lami
iv. Taka - kata
v. V. Wale - lewa
vi. Zaka - kaza
vii. Paka – kapa
viii. viii. Mali – lima
ix. Wape – pewa
x. Leo - ole

**Andika hali za vitenzi katika sentensi zifuatazo**

1. Bibi amepika chakula
   - ❖ Hali timilifu

2. Asha anasoma hadithi
   - ❖ Hali ya kuendelea

3. Watalii hupiga picha wanyama
   - ❖ Hali isiyodhihirika

4. Kaka ameungua moto
   - ❖ Hali timilifu

5 Mwalimu anawachapa wanafunzi
   - ❖ Hali ya kuendelea

6. Wachezaji wamecheza vizuri
   - ❖ Hali timilifu

7. Juma ahukumiwa kunyongwa
   - ❖ Hali isiyodhihirika

Andika kinyume cha maneno yafuatayo

i. 1.Rejea – Nenda
ii. Zama - Ibuka
iii. Cheka - Lia
iv. Nuna - Tabasamu
v. Baridi – Joto
vi. Mwenyeji –Mgeni
vii. Mchapakazi – Mvivu
viii. Mkali – Mpole
ix. Nyeupe - Nyeusi
x. Huku -Kule

| **UMOJA** | **WINGI** |
|---|---|
| Kikundi | Vikundi |
| Kingozi | Viongozi |
| Cheo | Vyeo |
| Kande | Makande |
| Mlo | Milo |
| Wanunuzi | Mnunuzi |
| Figa | mafiga |
| Mboga | Mboga |
| Sukari | Sukari |
| Mwaka | Miaka |
| Mtoto | Watoto |
| Kijana | Vijana |

**Badili sentensi zifuatazo katıka umoja**

1. Wazazi watanunua magari
   - ❖ Mzazi atanunua gari

2. Barabara mbili zimejengwa
   - ❖ Barabara moja imejengwa

3. Mito imejaa maji
   - ❖ Mto umejaa maji

4. Watoto wametengeneza matoroli ya mti
   - ❖ Mtoto ametengeneza toroli la mti

5. Wadudu wamevamia mashamba ya wakulima

- ❖ Mdudu amevamia shamba la mkulima

6. Miti imekatwa na wanakijiji
   - ❖ Mti umekatwa na mwanakijiji

7. Mipira imechanwa na watoto
   - ❖ Mpira umechanwa na mtoto

8. Vyakula vimepikwa na mama
   - ❖ Chakula kimepikwa na mama

9. Magari yanaendeshwa na watoto
   - ❖ Gari linaendeshwa na mtoto

10. Baiskeli zimenunuliwa na baba
    - ❖ Baiskeli imenunuliwa na baba

**Badili sentensi zifuatazo kuwa katika hali ya kutendwa**

1. Mbwana anakata mti
   - ❖ Mti unakatwa na mbwana

2. Watoto wanacheza mpira
   - ❖ Mpira unachezwa na watoto

3. Bibi anagonga mlango
   - ❖ Mlango unagongwa na bibi

4. Baba anasoma hadithi
   - ❖ Hadithi inasomwa na baba

5. Maneno na mazoea wametengeneza samani nzuri
   - ❖ Samanı nzuri zimetengenezwa na maneno na mazoea

6. Wazee wanunusa ugoro
   - ❖ Ugoro unanuswa na wazee

7. Mwalimu amekosea njia
   - ❖ Njia imekosewa na mwalimu

8. Mtoto amechota maji
    - ❖ Maji yamechotwa na mtoto

9. Jiwe limetoboa kiatu
    - ❖ Kiatu kimetobolewa na jiwe

10. Wachezaji wanafanya mazoezi
    - ❖ Mazoezi yamefanywa na wachezaji.

**Andika majina ya watu wafanyao kazi zifuatazo**

- **a)** Atengenezaye samani **- SEREMALA**
- **b)** Anayefua vyuma – **MHUNZI**
- **c)** Ajengaye kwa matofali na mawe – **FUNDI MWASHI**
- **d)** Anayetibu wagonjwa hospitalini – **DAKTARI**
- **e)** Anayeendesha meli – **NAHODHA**
- **f)** Anayeshona nguo – **FUNDI CHEREHANI**
- **g)** Anayetengeneza hereni, bangili, Mkufu n.k **SONARA**
- **h)** Anayefua nguo **- DOBI**
- **i)** Anayeendesha ndege - **RUBANI**
- **j)** Anayeendesha gari – **DEREVA**
- **k)** Anayevuna samaki - **MVUVI**

**b. Kuandika kirefu cha vifupisho vya maneno au Majina ya msingi (JKT UDA TBC TET BMT)**

Baadhi ya majina na maneno katika lugha nyingi za dunia hutokana na ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua herufi za mwanzo za maneno hayo ufupisho wa aina hii unahusu jina lenye maneno mengi. Jina hilo linakuja kuelezwa kwa silabi za mwanzo za maneno husika. Silabi hizo huunganishwa ili kuunda umbo mithili ya neno. Ufupisho huu huitwa akronimia

**Mfano**

- **a.** Baraza la Kiswahili la Taifa - **BAKITA**
- **b.** Baraza kuu la waislamu Tanzania – **BAKWATA**
- **c.** Ukosefu wa kinga mwilini - **UKIMWI**

**Faida za vifupisho**

Vifupisho husaidia kufupisha maelezo marefu kupita kiasi na kuwa mafupi na kuwa rahisi kuyatamka kwa mara moja.

**Hasara za vifupisho**

Wakati mwingine si vipashio vya mwanzo ambavyo huweza kutumiwa katika kuunda maneno hali ambayo huzua utata katıka kujua ni mbinu ipi ambayo ni sahihi

**Mfano**
**TARAKILISHI - Tarakimu + akili + mashine**
**Andika ufupisho wa maneno yafuatayo**

1) Baraza la sanaa la Taifa - **BASATA**
2) Teknolojia ya habari na mawasiliano - **TEHAMA**
3) Baraza la Kiswahili la Taifa - **BAKITA**
4) Kiwanda cha uchapishaji cha Taifa – **KIUTA**
5) Tawala za mikoa na serikali za mitaa– **TAMISEMI**
6) Chama cha Netiboli Tanzania – **CHANETA**
7) Taasisi ya kupambana na kuzuia rushwa – **TAKUKURU**
8) Upungufu wa kinga mwilini – **UKIMWI**
9) Mpango wa Elimu ya msingi kwa waliokosa - **MEMKWA**
10) Umoja wa michezo na Taaluma kwa shule za msingi Tanzania – **UMITASHUMTA**
11) Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili -**TUKI**
12) Taasisi ya Taaluma za Kiswahili – **TATAKI**
13) Mpango wa kurasımısha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania - **MKURABITA**
14) Mkakati wa kukuza uchumi na kupunguza umaskini Tanzania - **MKUKUTA**
15) Chama cha Kiswahili cha Taifa – **CHAKITA**
16) Baraza kuu la waislam Tanzania – **BAKWATA**
17) Umoja wa michezo ya shule za sekondari – **UMISSETA**

**Andika virefu vya vifupisho vifuatavyo**

1. JK.T.-Jeshi la kujenga Taifa
2. TET Taasisi ya Elimu Tanzania
3. UDA Shirika la usafiri Dar es salaam
4. TBC- Tanzania Broadcasting corporation (shirika la habari la Taifa)
5. BMT-Baraza la michezo Tanzania
6. J.W.T.Z- Jeshi-la wananehi Tanzanin
7. C.CM-Chama cha mapinduzi

MWL

**MAZOEZI YA LUGHA**
**Kanusha sentensi zifuatazo**

1. Baba anapaua nyumba
    - Baba hapaui nyumba

2. Mbwa hutaga mayai
- Mbwa hatagi mayai

3. Jiwe litaangukia nyumba
- Jiwe halitaangukia nyumba

4. Maziwa yamemwagika
- Maziwa hayajamwagika

5. Njiwa ameruka juu
- Njiwa hajaruka juu

6. Wazee wanacheza mziki
- Wazee hawachezi mziki

7. Kuku amepaa angani
- Kuku hajapaa angani

8. Mwanafunzi anaandikia mkaa
- Mwanafunzi haandikii mkaa

9. Mtoto analia
- Mtoto halii

10. Mwizi amepigwa risası
- Mwizi hajapigwa risasi.

**Pigia mstari neno lililotofauti na mengine**

1. Jicho, pua, sikio, **nywele,** mdomo
2. Halima Rahma, **Rahim,** Rehema, Asha
3. **Bia,** togwa, sharubati, soda, juisi
4. Tembe, msonge, ghorofa, manyata, **mkaa**
5. Biriani, walı, pilau, **sharubati,** ugali
6. Daftari, **mkeka,** kitini, jarida
7. Mlimau, mwembe, mpapai, **mkorosho**, mchungwa
8. Shangazi, babu**, mkoloni,** mjomba
9. Shule, **pango**, kanisa, msikiti
10. **Ninakula,** ninakimbia, ninaruka, ninacheza
11. Kufunika**, kuanika,** kuficha, kuhifadhi
12. **Mti,** kalamu, kitabu, wino
13. Majani, matawi, **mafuta**, miti
14. Nyuki, mbu, nyigu, **ng ombe**
15. Matofali **nazı**, sakafu, makuti

MWL

**Badili kauli taarifa kuwa kauli halisi**

1. Mwalimu alisema kvwamba Tanzania ni nchi nzuri
- Tanzania ni nchi nzuri

2. Kaka alitumbia tusile pilipili

- Msile pilipili

3. Mwalimu alisema kwamba atatufundisha masomo ya ziada
   - Nitawafundisha masomo ya ziada

4. Tumchotee maji
   - Mchoteeni maji

5. Aliuliza kama tumenawa mikono
   - Mmenawa mikono?

6. Alituagiza tumpelekee kibiriti na kuni
   - Nipelekeeni kibiriti na kuni

7. Aliuliza kama tumemuelewa
   - Mmenielewa?

8. Mama alituonya tusipite njia ile
   - Msipite njia ile

9. Mjumbe aliwaasa wananchi kutochoma takataka
   - Msichome takataka

10. Bibi alitukataza kucheza kwenye mvua
    - Msicheze kwenye mvua

**MIUNDO**

**Tunga sentensi kwa kutumia miundo**

1. Kwamba
   Alituambia kwamba hatakuja kwenye mkutano
2. kidogo tu
   Nikila kidogo tu tumbo linajaa

3. Baada ya………………………………………………………
   kusoma kwa bidi alifaulu mtihani wake

**c. Kufupisha habari katika maandishi bila kupotosha maana iliyokusudiwa na kwa kuzingatia alama za uandishi ufupisho maana.**

Ufupisho wa habari ni kuielezea habari upya kwa maneno machache zaidi bila kupoteza maana ya msingi Kwa kawaida idadi ya maneno inatakiwa kuwa thelathini ya habarı ya awali

**Hatua za kufuata katika ufupisho**

1) i Soma habari yote mpaka uielewe
2) Chagua taarifa na maneno maalumu
3) Linganisha taarifa muhimu na habari ya asili
4) Andika muhtasari kama inavyotakiwa
5) Linganisha usawa wa ufupisho na habari ya asili

**Umuhimu wa ufupisho**

i. Ufupisho humzoesha mtu kufikiri waziwazi, kwani mazoezi humtaka mtu asome kwa uangalifu ili aone habari muhimu
ii. Ufupisho humpa mtu mazoezi ya kupanga mawazo yake kwa uangalifu na katika sentensi zilizonyooka
iii. Husaidia katika uhariri wa habari
iv. Hutumika wakati wa kutayarisha ripoti na kumbukumbu za mikutano

**Mfano**

a. Mama alinunua mahindi, mtama, ngano, uwele
- ❖ Mama alinunua nafaka

b. Kaka amenunua meza, viti, kabati
- ❖ Kaka amenunua saman

**Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno yasiyozidi hamsini (50)**

**HISTORIA YA BARA LA AFRIKA**

Kamati imeundwa ikihusisha kikundi maalumu cha wataalamu, ambao watavalia njuga na kuandika upya historia ya bara la Afrika. Mpango huu ni mahsusi na tunaunga mkono wananchi wote. Ni mpango ambao utatokomeza maandishi yaliyoandikwa na wakoloni Walipotosha ukweli wa maisha, mila na utamaduni wetu.

Vitabu vingi vya historia ya bara letu vinavyotumiwa na vijana shuleni, viliandikwa na watu waliokuja kutawala na kujitafutia mali. Katika maandishi yaliyoandikwa na wakoloni walipotosha ukweli wa maisha, mila na utamaduni. Wao walitufanya tuamini kwamba lugha zao, mila na maisha yao vilikua ni vitu vya thamani kuliko vyetu.
Mpaka leo hu ni watu wachache wanaoamini kuwa tuna ustaarabu na utamaduni ulio imara tangu zama za wahenga Tunaamini kuwa miaka michache ijayo upeo utageuka kabisa katıka nadharia zilzo vichwani mwa watu wengi, waliolishwa kasumba ya ukoloni.

MWL.

**UFUPISHO**

Habarı hu unazungumzia kamati iliyoundwa kuandika upya historia ya bara la Afrika. Mpango huo unaungwa mkono na wananchi wote kwani utaondoa upotoshaji wa

wakoloni kuhusu maisha halisi, mila na desturi za waafrika Vitabu vingi vinavyotumika sasa shuleni vinapotosha ukweli halisi, kwani vinatukuza utamaduni wa wakoloni na kuudharau utamaduni wetu.

**UFAHAMU**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Mwandishi anazungumzia historia bara gani?
    - ❖ Mwandishi anazungumzia historia ya bara la Afrika

2. Kamati imeundwa ili kufanya nini?
    - ❖ Kamati imeundwa ili kuandika upya historia ya bara la Afrika

3. Wameunda kamati ili kutokomeza nini?
    - ❖ Wameunda kamati ili kutokomeza maandishi yaliyoandikwa na wakoloni, walipotosha ukweli wa maisha, Mila na utamaduni wetu.

4. Vitabu vingi vya historia ya bara letu la Afrika vimeandikwa na akina nani?
    - ❖ Vitabu vingi vya Historia bara letu la Afrika vimeandikwa na wakoloni.

5. Katika maandıshi yaliyoandikwa na wakoloni walipotosha nini?
    - ❖ Katika maandishi yaliyoandikwa na wakoloni walipotosha ukweli wa maisha, Mila na utamaduni.

**MSAMIATI**

**Andika maana ya msamiati na tunga sentensi kwa kila msamiati**

**i) Utamaduni**

- ❖ Mila, asili, jadi, na desturi za kundi la jamii fulani

**Sentensi**

- ❖ Mwalimu alituambia utamaduni wa wamasai ni kutoboa masikio na kuvaa rubega.

**ii) Thamani**

- ❖ Gharama au ubora wa kitu kutokana na hali na kuhitajika kwake na jamii.

**Sentensi**

- ❖ Baba alituambia tusome kwa bidii kwani elimu kwa sasa ni kitu cha thamani.

**iii) Tokomeza**

- ❖ Fanya kitu kisionekane tena

**Sentensi**

- ❖ Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwaambia wananchi watokomeze ujinga kwani ni adui wa Taifa.

**iv) Ustaarabu**

- ❖ Hali ya mtu kuwa na vitendo, tabia na mwenendo unaolingana na maadili ya jamii inayohusika.

**Sentensi**

- ❖ Mwalimu wa somo la historia alituambia kabla ya kuja kwa wakoloni watanzania walikua na ustaarabu wao.

**v) Kasumba**

- ❖ Mabadilisho ya fikra za mtu yanayosababishwa na elimu au utamaduni wa jamii, yanayomfanya afuate mwenendo usio mwafaka na utamaduni wake au utu wake wa asili.
- ❖ Mabaki ya fikra za kikoloni katika kichwa cha mtu ya kikoloni propaganda anayotiwa mtu kichwani akiamini na kutenda mambo yanayooana na tabia za wakoloni.

**Sentensi**

- ❖ Baba alituambia tuache kasumba za kufuata utamaduni wa kigeni bali tudumishe utamaduni wetu.

**MIUNDO**

**Tunga sentensı kwa kutumia Miundo**

1. moja kwa moja-
- ❖ Waliingia moja kwa moja ndani

2. ………………………kwamba………………………………
- ❖ Walifikiri kwamba baadhi ya vyakula hulıwa na wageni tu

3. kinagaubaga
- ❖ Mambo mengi juu ya ugonjwa wa malaria yalielezwa kinagaubaga.

4. …………………..nyuma ya…………………………………..
- ❖ Paka hupenda kukaa nyuma ya mlango

5. ………………………….miongoni mwa……………………………..
- ❖ Juma ni miongoni mwa wanafunzi bora

6. ……………………………kati ya………………………………
- ❖ Asha ameshika nafasi ya kwanza kati ya wanafunzi hamsını

**METHALI**

**Panga vizuri maneno ya methali yaliyochanganywa ili kupata methali sahihi**

1. Huishia mbio za ukingoni sakafuni
- ❖ Mbio za sakafuni huishia ukingoni

2. Kwa mbachao usiache msala upitao
- ❖ Usiache mbachao kwa msala upitao

3. Kazi ya makosa haina Mungu
- ❖ Kazi ya Mungu haina makosa

4. Cha hufa ndugu mtumaini maskini
- ❖ Mtumainia cha ndugu hufa maskini

5. Hakivunji kidole chawa kimoja
- ❖ Kidole kimoja hakivunji chawa

6. Baada ya mkasa kisa
- ❖ Baada kisa mkasa

7. Ndiye mla simba mwenda nyama pole
- ❖ Simba mwendapole ndiye mla nyama

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Tumia maneno yafuatayo kujaza nafasi wazi**

**Ndiye, ndiyo, ndio, yupo, yumo, yuko, na kwa, ngeli ngali, nge.**

1. Tulisafiri treni kutoka mwanza hadi Tabora
   Tulisafiri kwa treni kutoka Mwanza hadi Tabora

2. Wewe utakayekwenda kumsalimia babu
   Wewe ndiye utakayekwenda kumsalimia babu

3. Mtoto… nje ya Nyumba
   Mtoto yupo nje ya nyumba

4. Angekula chakula as… sikia njaa
   Angekula chakula asingesikia njaa

5. Angelikua na pesa angelinunua gari
   Angelikua na pesa angelununua
   gari

6. Panya katika shimo
   Panya yumo katika shimo

7. Asha anapenda kula wali nyama
   Asha anapenda kula wali na nyama

8. Ningalikuwa mkubwa nis
   Ningalikuwa mkubwa ningalinunua gari

9. Wananchi wengi walimpigia kura za
   Wananchi wengi walimpigia kura za ndiyo

10. Hawa waliopigania uhuru wa Taifa hili
    Hawa ndio walipigania uhuru wa taifa hili

**Ondoa silabi moja katika maneno yafuatayo ili kuunda neno moja**
**Mfano msitu – mtu**

1. Baada - ada
2. Karanga - kanga
3. Wazazi – wazi
4. Barafu – bafu
5. Wakati - kati
6. Majeruhi - jeruhi
7. Karaha– raha
8. Fahanmu – hamu
9. Katika - kaka
10. Kubali - kuli
11. Asali- Sali

**Kanusha sentensi zifuatazo**

1. Jogoo wanataga mayai
   - ❖ Jogoo hatagi mayai

2. Rubani atatengeneza samanı
   - ❖ Rubani hatatengeneza samani

3. Mwanafunzı atatunga mtihani
   - ❖ Mwanafunzi hatatunga mtihani

4. Swea ni kifaranga mdadisi

- ❖ Swea si kifaranga mdadisi

5. Maisha ya bata yanavutia ndege wengine
   - ❖ Maisha ya bata hayavutii ndege wengine

6. Kobe ni kısıwa cha amanı
   - ❖ Kobe si kisıwa cha amanı

7. Mto utajaa maji
   - ❖ Mto hautajaa maji

8. Bibi atapika ugali wa mtama
   - ❖ Bibi hatapıka ugali wa mtama

9. Nahodha ataendesha gari
   - ❖ Nahodha hataendesha gari

10. Bibi anapika ugali wa mtama
    - ❖ Bibi hapiki ugali wa mtama

11. Shangazi ataninunulia gari
    - ❖ Shangazi hataninunulia gari

12. Vijana wana umoja
    - ❖ Vijana hawana umoja

13. Ngoma itapasuka
    - ❖ Ngoma haitapasuka

14. Amejenga kiwanda cha mbao
    - ❖ Hajajenga kiwanda cha mbao

15. Mbuzi wana jeshi imara
    - ❖ Mbuzi hawana jeshi imara

**d. Kuandika methali zenye mafunzo kulingana na kifungu cha habari Methali maana**

Methalı, Ni usemi mfupi wenye mpangilio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari firka au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jami husika. Ni kauli fupi yenye pande ambazo upande wa kwanza huanza na upande wa pili humalizia

**Mfano**

**Ashibaye hamjui mwenye njaa**

MAFUNZO

- ❖ Mara nyingi mtu huponzwa na neema alizonazo hata asitake kutambua shida walizonazo wengine.

**Aisifiaye mvua imemnyeshea**

MAFUNZO

- ❖ Mtu asifiaye jambo Fulani bila shaka ameshatambua utamu wake.

**UMUHIMU WA METHALI**

Methali huonya/hutahadharisha watu katika jamii dhidi ya maovu mfano usipoziba ufa utajenga ukuta.

a) Methali hutoa mafunzo mfano Elimu hama mwisho

b) Methali hutumiwa na waandishi, wazungumzaji na katika kazi mbalimbali za sanaa kama mapambo ya lugha

c) Hutumika kutoa mawaidha katika jamii Mfano: Asiefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

d) Hutumika kuunganisha jamii pamoja mfano.

- ❖ Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
- ❖ Kidole kimoja hakivunji chawa.

**MAISHA YA JUMA**

Siku moja na kikundi chake kilichojulikana kama "Mbwa mwitu" walivamia nyumbani kwa mzee Musa. Mzee Musa ni mfanyabiashara mkubwa wa mahindi katika mji wa pasua.

Mzee musa alıshtuka kutoka usingizini na kuchukua bastola yake na kunyata kuelekea sebuleni Mara aliwaona vijana watatu wakiwa wamebeba televisheni deki redio na kompyuta Mzee Musa alianza kuwakimbıza huku akıpıga kelele wezı!wezi!wezi. vijana wankimola huku wakiwa wamebeba mali walizoiba. MIZEE Musa aliwaamuru wasimame a Sivyo atawapiga nisasi. DIKIO Ta kuraiaisUsi Ukwa, vijana wale walikaidı onyo la mzee Musa Kweli siku za mwizi ni arobaini Mzee Musa alifyatua risasi iliyompata Juma kwenye mguu wenzake walifanikiwa kutoroka.

Mzee Musa alipiga simu kituo cha polisi ili kuwataarifu juu ya tukio hilo. Polisi walifika mara moja na kumkuta Juma akiwa chini ya ulinzi mkali wa mzee Musa pamoja na majirani wa mzee Musa.

Walimchukua hadi kituo cha polisi ili kuandikisha maelezo yake, kisha walimpeleka hospitali kutibiwa. Usiku uleule walianza msako mkali wa wale wezi wengine waliotoroka. Kufika asubuhi wezi wote walikua wamekamatwa na kuunganishwa na Juma

Taarifa za kujeruhiwa na kukamatwa kwa Juma ziliwafikia wazazi wake. Walizipokea kwa masikitiko makubwa Baba yake Juma alisema, ama kweli asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu Huku majirani nao wakisisitiza na kusema ama kweli mbio za sakafuni huishia ukingoni na hakuna marefu yasiiyo na ncha

Baada ya upelelezi kukamilika, Juma na wenzake walipelekwa mahakamani kusomewa mashtaka. Baada ya ushahidi kutolewa Juma na wenzake walikutwa na hatia na kuhukumiwa kwenda jela miaka mitano na viboko vitano kila siku. Baada ya hukumu Juma alilia sana na kujutia. Akajisemea moyoni asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Lakini majuto yake hayakusaidia kitu kwani majuto ni mjukuu.

**UFAHAMU**

1. Juma alikua na tabia gani?
    - Juma alikua na tabia ya wizi

2. Kikundi cha Juma kiliitwaje?
    - Kikundi cha Juma kiliitwa mbwa mwitu.

3. Juma na wenzake walikwenda kuiba wapi?
    - Juma na wenzake walikwenda kuiba nyumbani kwa mzee Musa

4. Juma na wenzake waliiba nini?
    - Juma na wenzake waliiba televisheni, redio, deki na kompyuta

5. Mzee Musa alipofyatua risasi ilimpata nani?

- ❖ Mzee Musa alipofyatua risasi ilimpata Juma mguuni

6. Mzee Musa alipiga simu wapi?
   - ❖ Mzee Musa alipiga simu kituo cha polisi

7. Polisi walimpeleka Juma wapı kutibiwa
   - ❖ Polisi walimpeleka Juma hospitali

8. Juma na wenzake walihukumiwa kwenda jela miaka mingapi?
   - ❖ Juma na wenzake walihukumiwa kwenda jela miaka mitano

**MIUNDO**

Tunga sentensi kwa kutumia miundo ifuatayo

a) Matatizo………………………………………………………………………………

Matatizo mengi yamesababishwa na mafisadi

b) Hapana budi…………………………………………………………………………….

Hapana budi kuwa waadilifu

c) Pamoja na hayo……………………………………………………………………….

Pamoja na hayo walimsikiliza kwa makini

d) Japokuwa………………………………………………………………………

Japokuwa mvua ilinyesha tuliendelea na safari

e) …………………….alipofika…………………………………………….

Mwalimu alipofika alitufundisha kutunga hadithi

**METHALI**

**Orodhesha methali zote zilizotumika katika hadithi**

a) Sikio la kufa hahisikn dawa
b) Siku za mwizi ni arobaini
c) Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu
d) Mbio za sakafuni huishia ukingoni
e) Hakuna marefu yasiyo na ncha
f) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
g) Majuto ni mjukuu

MWL

**Eleza mafunzo yanayopatikana katika methali hizi**

**a) Sikio-la-kufa halisikii dawa**

**MAFUNZO**

- ❖ Jambo lililokwisha kuharibika ama kwenda mrama haliwezekani kunusuriwa, lazima liharibike.

**b) Siku za mwizi ni arobaini MAFUNZO**

- ❖ Huwezi kushamiri katika uovu milele ipo siku utafahamika na kuumbuka

**c) Asiyefunzwa na mamaye hufunnzwa na ulimwengu MAFUNZO**

- ❖ Yeyote aliyekosa kufudishwa adabu na ndugu jamaa zake wa karibu, taabu na matatizo ya dunia yatamtunza na kumwadabisha

**d) Asiyesikia la mkuu huvunjika guu MAFUNZO**

- ❖ Anayekataa makanyo ama mafundisho apewayo na wakubwa zake huishia kufikwa na mabaya ambayo angesikilıza pengine angeyaepuka

**e) Majuto ni mjukuu MAFUNZO**

- ❖ Mtu hujuta madhara ama athari za matendo yake baada ya kulitenda jambo na si kabla

**f) Hakuna marefu yasıyo na ncha MAFUNZO**

- ❖ Kila jambo hufikia hkomo, hata liwe gumu au baya namna gani

**NAHAU**

**Toa maana ya nahau zifuatazo**

1. Angukia pua
   - ❖ Shindwa vibaya
2. Bwaga matusi
   - ❖ Toa matusi mengi
3. Kata kauli
   - ❖ Fariki.
4. Kata maini
   - ❖ Umiza sana hisia, shtua sana
5. Pata kichwa

- Pata kiburi au jeuri kutokana na cheo, mafanikio au sifa

6. Piga chuku
- Tia chumvi, weka uongo mwingi

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Andika kinyume cha sentensi zıfuatazo**

1. Dada alifunua chupa
- Dada alifunga chupa

2. Fundi alifunga tairi la garı
- Fundi alifungua tairi la

3. Makuli walipakia shehena katika meli
- Makuli walipakua shehena katika meli

4. Ukipanda juu usisahau tochi
- Ukishuka chini ukumbuke tochi

5. Mama ameanika mahindi
- Mama amaeanua mahindi

6. Aliinuka baada ya kula
- Alikaa baada ya kula

7. Dada alipanga vitabu kabatini
- Dada alipangua vitabu kabatini

8. Mafundi wanazibua mtaro
- Mafund wanaziba mtaro-

9. Juma ameharibu kabati
- Juma ametengeneza kabati

10. Mama anafumua nywele
- Mama anasuka nywele

11. Fatuma amehifadhi takataka
- Fatuma ametupa takataka

12. Watoto wanacheka sana

- ❖ Watoto wanalia sana

13. Wanakijiji wamepanda mazao
    - ❖ Wanakijiji wamevuna mazao

14. Baba alijenga banda la kuku
    - ❖ Baba alibomoa banda la kuku

**Chagua jibu sahihi kutoka katika parandesi ( mabano)**

1. Mama ni hodari wa kupika (plau, pilau)
    - ❖ Mama ni hodari wa kupika pilau

2. Maji yalijaa (pomoni, komoni)
    - ❖ Maji yalijaa pomoni

3. Kesho tutapiga kuchagua viongozi (kula, kura)
    - ❖ Kesho tutapiga kura kuchagua viongozi

4. Ali ka baada ya kuanguka hadharani (athiri, adhirika)
    - ❖ Aliadhirika baada ya kuanguka hadharani

5. Kila mtu humwabudu apitapo (Mungu, Mlango, Mti)
    - ❖ Mlango

6. Mama Alikwenda sokoni miguu (na, kwa, ya)
    - ❖ Mama alikwenda sokoni kwa miguu

7. Dada ni mpole saia yangu, wangu, vyangu)
    - ❖ Dada yangu ni mpole sana

8. Kaka mchicha jana jioni (anakula, atakula, alikula)
    - ❖ Kaka alikula mchicha jana jioni

9. Juma shuleni sasa hivi (alikwenda, anakwenda, akatembea)
    - ❖ Juma anakwenda shuleni sasa hivi

10. Mimi na dada hadithi (anasoma, wanasoma tunasoma)
    - ❖ Mimi na dada tunasoma hadithi

**Taja methali ambayo inaweza kutumika kutokana na maelezo haya**

1) Chui alivamia zizi la mzee Hamisi na kukamata mbuzi. Alipotoka na mkuki kumkabili alishindwa Akapiga yowe wanakijiji wakakusanyika. Wakampiga chut hadi wakamuua
**METHALI**
Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu

2) Dereva aliendesha gan kwa kasi na kusababisha ajali mbaya
**METHALI**
Haraka haraka hama Baraka

3) Mtoto alilelewa vibaya na hatimaye akawa jambazi
**METHALI**
Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo

4) Ndege alijenga kiota kwa kuchukua jani moja moja na hatimae kiota kikakamili
**METHALI**
Haba na haba hujaza kibaba

**ANDIKA VISAWE VYA MANENO YAFUATAYO**

1) Tisa - kenda
2) Beseni - karai
3) Wali- ubwabwa
4) Jogoo- jimbi
5) Ndoto - njozi
6) Godoro - tandiko
7) Duara - Mviringo
8) Familia – aila
9) Ziro - sifuri
10) Mashaka – hofu
11) Bamia - binda
12) Huzuni – majonzi
13) Siri-faragha
14) Mazishi – matanga
15) Uso - wajihi

MWL

**Andıka vitawe (maneno yenye maana zaidi yamoja vyunraneno aya-**

**1. Paa**

- Kwenda ( enda juu)
- Mnyama wa porini anayefanana na mbuzi
- Sehemu ya juu ya nyumba

**2. Kaa**

- Sehemu yenye moto wa kuni
- Mnyama wa majini
- Kuwa mahali fulani kwa muda

**3. Fua**

- Unda vyombo/vifaa mbalimbali kwa kutumia chuma
- Ondoa uchafu kwenye ngao/ osha nguo

4 Kiboko

- Mnyama mkubwa wa baharini
- Silaha inayotumikia kwa kuchapa au kupiga

5. Vua

- Toa nguo kutoka mwilini
- Toa samaki kwenye maji

6. Mbuzi

❖ Mnyama anaefugwa
❖ Kifaa au chombo cha kukunia nazi

**e. Kuandika kumbakumbu za mkntano kwa kuzingatia vipengele vyake vya uandishi**

**Mkutano maana**

Mkutano ni Mkusanyiko wa watu wenye agenda au lengo maalumu lililopangwa na kuendeshwa na mwenyekiti, katibu na wajumbe.

Kumbukumbu za mkutano maana

Kumbukumbu za mkutano ni rekodi zinazowekwa na katibu wa mkutano wakati mkutano unapoendelea ili kuhifadhi yanayojadiliwa na kukubaliana katika mkutano huo. Ni muhimu kuandıka kumbukumbu za mkutano ili kusaidia na kurahisisha utekelezaji wa mambo yanayoamuliwa Pia kurahisisha marejeo ya mambo yaliyoanzimwa katika mkutano kwa siku za baadaye.

**MUUNDO WA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO**

1. Kichwa cha kumbukumbu
    - Kichwa cha kumbukumbu kinapaswa kutaja mambo yafuatayo

a) Ni mkutano wa akina nami
b) Unaandaliwa wapi?
c) Unaandaliwa lini?
d) Unaanza saa ngapi

Kwa maneno mengine kichwa cha kumbukumbu huonesha malengo, tarehe, saa, na mahali mkutano ulipofanyika.

**Mfano**

Kumbukumbu za mkutano wa Rotary club shuleni ulioandaliwa tarehe tano April 2020 katika ukumbi wa mkutano kuanzia saa tano.

**2) Rekodi ya mahudhurio**
**Huorodhesha**

a) Waliohudhuria kwa kuanza na viongozi wa kikao
b) Orodha ya waliokosa kuhudhuria kwa udhuru
c) Orodha ya waliokosa kuhudhuria bila udhuru
d) Urodha ya waliokosa kuhudhuria bila udhuru
e) Waalikwa- majina ya waliohudhuria huandikwa kwa kutangulizwa vyeo vyao na kuzingatia nafasi zao.

**iii) Ajenda**

- Haya ni mambo ya kuzungumziwa ambayo huorodheshwa kwa kutegemea umuhimu wake. Kila agenda huandikwa maelezo yake yakionesha kilichojadiliwa.na kilichoazimwa

iv) Kufungua mkutano

- Mara nyingi Mwenyekiti ndıye anayefungua mkutano Mwenyekiti akishafungua mkutano, katibu aandike saa ya kufungua kikao na muhtasari wa yaliyozungumzwa.

v) Mengineyo

- Hapa ni mambo mengine yanayozungumzwa ambayo siyo sehemu ya ajenda

vi) Kufunga mkutano

- Baada ya majadıliano ya ajenda, mwenyekiti hufunga mkutano katibu azingatie muda wa kikao kufungwa. Baada ya mkutano katibu apitie tena kumbukumbu hizo ili aziandike vizuri na kuzihifadhi kwa ajıli ya marejesho ya mkutano ujao. Kumbukumbu hizo zitiwe saini na mwenyekiti na katibu kisha wakati wa mkutano mwingine zisambazwe na kusomwa na wajumbe wa mkutano.

vii) Tarehe ya mkutano ujao

- Hapa hutajwa tarehe ya kikao kingine kitakachofanyika siku za usoni.

viii) Kimalizio

- Hii-ni sehem-imayoachwa wazi ya majina ya mwenyekiti na katibu na sehemu ya kutia saini. Baada ya kumbukumbu kusomwa na kuthibitishwa na wajumbe, mwenyekiti na katibu watie saini ya kuonesha uthibitisho huo.

**KUANDIKA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO**
**KIKAO CHA HARUSI YA ADAMU DOTO KILICHOFANYIKA TAREHE 12.3.2020 NYUMBANI KWAO TEGETA.**

**WALIOHUDHURIA**
1. Doto kajichema – mwenyekiti
2. Musa Hasani – makamu mwenyekiti
3. Husna Amil - mweka hazina
4. Abdul Juma - katibu
5. Simon petro- Mjumbe
6. Upendo shujaa - mjumbe

**WASIOHUDHURIA KWA UDHURU**
1. Banki Juma - Mgonjwa
2. Chirwa Mgosi-ana kikno-kingine-

**WASIOHUDHURIA BILA UDHURU**
1. Musa abasi
2. Juma songambele
3. Paulo zakayo

**AJENDA**

i. Kufungua kikao
ii. Kusomwa na kuthibitisha kwa kumbukumbu za mkutano uliopita
iii. Yatokanaye na kumbukumbu hizo
iv. Kupeana majukumu
v. Mengineyo
vi. Kufungua kikao/mkutano

KUFUNGUA KIKAO/MKUTANO

Mkutano ulifunguliwa saa 10:00 jioni na mwenyekiti na kisha kumwomba sauda Juma afanye sala fupi.

KUPITIA NA KUIDHINISHA KUMBUKUMBU ZA KIKAO KILICHOPITA

Kumbukumbu za mkutano uliopita zilisomwa. Wajumbe walikubaliana kuwa ziliakisi yote yaliyozungumzwa katika mkutano uliopita. Baadaye, mwenyekiti na katibu walitia sahihi kuthibitisha.

**YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU HIZO**

1. Ilielezwa kuwa sh. 550,000/=zilizolipwa kwa ajili ya mapambo ni malipo halisi ya mapambo peke yake. Hivyo inabidi kulipia fedha nyingine kwa ajili ya glasi.
2. Kadi za mwaliko - Bwana harusi mtarajiwa alipewa jukumu la kufuatilia na alitoa taarifa kuwa amepata kadi alızozipenda kwa bei ya sh. 1200 kwa kadi moja Alishauriwa atafute kadi za bei nafuu zaidi ili kuendana na bajeti.

**MICHANGO**

Waliopunguza ahadı zao ni

1. Simony petro sh 200,000/=
2. Upendo shujaa sh 150,000/= Jumla 350,000/=

**KUPEANA MAJUKUMU**

**Kamati ya chakula**

**Watakaoshughulikia na kamati hii ni**

1) Upendo strujaa
2) Abduli Juma

**Kamati ya usafiri**

1. Musa Hasani

2. Dodo kadichema

**Kamati ya vinywaji**

1. Husna Amil
2. Upendo Shujaa

Kugawa kadi za michango
Katibu aliwasilisha kadi za kuomba michango ziligawanywa kama ifuatavyo

1. 1 Musa Hasanı alichukua kadı 5
2. Abduli Juma alichukua kadi 15
3. Upendo shujaa alichukua kadi 4

**MENGINEYO**

Ndugu upendo shujaa aliwafahamisha kuwwa kamwene ana kikundi cha ngoma ya mdumange kinachokodishwa kwa Sh 200,000/= iwapo kitahitajika. Iliamuliwa kwamba suala hilo lisubiri halı ya fedha.

**KUFUNGA MKUTANO**

Mkutano ulifungwa na mwenyekiti mnamo saa 12:30 Jioni kwa sala Pia mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria mkutano kwa kuchangia mawazo yao. Ilıkubaliwa kuwa mkutano mwingıne utafanyika 12.4.2020 saa kumi (10:00) jioni Tegeta.

**UTHIBITISHO**

| | **Saini** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| Mwenyekiti | ……………………………. | ………………………… |
| Katibu | …………………………….. | ………………………… |

**UFAHAMU**Jibu maswali yafuatayo

1. Nini maana ya mkutano?
   - ❖ Mkutano ni Mkusanyıko wa watu wenhye agenda au lengo maalumu lililopangwa na kuendeshwa na mwenyekiti katibu na wajumbe.

2. Kichwa cha kumbukumbu kınapaswa kutaja mambo gani?
   - ❖ Kinapaswa kutaja malengo, tarehe, saa na mahali pa kufanyia mkutano.

3. Katika uandıshi wa kumbukumbu za mikutano, sehemu ya mahudhurio hugawanyika katika sehemu ndogo ngapi?
   - ❖ Sehemu ya mahudhurio imegawanyika katıka sehemu ndogo tatu nazo ni

MWL

1. Waliohudhuria
2. Wasiohudhuria kwa udhuru
3. Wasiohudhuria bila udhuru

**MSAMIATI**

Toa maana ya msamiati na kisha tunga sentensi kwa kutumia msamiati

**1. Mkutano**

- ❖ Mkusanyiko wa watu kwa ajili ya kujadiliana jambo maalumu au kusikiliza hotuba.

**SENTENSI**

- ❖ Mwenyekiti wa kijiji aliandaa mkutano ili kuwahamasisha wanakijiji watunze mazingira

**2. Katibu**

- ❖ Mtu anayefanya kazi za kuandika kumbukumbu na kuhifadhi maandishi ya shirika, kampuni au chama.
- ❖ Ofisa au mfanyakazi angepewa wadhifa maalumu na shirika, kampuni au chama
- ❖ Katibu mkuu mtendaji mkuu katika wizara au taasisi Fulani

**SENTENSI**

- ❖ Katika mahafali ya darasa la saba mwaka 2019 mgeni rasmi alikua ni katibu wizara ya Elimu sayansi na Teknolojia.

**3. Ajenda**

- ❖ Orodha ya mambo yatakayozungumzwa kwenye mkutano

**SENTENSI**

- ❖ Mwalimu mkuu aliandaa ajenda za mkutano wa wazazi na kamati ya shule

**4. Saini**

- ❖ Maandishi ya jina la mtu ya kuthibitisha au kuidhihirisha kutendeka au kupatikana kwa kitu au jambo fulani
- ❖ Toa idhini ya kutendeka au thibitisha kupatikana kwa kitu au jambo fulani kwa kuandika jina lako, kitendo cha kutia saini.

**SENTENSI**

- ❖ Tulipofanya mtihani wa Taifa wa darasa la nne kila somo tulitia saini.

**NAHAU**

**Toa maana ya nahau zifuatazo kisha zitungie sentensi**

**i) Ana kwa ana**

- -Kutana na mtu

**SENTENSI**

- Tulipotoroka shule tulikutana na mwalimu ana kwa ana

**ii) Acha kwenye mataa**

- Telekeza au acha mtu nyuma, acha mtu bila yeye kutarajia.

**SENTENSI**

- Tulipokua kwenye sherehe wakati wa kurudi nyumbani dada alituacha kwenye mataa

**iii) Fuata nyayo**

- Fuata matendo au mwenendo wa mtu

**SENTENSI**

- Kaka alifuata nyayo za baba yake

**iv) Fungasha**

- Panga vitu kwa ajili ya safari au kuhama mahali Fulani
- Nenepa hasa sehemu za makalio

**SENTENSI**

- Tulipokwenda likizo tulifungasha mizigo mingi

**v) Hata kwa dawa**

- Kamwe, goma kutenda kitu, katu

**SENTENSI**

- Dada alisema hata kwa dawa hawezi kuiba vitu vya watu.

**vi) Inamisha uso**

- Ona haya au huzuni, ona aibu

**SENTENSI**

- Mwizi alıpokamatwa na wananchi wenye hasira aliinamisha uso kanakume

**vii) Jikaza kiume**

- Vumilia kwa ujasıri

**SENTENSI**

- Mdogo wangu alipochomwa sindano alijikaza kiume

**viii) Kata na shoka**

- Uzuri, umahiri na ukubwa uliopitiliza, isiyo ya kawaida

**SENTENSI**

- ❖ Harusi ya dada yangu ilikua ya kukata na shoka

**ix) Kaza buti**

- ❖ Ongeza juhudi katika kutenda

**SENTENSI**

- ❖ Mwalimu wa Kiswahili alituambia tukaze buti katika masomo.

**x) Kwa moyo mkunjufu**

- ❖ Tendajambo kwa kulipenda au bila kinyongo, tenda jambo kwa furaha

**SENTENSI**

- ❖ Shangazi alitukaribisha kwa moyo mkunjufu

**METHALI**

**Andika methali zinazofanana au zinazofananishwa na methali zifuatazo**

1. Abadi abadi kama hukata jiwe
   Methali inayofananishwa
   **Chovya chovya humaliza buyu la asali**

2. Baada ya dhiki faraja
   Methali inayofananıshwa
   **Mchumia juani hulia kivulini**

3. Cha mywenzio si chako
   Methali
   inayofananishwa
   **Chakupewa si chako**

4. Damu nzito kulıko maji
   Methali inayofananishwa
   **Mla nawe hafi nawe ili mzaliwa nawe**

5. Elimu bahari haishi kwa
   kuchotwa Methali
   inayofananıshwa
   **Elimu haina mwisho**

6. Fahali wawili hawakai zizi
   moja Methali inayofananishwa
   **Akunyimaye kunde akupunguzia mashuzi**

**7.** Fimbo ya mbali haiuwi nyoka Methali inayofananıshwa **Fua chuma kingali moto**

8. Fuata nyuki ule asalı Methali inayofananishwa **Simba mwenda pole ndiye mla nyama**

**9.** Haba na haba hujaza kibaba Methali inayofananishwa **Tone na tone hujaza bahari**

**10.** Ivumayo haidumu Methali inayofananishwa **Chema hakidumu**

**11.** Jembe halimtupi mkulima Methali inayofananishwa **Mgaagaa na hali wali mkavu**

**12.** Jungu kuu halikosi ukoko Methali inayofananishwa **Koti la mzee halikosi chawa**

**VITENDAWILI**

Tegua vitendawili vifuatavyo

1) Afuma hana mshale Nungunungu

2) Akitembea huringa hata akiwa hatarini Jongoo

3) Akopa halipi

Kaburi

4) Baba amenipiga na kuninyima chakula lakini mama amenipiga na kunipa chakula
Nyigu na nyuki

5) Baba yuko ndani na ndevu zake zimechomoza
nje Hadi na simgazake

6) Nyumba yangu ndogo lakini wapangaji
wengi Kiberiti

7) Fatuma
mchafu Ufagio

8) Ghala lake limejaa punje za
mahindi Kinywa

9) Haji kwetu ilakwa kelele
Mvua iambatanayo na radi au ngurumo

10) Hakionekani wala hakishikiki lakini
kipo Upepo na hewa

11) Hamwogopi
mtu Kifo au
njaa

12) Hana miguu lakini huenda wala huwezi kumshinda
mbio Nyoka

13) X111. Hata mzungu
ameshindwa Kifo

14) Hausimiki
hausimami Mkufu,
kamba au uzi

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Sentensi zifuatazo zipo katika kauli halisi na kauli taarifa bainisha kauli hizo**

1. Lete vijiko vitatu
   - ❖ Kauli halisi

2. Walimpelekea maji ya kuoga
   - ❖ Kauli taarifa

3. Walimuuliza kama amewahi kupanda mlima Kilimanjaro
   - ❖ Kauli taarifa

4. Musa alituambia "siwezi klatheza mpra

- ❖ Kauli taarifa

5. Twendeni naona giza linaanza kuingia
    - Kauli halisi

6. Naomba unichotee maji.
    - Kauli halisi

7. Malizeni kazi mpumzike.
    - Kauli halisi

8. Dada alisema kwamba ataanzisha genge
    - Kauli taarifa

9. Kaeni chini
    - Kauli halisi

10. Jana sikulala kabisa.
    - Kauli halisi

11. Nani anagonga mlango?
    - Kauli halisi

12. Alituambia tuzilinde rasilimali zetu
    - Kauli taarifa

13. Amesema hawezi
kupigana Kauli taarifa

14. Aliwaambia wamsubiri
kituoni Kauli taarifa

**Ondoa silabi katika maneno ili kuunda neno jipya**

1. Butwaa-twaa
2. Hamasa - hasa
3. Mchumba - chumba
4. Chelea- lea
5. Angamiza - ngamia
6. Kifani - fani
7. Ajali - jali
8. Anasa - nasa
9. Dhihakr - haki

10. Bainisha - baini
11. Hadharani – hadhara
12. Azizi - zızı
13. Uzazi - uza
14. Duara - dua
15. Kitasa -tasa
16. Barafu - bara bafu
17. Mkufu - mfu

**Tumia silabi "n" au "li" kukamilisha maneno yafuatayo**

1. Wa - **wali**
2. Se_ ka_ **serikali**
3. Ma**__mali**
4. Mala**___**a **malaria**
5. Ka**___**pia **karipia**
6. **___**poti **ripoti**
7. **____**ma **lima**
8. **___**sala**____risala**
9. Re**____reli**
10. Si**____Siri**

**F. Kuandika Risala Fupi Kwa Kuzingatia Muundo Na Kanuni Za Uandishi Risala Maana**

**Risala ni** taarifa fupi inayosomwa mbele ya kiongozi mgeni rasmi kwa niaba ya kundi fulani la watu ili kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi. Ni aina ya taarıfa ambayo hupelekwa kwa mtu au watu inayoeleza haja inayotakiwa.

**Risala Imegawanyika Katika Sehemu Kuu Tatu.**

1. **Mwanzo**
   Hapa panahusu salamu, ukaribisho na lengo la risala.
2. **Kati**
   Hapa ndipo kiini cha risala ambacho huonesha mafanikio, matatizo, mapendekezo nk.
3. **Mwisho**
   Mwisho wa rısala hueleza msisitizo na shukrani

**Risala Ya Wanakijiji Wa Pasua Kwa Mkuu Wa Wilaya Katika Ziara Yake Kijijini Hapo Tarehe 05.07.2020**

Ndugu mgeni rasmi ndugu viongez-wa-tarafa na kata nduou vionaoziwa kim cha pasua mabibi na mabwana.

Ndugu mgeni rasmı sisi wanakijiji wa pasua tunayo furaha kubwa kukukaribisha kwa mara ya kwanza kijijini kwetu. Tunaona ni heshima kubwa kwetu kuja kutembelewa nawe. Tunasema karibu sana.

Kufika kwako kutakuwezesha kuona na kushuhudia shughuli mbalimbali za uvuvi hapa kijijini kwetu.

Ndugu mgeni rasmi, kijiji hiki kilianzishwa miaka kumi iliyopita. Awali kilianza na wavuvi themanini tu. Lakini kadri walivyopata mafanikio ndivyo walivyowavutia wavuvi wengine kuja kijijini hapa Mpaka sasa kijiji kina wavuvi mia mbili na hamsini wakiwemo wanawake ishirini. Watu hao wote hujipatia ajira na kipato kutokana na shughuli za uvuvi.

Ndugu mgeni rasmı, halı ya uvuvi katıka kijiji chetu haijawa bora kwani wengi wao wanatumia zana duni za uvuvi. Pia wanatumia nishati ya mkaa ili kukaushia samaki. Ukosefu wa umeme unaifanya nishati ya mkaa iwe ndıyo pekee inayotegemewa na wavuvi.

Ndugu mgeni rasmi, tunasikitika sana kukueleza kwamba, matumizi ya nishati ya mkaa imepelekea uharibifu mkubwa wa mazingira iwe ndiyo pekee inayotegemewa na wavuvi. Ndugu mgeni rasmi, tunasikitika sana kukueleza kwamba, matumizi ya nishati ya mkaa imepelekea uharibifu mkubwa wa mazingira. Hivyo kusababisha kijiji chetu kuwa na upungufu mkubwa wa mvua pamoja na upepo mkali na vimbunga vilevile mito nayo inakauka.

Ili kukabili tatze hilo, sisi wanakijiji wa pasua tumeanzisha shamba la miti lenye ukubwa ekari mia mbili. Sisi wanakijiji wa pasua shughuli yetu ya uvuvi imetuwezesha kujenga makazi ya kudumu. Hivyo tunaiomba serikali ituletee umeme.

Mwisho ndugu mgeni rasmi, tunashukuru kwa kuja kututembelea, kuona maendeleo yetu na kusikiliza ma yetu. Ndugu mgeni rasmi tuna imani utafikisha maombi yetu kwenye vyombo vinavyohusika na kuwashawishi waweze kutuletea umeme. Pindi upatapo wasaa tunakukaribisha uje tena kututembelea. Asante.

**UFAHAMU**

**Jibu maswali yafuatayo kutokana na risala**

1. Risala ni nini?

- Risala ni taarifa fupi inayosomwa mbele ya kiongozi mgeni rasmi kwa niaba ya kundi fulanı la watu ili kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hili kwa kiongozi

2. Kijiji kilichoandaa risala hiyo ni kinaitwaje?
   - Kijji kilichoandaa risala hiyo kinaitwa pasua

3. Wanakijiji wa pasua wanajishughulisha na shughuli gani?
   - Wanakijji wa pasua wanajishughulisha na shughuli za uvuvi

4. Kijiji kilianzishwa miaka mingapi iliyopita?
   - Kijiji kilianzishwa miaka kumı iliyopita

5. Shughuli za uvuvi zimeathiri vipi mazingira ya kiiji cha pasua
   - Shughuli za uvuvi zimeathiri mazingira kwa kijiji kukumbwa na uhaba wa mvua, mito kukauka, upepo mkali na vimbunga.

6. Nani alikuwa mlengwa katika risala?
   - Aliyekua mlengwa katika risala ni mkuu wa wilaya

7. Wanakijiji wa pasua walimuomba nini mgeni rasmi?
   - Wanakijiji wa pasua walimuomba mgeni rasmi awashawishi vyombo vinavyo husika wapate nishati ya umeme
8. Risala imegawanyika katika sehemu ngapi?
   - Risala imegawanyika katika sehemu tatu.

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Bainisha aina za maneno katika sentensi zifuatazo**

1. Dada alikua anajisomea chumbani N Ts T E
2. Mama amekwenda sokoni N T E
3. Ameanguka mara mbili T E
4. Mtoto mzuri anaandika vizuri N V T E
5. Mbwa mkali amegongwa na gari N V T U N
6. Wale ni watoto wema W U N

V

**Panga herufi zilizochanganywa ili zilete neno sahihi**

1. Luime - elimu
2. Rasada- darasa
3. Windava - viwanda
4. Ngilu – nguli
5. Ruchaka – charuka
6. Yinbom - nyimbo

**BADILI VITENZI KUWA KATIKA KAULI ZA UTENDAJI ZIFUATAZO**

| | KUTENDA | KUTENDWA | KUTENDEA | KUTENDEWA | KUTENDEANA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuma | Tumwa | Tumia | Tumiwa | Tumiana |
| 2 | Andika | Andikwa | Andikia | Andikiwa | Andikiana |
| 3 | Peleka | Pelekwa | Pelekea | Pelekewa | Pelekeana |
| 4 | Piga | Pigwa | Pigia | Pigiwa | Pigiana |
| 5 | Chora | Chorwa | Chorea | Chorewa | Choreana |
| 6 | Tazama | Tazamwa | Tazamia | Tazamiwa | Tazamiana |
| 7 | Kusanya | Kusanywa | Kusanyia | Kusanyiwa | Kusanyiana |
| 8 | Funga | Fungua | Fungia | Fungiwa | Fungiana |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Sem | Semwa | Semea | Semewa | Semeana |
| 10 | Chunga | Chungwa | Chungia | Chungiwa | Chungiana |

**Taja Kauli Za Utendaji Za Sentensi Zıfuatazo**

1. Baba amesoma gazeti - kutenda
2. Mpira umeibwa na wezi- kutendewa
3. Mwalimu anaandika ubaoni – kutenda
4. Mwalimu anaandika ubaoni - kutenda
5. Mwizi alipigwa vilivyo - kutendwa
6. Bibi amechotewa maji -kutendewa
7. Wanafunzi waliandikiana barua - kutendeana
8. Juma na Ali wanatazamana usoni - kutendana
9. Wanakijiji walikusanyika kusubiri mkutano - kutendeka
10. Ubao wetu ulichorwa -kutendewa

Kamilisha methali zifuatazo

1. Shibe mwana malevya njaa mwana malegeza
2. Penye nia pana njia
3. Hakuna masika yasiyokuwa na mbu
4. Hasira hasara
5. Hauchi hauchi unakucha
6. Kanzu ya kuazima usivae ijumaa
7. Kata pua uunge wajihi
8. Jifya moja haliinjiki chungu
9. Jitihada haiondoi kudura
10. Jogoo wa shamba hawiki mjini
11. Jungu kuu halikosi ukoko
12. Kauli ni bora kuliko mali
13. Kiburi si mwaungwana
14. Kidole kimoja hakivunji chawa
15. Mchagua jembe si mkulima
16. Penye miti hapana wajenzi

MWL

**G. Kuandika Insha Kimantiki Kuhusu Elimu Ya Afya Na Uzazi Insha Maana**

Insha ni kifungu cha maneno kilichopangwa kwa mpangilio maalum wenye kueleza kuhusu jambo fulani lililopangwa katika aya.

**MUUNDO WA INSHA**

**Kimuundo insha imegawanyika katika sehemu kuu nne**

1. Kichwa-eke-inshe-
2. Utangulizi wa insha
3. Kiini cha insha/lengo la insha
4. Mwisho wa insha

**1. KICHWA CHA INSHA**

Huandikwa mwanzoni kabisa mwa insha na pia huandikwa katikati juu ya insha kwa herufi kubwa na hupigiwa mstari. Mara nyingi kichwa cha insha huandikwa kwa maneno machache

**2. UTANGULIZI WA INSHA**

Sehemu hii hufuata baada ya kichwa cha insha na hueleza kwa ufupi jambo linalozungumziwa.

**3. KIINI CHA INSHA/LENGO**

Hii ni sehemu kuu kabisa. Sehemu hii hufuata baada ya utangulizi. Pia hii ndiyo sehemu ambayo mwandishi huelezea kwa undani zaidi kuhusu jambo alililoliandika. Kila jambo analolizungumzia katika sehemu hii lazima liwe katika aya.

**4. MWISHO WA INSHA**

Hii ni sehenu ya mwisho ya insha Mwandishi hutumia msisitizo na ufupisho wa yale aliyoyaandika Pia mwisho wa insha huanza katika aya

Mambaya kuzingatia-katika-insha

1. Kuzingatia kichwa cha habari na maelezo kama yapo
2. Kuandika kwa kutumia taratibu za uandishi na lugha fasaha
3. Kutotumia lugha ya mkato kama vile mwl badala ya mwalimu
4. Kuandika utangulizi unaovuta umakini wa wasomaji au wasikilizaji
5. Kuandika kiini cha insha kwa mpangilio unaofaa Kila wazo kuu lipewe aya yake. Mawazo ya aya zote yahusiane.
6. Kuandika mwisho wa insha unaovutia ili wasomaji wapende kuendelea kusoma.

**Umuhimu wa uandishi wa insha**

i. Hukuza uwezo wa mwandishi kujitambulisha kimaandishi.au hata kimazungumzo
ii. Mwanafunzi hupata ujasiri pale anapokua na uzoefu katika kuandika

MWL

iii. Huwa ni kigezo cha kumpa mwanafunzi uwezo wa kuzitumia fani za lugha
iv. Hukuza lugha na upanuzi wa misamiati hivyo huwa kurunzi ya kumwongoza awe mtaalamu
v. Huwa ni kielelezo cha kumbainishia mwanafunzi kiwango alichofikia kiubunifu.

**INSHA**
**ELIMU YA AFYA NA UZAZI**

Elimu ni njia ambayo hutumiwa na jamii kwa ajili ya kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Afya ni hali nzuri ya mwili bila maradhi. Elimu ya afya na uzazi ni elimu inayotolewa kwa ajili ya kupangilia afya ya uzazi.

Elimu ya afya na uzazi ina umuhimu mkubwa katika jamii kwanza husaidia kupangilia idadi ya watoto mtu anaowahitaji au idadi ya watoto anaoweza kuwahudumia

Pili elimu ya afya na uzazi husaidia mtu aweze kupangilia jinsi ya kupishanisha watoto. Yaani pawe na muda wa kutosha kati ya mtoto aliyetangulia na atakayefuata na hii inapelekea mzazı kuwa na wezo wa kujishughulisha na shughuli za maendeleo.

Tatu elimu ya afya na uzazi husaidia mama na mtoto kuwa na afya njema Kwani mzazi hupata muda mrefu wa kumhudumia mtoto wake hasa kunyonyesha kwa muda mrefu.
Pia elimu ya afya na uzazı husaidia kupungua kwa watoto wa mitaani. Wengi wa watoto wanaozaliwa bila mpangilio mzuri, wazazi wao hushindwa kuwapa huduma zinazotakiwa na matokeo yake huzagaa mitaani.

Vilevile elimu ya afya na uzazi huisadia serikali kuwa na mipango mizuri ya kutoa huduma za jamii matibabu, elimu, maji na umeme kwa urahisi. Katika kutilia mkazo elimu ya afya na uzazi, serikali imeanzisha mafunzo katika vituo vya afya. Kuna wataalamu wa afya ya mama na mtoto ambao kazi yao ni kuwaelimisha mama na baba juu ya elimu ya afya na uzazı.

Zipo changamoto zinazokwamisha kusambaa kwa elimu hii ya afya na uzazi. Baadhi ya changamoto hizo ni mila potofu za baadhi ya makabila ambayo huamini kuwa, watoto wengi ni utajiri wakati sio kweli. Wanaume wengi kutokubaliana na elimu hiyo hivyo kukataa kwenda kliniki pamoja na wake zao.

Hivyo elimu ya afya na uzazi ina umuhimu sana katika maendeleo ya jamii, hasa kwa wazazi na nchi kwa ujumla. Kwa wazazi elimu hiyo huwasaidia kupangılia namna ya kuzaa watoto wanaoweza kuwahudumia, kwa nchi husaidia kuweza kupangilia namna ya utoaji huduma za jamii kama vile matibabu na elimu.

**Ufahamu**

**Jibu Maswali Yafuatayo**

1. Kwa mujibu wa insha elimu ya afya na uzazi ni nini?
   - ❖ Elimu ya afya na uzazi ni elimu inayotolewa kwa ajili ya kupangilia afya ya uzazi.

2. Elimu ya afya na uzazi hutolewa wapi na hutolewa na nani?
   - ❖ Elimu ya afya na uzazi hutolewa katika vituo afya na hutolewa na wataalamu wa afya.

3. Nini maana ya elimu kwa mujibu wa insha hii?
   - ❖ Elimu ni njia ambayo hutumiwa na jamii kwa ajili ya kupitisha maarifa, ujuzi na maadili kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.

4. Ni changamoto gani inakwamisha kusambaa kwa elimu ya afya na uzazi?
   - ❖ Changamoto inayokwamisha kusambaa kwa elimu ya afya na uzazi ni mila potofu kwa baadhi ya makabila ambayo huamini kuwa watoto wengi ni utajiri. Pia wanaume wengi kutokubaliana na elimu ya afya na uzazi na kukataa kwenda kliniki pamoja na wake zao.
5. Nini chanzo cha watoto wa mitaani?
   - ❖ Chanzo cha watoto wa mitaani ni kutokua na elimu ya afya ya uzazi.
6. Nini faida ya elimu ya afya na uzazi Faida ya elimu ya afya na uzazi ni
   i. Husaidia kupangilia idadi ya watoto mtu anayoweza kuwalea
   ii. Husaidia kupishanisha watoto kwa kipindi fulani cha muda mfano; Muda kati ya mtoto miaka mitatu.
   iii. Husaidia mama na mtoto kuwa na afya njema kwani mzazi hupata muda wa kutosha wa kumhudumia mtoto hasa kumnyonyesha kwa muda mrefu
   iv. Husaidia kupungua kwa watoto wa mitaani
   v. Husaidia serikali kuwa na mipango mizuri ya kutoa huduma za jamii kama vile maji, umeme, matibabu elimu.

MWL

**VITENDAWILI**

**Tegua vitendawili vifuatavyo**

i. Afahamu sana kuchora lakini hajui achoracho KONOKONO

ii. Ajenga ingawa hana mikono NDEGE

iii. Ana macho lakini
haoni POPO

iv. Blanketi la babu
haliraruki ULIMI

v. Bwana mkubwa kaanguka na mikotikoti
yake MGOMBA

vi. Chungu changu cha udongo
hakipasakr MJUSI

vii. Daima hunifuata nyuma, nijaribupo kumfuatia
hunikimbia KIVULI

viii. Gari hili la ajabu hata lofa
analo MIGUU

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Tumia viambishi po, ko, na mo katika sentensi zifuatazo**

1. Musa yu Dodoma
   Musa yuko Dodoma

2. Maji ya_________
   mtungini Maji yamo
   mtungini

3. Wanakijiji wa________________porini kutafuta
   kuni Wanakijiji wapo porini kutafuta kuni

4. Mama yu____________________njiani
   Mama yuko njiani

5. Nguo zi________kabatini
   Nguo zimo kabatini

6. Panya yu_________________shimoni
   Panya yumo shimoni

7. Gari li nje ya nyumba
   Gari liko nje ya nyumba

8. Pikipiki i______________chini ya mti

Pikipiki ipo chini ya mti

9. Dada yu darasanı
   Dada yumo darasani

10. Dada yu shuleni
    Dada yuko
    shuleni.

**Tumia nahau zifuatazo kukamilisha sentensi zifuatazo**
**Vunja sheria, chapwa viboko, kata rufaa, piga kura, tilia shaka, toza faini, shika usukani, zunguka mbuyu, mkono mrefu, toa ya mwaka**

1. Wote tunam ______Asha kuwa ndiye aliyeiba simu
   - ❖ Wote tunamtilia shaka Asha kuwa ndiye aliyeiba simu

2. Siku hizi Anasia ana_____kwani ukiacha kitu huwezi kukikuta
   - ❖ Siku hizi Anasia ana mkono mrefu kwani ukiacha kitu huwezi kukikuta

3. Tuliamua ku_____baada ya kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa
   - ❖ Tuliamua kukata rufaa baada ya kutoridhishwa na hukumu iliyotolewa.

4. Tabia yaku _ imewapeleka jela watu wengi
   - ❖ Tabia ya kuzunguka mbuyu imeshawapeleka jela watu wengi

5. Uki___za nchi utahukumiwa kwenda jela
   - ❖ Ukivunja sheria za nchi utahukumiwa kwenda jela

6. Wanafunzi wote waliochelewa wali___na mwalimu wa zamu
   - ❖ Wanafunzi wote waliochelewa walichapwa viboko na mwalimu wa zamu

7. Wiki ijayo tuta______kuchagua viongozi wa shule
   - ❖ Wiki ijayo tutapiga kura kuchagua viongozi wa shule.

8. Baba alim____mtu anayeingiza mifugo shambani kwake
- ❖ Baba alimtoza faini mti aliyeingiza mifugo shambani kwake

9. Katika kata yetu, shule yetu ina
- ❖ Katika kata yetu shule yetu inashika usukani katika taaluma

**Pigia Mstari Viambishi Vinavyoonesha Wakati Katika Vitenzi**

1. Wanacheza - wanacheza- wakati uliopo
2. Watashinda - watashinda - wakati ujao
3. Alifariki – alifariki - wakati uliopita
4. Anakimbia - anakimbia - wakati uliopo
5. Alimsaidia - alimsaidia - wakati uliopita

**Tumia irabu a e. o, u kujaza nafasi ili kuunda maneno**

1. Kidond **kidonda**
2. K_z_mb_n **kizimbani**
3. Sh reh **sherehe**
4. H_k_m_ **hakimu**
5. T mb **tembo, tambi**
6. J m _jamii , **jamaa**
7. R_shw_r**ushwa**
8. J_k_f_**jokofu**
9. Ch p **chupa**

**1.4 Kutumia Msamiati Katika Kuandaa Matini Mbalimbali**
**A. Kuandika Sentensi Kwa Kutumia Maneno Yanayoonesha Umiliki**

**Sentensi maana**
- ❖ Sentensi ni kipashio cha juu kabisa katika tungo, chenye muundo wa kiima na kiarifu ambacho hutoa taarifa kamili.

AU
- ❖ Sentensi ni kifungu cha maneno kuanzia neno moja na kuendelea chenye kiima na kiarifu, kinacholeta maana kamili.

MWL.

**AINA ZA SENTENSI**

i. **Sentensi sahili**

- ❖ Hii ni aina ya sentensi iliyoundwa kwa kishazi huru kimoja tuu. Mfano mama anakula

ii. **Sentensi changamano**

- ❖ Hii ni haina ya sentensi iliyoundwa na kishazi tegemezi na kishazi huru. Mfano, mtoto aliyeondoka kwa shangwe na vigelegele amepotea.

iii. **Sentensi ambatano**

- ❖ Hii ni-aima ya Sentensi ilryoundwa kwa sentensi mbili zilizounganishwa na kiunganishi mfano:
- ❖ Baba analima na mama anasoma gazeti

iv. **Sentensi shurutia**

- ❖ Hi ni aina ya sentensi inayoundwa kwa mofimu za masharti au ni aina ya sentensi yenye kuonesha masharti mofimu za masharti ni Ki, nge, ngeli. Mfano Akija anione

**MUUNDO WA SENTENSI**

Sentensi huundwa na sehemu kuu mbili ambazo ni

i. Kiima
ii. Kiarifu

**Kiima**

- ❖ Hii ni sehemu katıka sentensi ambayo hukaliwa na mtenda au mtendwa wa jambo.
- ❖ Mfano:- Baba yangu, Mtoto mrefu

**Kiarifu**

- ❖ Hii ni sehemu katika sentensi ambayo huonesha au huarifu tendo lililofanywa, linapofanya au litakapofanywa
- ❖ Mfano:- Ameondoka, anaimba vizuri

**MANENO YANAYOONESHA UMILIKI**

Haya ni maneno yanayoonesha uhusiano uliopo baina ya vitu viwili au zaidi ambapo kimoja kinamilikiwa na kingine.

Mfano

- ❖ Mama yangu anaumwa
- ❖ Mbuzi wetu ametumbukia kisimani
- ❖ Nguo zangu zimeibwa

**Jibu Maswali Yafuatayo**

**Bainisha Vimilikishi Katika Sentensi Zifuatazo**

1. Kitabu changu kimepotea

2. Gari lao linatoa moshi kuchoma
3. Nyumba yetu imejengwa kwa matofali
4. Mtoto wangu amefaulu
5. Kwao kuna mbuzi wengi
6. Viatu vyake vimeliwa na mchwa
7. Kijiji chao kina miti mıngi
8. Funguo zangu zimepotea
9. Chumba cha darasa letu ni kidogo sana
10. Kalamu yake imeandika vizuri
11. Lugha yetu ya asili ni kichaga
12. Ni jukumu lao kutunza mazingira
13. Mwajiri wao alisikia kilio chao
14. Miguu yangu inauma
15. Mbuzi wenu amegongwa na gari

**Mazoezi Ya Lugha**
**Badılh Sentensi Zifuatazo Kuwa Katika Halı Ya Mazoea**

1. Mama anakula mahindi ya kuchoma
2. Mjomba aliendesha pikipiki kwa uangalifu
3. Kaka aliendesha baiskeli kwenda shule
4. Dada anajibu barua zote alızoandikiwa na rafiki yake
5. Baba atatembelea wagonjwa wakati wa likizo
6. Mtoto wa mjomba anainwa binamu
7. Wakulima rananalılia mabhinds mara mbilı kwa mwak
8. Mtoto wa mjomba anaitwa binamu
9. Wakulima wanapalilia mahindi mara mbili kwa mwaka
10. Gari linatoa moshi mwingi
11. Mjomba atakuja na mtoto wake nyumbani
12. Mbwa wetu anabweka kiona wageni

**Majibu**

MWL.

1.Mama hula mahindi ya kuchoma
2.Mjomba huendesha pikipiki kwa uangali

fu
3.Kaka
huende
sha
baiskel
i
aendap
o
shuleni
4.Dada hujibu
barua zote
aandikiwazo na
rafiki yake
5.Baba
hutembelea
wagonjwa
wakati wa
likizo 6.Mtoto
wa mjomba
huitwa binamu
7.Wakulima hupalilia
mahindi mara mbili
kwa mwaka 8.Gari
hutoa moshi mwingi
9.Mjomba huja na mtoto wake nyumbani
10. Mbwa wetu hubweka aonapo wageni

**Tunga sentensi kwa kutumia nahau zifuatazo**

1. Piga marufuku
   - ❖ Mwenyekiti wa kijiji amepiga marufuku ukataj, ovyo wa miti

2. Kaza mwendo
   - ❖ Bibi alikaza mwendo kufika kijiji cha jirani

3. Fanya juu chini
   - ❖ Wazazi walifanya juu chini kuhakikisha utoro wa watoto unakoma

4. Bega kwa bega
   - ❖ Wanakijiji walishirikiama bega kwa bega kutunza mazingira

5. Unga mkono
   - ❖ Wananchi wote waliunga mkono Azimio la Arusha

6. Piga vita
   - ❖ Mwalimu mkuu alipiga vita utoro wa shuleni

7. Punde si punde
   - ❖ Punde si punde mwalimu aliingia darasani

8. Pigwa na butwaa
   - ❖ Wote walipigwa na butwaa tuliposikia Juma kaiba kuku

9. Moyo mweupe
   - ❖ Dada alinipa fedha kwa moyo mweupe

10. Kata maini
    - ❖ Mjomba alinikata maini aliponiambia habari za msiba wa bibi.

MWL.

**Pigia Mstari Neno Lililotofauti Na Maneno Mengine**

1.Panga, kisu, **mizani,** bunduki, mkuki
2.Asali, sukari, muwa, pipi, **shubiri**
3.Mahabusu, rumande, hakimu, **mhenga,** mfungwa
4.Kaburi, jeneza, maiti, **kitabu,** sanda
5.Mshororo, **ndizi**, mizani, vina, kituo
**6.**Mwalimu, dawati, kitabu, mwanafuzi, chaki, **mswaki**
7.Basi, treni**, redio,** pikipiki, baiskeli,
8.Vijana, wazee, watoto, vikongwe, **visu,** wajane

9.Kiti, meza, kabati, **bakuli,** kochi, kitanda
10. **Ubani,** karatasi, bahasha, stempu, kalamu
11. Mchicha, **juisi,** kisamvu, kabeji, tembele
**12.** Ugali, makande, pilau, biriani, **chenza**

**Pigia Mstari Vivumishi Katika Sentensi Zifuatazo**

1. Mkimbiaji **hodari** ameshinda mbio za marathoni
2. Mama amenunua gauni **jipya**
3. Mtoto **mzuri** amepotea
4. Uchafu **wote** umezagaa
5. Shule ile ina walimu **wachache**
6. Mjukuu **wangu** anapenda maziwa
7. Mama ni **mpole**
8. Mti **mrefu** umevunjika
9. Mwanafunzi **mtiifu** husoma kwa bidii
10. Mbwa **mweusi** amegongwa na gari **jeupe**

**Panga Sentensi Zifuatazo Katika Mpangilio Sahihi**

1. Walikata miti hiyo kulingana na vipimo vilivyoandikwa katika karatasi
2. Walianza kuchora mchoro katika karatasi isiyo na maandishi
3. Mihambo na Kabula walitafakari jinsi ya kutengeneza toroli la miti
4. Kazi ya kutengeneza toroli iliwachukua siku nzima sasa wanalitumia kusombea maji
5. Baadae walikwenda katika msitu ulio jirani na nyumbani kwao kutafuta miti

MWL

**MPANGILIO**

1. Mihambo na kabula walitafakari jinsi ya kutengeneza toroli la miti
2. Walianza kuchora mchoro katika karatasi isiyo na maandishi
3. Baadae walikwenda katika msitu ulio jirani na nyumbani kwao kutafuta miti
4. Walikata miti hiyo kulingana na vipimo vilivyoandikwa katika karatasi
5. Kazi ya kutengeneza toroli iliwachukua siku nzima sasa wanalitumia kusombea maji

**B. Kuandikrbabari-Fupi Kwa Kutumia Majina Sahihi Ya Kazi Za Watu**

**Habari Fupi Ni Maelekezo Yanayotolewa Kwa Ufupi Kuhusu Jambo Fulani Au Tukio Fulani**

**KAZI ZA WATU**

1. Rubani - mtu anayeendesha ndege
2. Daktari - mtu anayetibu watu
3. Mwalimu - mtu anayefundisha
4. Dobi- mtu anayefua nguo kwa pesa

**Soma Habari Ifuatayo Kisha Jibu Maswali**

Manka anaishi katika kijiji cha lokiri katika wilaya siha mkoani Kilimanjaro. Kijiji hiki kimebarikiwa kuwa na wakazi wengi wenye kazi zao. Kundi la kwanza ambalo ndio wengi mi wakulima na wafugaji kundi la pili ni wafanyakazi kama vile, walimu, madaktari, manesi, wanajeshi na wafanyakazi wengine. Kundi la tatu ni la watu waliojiajiri wenyewe kama vile fundi mwashi, fundi cherehani, wavuvi, sonara

Manka ni mhasibu katika benki ya NMB iliyopo kijijini hapo. Manka anao ndugu watatu, wa kwanza ni rubani, wa pili ni nahodha na wa tatu ni mhandisi. Manka pia hujishughulisha na kilimo cha mbogamboga anapotoka kazini ili kujiongezea kipato. Wanakijiji wa lokiri wanampenda Manka kwa kua ana adabu na anapenda ushirikiano na wanakijiji wenzake.

**UFAHAMU**

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Kijiji cha Lokiri kipo katika wilaya gani
   - Kijiji cha Lokini kipo katika wilaya ya Siha

2. Watu wanaishi katika kijiji cha Lokiri wapo katika makundi mangapi? Yataje.
   - Watu wanaoishi katika kijiji cha lokiri wapo katika makundi matatu. Makundi hayo ni, wakulima na wafugaji, wafanyakazi kama vile walimu, manesi, madaktari, na waliojiajiri wenyewe kama vile fundi, cherehani, fundi mwashi, wavuvi.

MWL

3. Manka anafanya kazi gani?
   - Manka ni mhasibu katika benki ya N MB

4. Manka anao ndugu wangapi?

- Manka anao ndugu watatu

5. Ndugu wa pili wa Manka anafanya kazi gani?
    - Ndugu wa pili wa Manka ni Nahodha

6. Mbali na uhasibu Manka hujishughulisha na kazi gani nyingine
    - Mbali na uhasibu manka hujishughulisha na kilimo cha mbogamboga

**MSAMIATI**

**Toa maana ya msamiati kisha tunga sentensi**

**i. MHANDISI**

Mtu mwenye maarifa na ujuzi wa kuunda, kutunza na kutengeneza mitambo, majengo na vitu mbalimbali (injinia)

**Sentensi**

Waziri wa ujenzi alimfukuza kazi mhandisi aliyetengeneza daraja chini ya kiwango

**ii. MHASIBU**

- Mtu anayetunza hesabu na fedha za ofisi, shirika na kampuni

**Sentensi**

- Baba alipofungua kampuni aliajiri mhasibu wa kampuni

**iii. RUBANI**

- Mtu anayeendesha na kuongoza chombo kama vile ndege

**Sentensi**

- Rubani aliendesha ndege kwa uangalifu mkubwa

**iv. WILAYA**

- Sehemu ndogo katika jimbo au mkoa lakini kubwa kuliko tarafa

**Sentensi**

- Mkuu wa wilaya aliwahimiza wananchi wake kutunza mazingira

**v. KIJIJI**

- Mahali panapoishi watu wengi pamoja ambapo si mji

**Sentensi**

- Kijiji cha songambele kimeshika usukani katika utunzaji wa mazingira.

MWL

Taja majina ya kazi za watu wafuatao

i. Mtu anayelima mazao mbalimbali shambani huitwa MKULIMA
ii. Mtu anayefanya kazi ya kununua na kuuza bidhaa huitwa MFANYA BIASHARA
iii. Mtu mwenye taaluma ya ujuzi wa kubuni, kutengeneza au kurekebisha madaraja, barabara, au mitambo huitwa MHANDISI
iv. Mtu anayefanya kazi ya kuvua samaki huitwa MVUVI
v. Mtu anayeongoza chombo kinachosafiri majini huitwa NAHODHA
vi. Mtu anayeazimisha vitabu maktaba huitwa MKUTUBỊ
vii. Mtu anayefanya kazi ya kurusha ndege huitwa RUBANI
viii. Mtu anayefanya kazi ya kufua vyuma huitwa MHUNZI
ix. Mtu anayefanya kazi ya kulinda nchi yake pamoja na mipaka ya nchi yake huitwa MWANAJESHI
x. Mtu anayefanya kazi ya kulinda raia na mali zake huitwa POLISI
xi. Mtu anayefundisha chuo kikuu huitwa MHADHIRI
xii. Mtu anayefanya kazi ya kutafsiri mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine huitwa MKALMANI
xiii. Mtu anayefanya kazi ya kujenga nyumba kwa kutumia matofali au mawe huitwa FUNDI MWASHI
xiv. Mtu anayefanya kazi ya kuamua kesi mahakamani huitwa HAKIMU
xv. Mtu anayefanya kazi ya kutibu wagonjwa huitwa DAKTARI
xvi. Mtu anayetengeneza samani (faida) kwa kutumia mbao huitwa FUNDI SEREMALA
xvii. Mtu anayefuga wanyama kama vile ng'ombe mbuzi nk., MFUGAJI
xviii. Mtu anayetengeneza, hereni, bangili kwa kutumia madini huitwa SONARA
xix. Mtu anayefanya kazi ya kutunza hesabu na fedha za ofisi au kampuni huitwa MHASIBU
xx. Mtu anayefanya kazi ya kufua na kupasi kwa Malipo huitwa DOBI
xxi. Mtu anayefanya kazi ya kutoa taaluma huitwa MWALIMU

MWL.

MAZOEZI YA LUGHA

Andika kinyume cha maneno yafuatayo

Jenga-bomoa

i. Fumba-fumbua
ii. Pana-nyembamba
iii. Upendo- chuki
iv. Asali- shubiri

v. Mnunuzi- muuzaji
vi. Refusha- fupisha
vii. Kaza-legeza
viii. Twika- tua
ix. Tega- tegua
x. Lia-cheka
xi. Msafi-mchafu

**Andika methali zinazoweza kuhusianisha na vifungu vifuatavyo vya habari**

1) Sketi yangu ya shule ilitoboka kidogo baada ya kukalia msumari uliochomoza katika dawati. Kutokana na mimi kutotilia maanani sketi ilizidi kuchanika. Hivi sasa nashindwa hata kulishona

❖ **USIPOZIBA UFA UTAJENGA UKUTA**

2) Walimu na wazazi walimwonya mbwana kuhusu kutumia muda wake vizuri lakini yeye hakujali. Hata wenzake walipojaribu kumweleza aliwajibu kuwa bado wakati unatosha na kwamba atasoma mitihani itakapokaribia Mwezi mmoja kabla ya mitihani aliugua na kulazwa Aliruhusiwa wiko moja isingetosha kwa maandalizi ya mtihani

❖ **ASIYESIKIA LA MKUU HUVUNJIKA GUU AU MAJUTO NI MJUKUU**

3) Timu yetu ya Taifa iliweza kuifunga timu ya Ghana katika uwanja wa Taifa. Ushindi huu umechangiwa na hamasa iliyokuwepo uwanjani. Watanzania wote waliokuwepo uwanjani walishangilia mwanzo hadi mwisho wa mpira kuchezea nyumbani kuliwapa ari kubwa wachezaji

❖ **MCHEZA KWAO HUTUNZWA**

4) Asha alijiajiri kwa kufungua duka lenye bidhaa mbalimbali watu walifurika kununua vitu dukani na wengine kukopa. Hakua akiweka kumbukumbu ya wadeni wake wala mahesabu yake. Taratibu duka likanza kudorora na kupata hasara kubwa. Hivi sasa amelifunga kabisa

❖ **MALI BILA DAFTARI HUPOTEA BILA HABARI**

**Tunga Sentensi Kwa Kutumia Vifungu Vifuatavyo Vya Maneno**

1. Kuwa makini
   Mwalimu alitusisitiza kuwa makini na masomo

2. Ninaamini kwambwa wakati umefika
   Ninaamini kwamba wakati umefika wa mdogo wangu kuanza darasa la kwanza

3. Wengi kaia sralu
   Mkutano ule wa injili ulikuwa na watu wengi kama siafu

4. Watoto yatima
   Kila mwaka mpya unapofika baba huwapa watoto yatima zawadi

5. Mambo yangemwendea kombo
   Asingesoma kwa bidii mambo yangemwendea kombo

**C. Kuandika Shairi Linaloelezea Muonekano Wa Hali Ya Hewa Katika Mazingira Kwa Kuzingatia Kanuni Za Ushairi.**

**SHAIRI - MAANA**

Shairi ni tungo yenye kutumia mapigo ya silabi kwa utaratibu maalumu wa kimuziki kwa kutumia lugha ya mkato au lugha ya picha

**AINA ZA MASHAIRI**

**i) MASHAIRI YA KIMAPOKEO**

Haya ni mashairi yanayozingatia kanuni za ulinganifu wa mizani, vina na idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katika shairi.

**ii) MASHAIRI YA KISASA**

Haya ni mashairi yasiyozingatia kanuni za kimapokeo yaani hayazingatii kanuni za ulinganifu wa mizani, vina idadi ya mistari katika kila ubeti na kituo katıka shairi.

**HALI YA HEWA**

Hali ya hewa ni hali ya anga la sehemu inavyobadilika kila mara. Hali hiyo inaweza kuwa ya mawingu, mvua, joto, baridi au upepo.

**MSAMIATI**

**Toa maana ya maneno yafuatayo kisha tunga sentensi kwa kila neno**

**i) Majira**

- Kipindi maalumu cha hali ya hewa
- Mwendo wa kawaida wa saa

**Sentensi**

- Mwalimu alituambia wakati wa majira ya baridi ni vizuri kuvaa nguo nzito

**ii) Ukame**

- Hali ya nchi kuwa kavu kiasi cha kutoweza kupata mavuno ya kutosha

**Sentensi**

- Mwenyekiti wa kijiji aliwaambia wanakijiji wenzake wapande miti mingi ili kujiepusha na ukar

MWL

**iii) Kiangazi**

- Majira ya mwaka wakati jua linapokua kali baina ya vuli na masika

**Sentensi**

- Mama alituambia kipindi cha kiangazi tuhakikishe tunakunywa maji mengi

**iv) Maji**

- Kiowevu kinachopatikana kutokana na mvua katika bahari maziwa, mito n.k

**Sentensi**

- Bibi alitutuma kisimani tukamchotee maji

**v) Kipupwe**

- Majira ya baridi yanayotokea katika miezi ya Juni, Julai, na Agosti kwa Afrika ya mashariki.

**Sentensi**

- Kipindi cha kipupwe miti mingi hupukutisha majani

MWL.

# KUONESHA UELEWA WA JAMBO ALILOSIKILIZA AU KULISOMA

**2.1. Kusikiliza na kuonesha uelewa juu ya jambo alilosikiliza**
**a) Kusikiliza habari na kujibu maswali yatokanayo na habari**
Shujaa ni mtu mwenye moyo wa ujasirn katika kukabili mambo hata kama ni hatari. Mambo ya kishujaa yanaweza kuwa ni kupigana vita na maadui, kupambana na majambazi hatari, kuokoa watu katika janga fulani, kupambana na wanyama wakali na kukomboa watu kutoka katika utawala wa kikandamizaji na katika unyonyaji.

Katika historia, Bara la Afrika liliwahi kuvamiwa na kutawaliwa na wakoloni. Waafrika wengi walipinga uvamizi wa wakoloni wakiongozwa na machifu wao.

Wakoloni walipokuja kulivamia Bara la Afrika, hapo hapo kuna machifu wa jamii mbalimbali walikataa na kupinga uamuzi huo. Walipambana na wakoloni ili wasieneze utawala wao. Viongozi hao waliona hapana budi kutetea himaya zao. Miongoni mwa watawala hao ni mtwa mkwawa wa mtemi Mirambo katika Tanzania. Shaka Zulu wa Afríka kusini na kabaka Mutesa wa Uganda. Hawa walisimama kidete kuhakıkisha wanapambana na wakoloni ili wasiwatawale maeneo yao na wananchi kuonewa.

Wakati Bara la Afrika lilipokuwa linatawaliwa na wakoloni, waliibuka wapigania uhuru wa nchi zao. Wao walipigania uhuru tuliokuwa tumenyanganywa na wageni. Mashujaa hao ni kwame Nkurumah wa Ghana, mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania, Samora Masheli wa Msumbiji. Hao walipambana na ukoloni hadi waliporejesha uhuru wa nchi zao na wakoloni wakafunga virago vyao na kundi makwao.

Baada ya uhuru wa nchi zao, mashujaa hao wamebakia kuwa watu muhimu wa kukumbukwa katika historia ya Bara la Afrika.

Wengi wao hawakuwa na tamaa ya madaraka. Mfano Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ni kiongozi aliyeamua kuachia madaraka akıwa na nguvu, anapendwa na watu na bado alikua na uwezo wa kuongoza. Nelson Mandela ni kiongozi mwingine ambaye baada ya kuikomboa Afrika kusini kutoka kwa makabaru, aliongoza kwa miaka mitano kisha akaachia madaraka

**UFAHAMU**
1. Shujaa ni mtu wa namna gani?

❖ Shujaa ni mtu mwenye moyo wa ujasiri katika kukabili mambo hata kama ni ya hatari.

2. Taja vitendo vya kishujaa Vitendo vya kishujaa ni

1. Kupigana vita na maadui
2. Kupambana na majambazi hatari
3. Kuokoa watu katika janga fulani
4. Kukomboa watu katika utawala wa kikandamizaji

3. Katika historia Bara la Afrika liliwahi kuvamiwa na kutawaliwa na nani?

❖ Katika historia Bara la Afrika liliwahi kuvamiwa na kutawaliwa na wakoloni

4. Taja machifu waliopambana ili ukoloni usienee ni

a) Machifu waliopambana ili ukoloni usienee ni:-
b) Mtwa mkwawa wa Tanzania
c) Mtemi mirambo wa Tanzania
d) Shaka zulu wa Afrika kusini
e) Kabaka metesa wa Uganda

5. Kwame Nkurumah alipigania uhuru wa nchi gani?

❖ Kwame Nkurumah alipigania uhuru wa Ghana

6. Viongozi gani ambao hawakuwa na uroho wa madaraka.

❖ Viongozi ambao hawakuwa na uroho wa madaraka ni mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Nelson Mandela wa Afrika ya kusini.

**MSAMIATI**

**Toa maana ya msamiati na kisha tunga sentensi**

**i) Shujaa**

Mtu mwenye moyo thabiti anayeweza kukabili mambo hata kama ni ya hatari.

Sentensi

Mwalimu wa historia alituambia mwalimu Julius Nyerere alikua shujaa Mwanamapinduzi

MWL.

**ii) Vita**

Mapigano baina ya watu, wanyama, au mataifa

Sentensi

Baba yangu aipigana Vita-ya pth-ya dunua

**iii) Koloni**

❖ Nchi inayotawaliwa na nchi nyingine yenye walowezi walioshika madaraka

**Sentensi**

❖ Babu yangu aliniambia elimu ya kikoloni ilikua ya kibaguzi

**iv) Uhuru**

❖ Hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine, hali ya kufanya mambo bila kuingiliwa.

**Sentensi**

❖ Nchi yetu ya Tanzania ilipata uhuru mwaka 1961

**METHALI**

**Kamilisha methali zifuatazo**

**1.** Ada ya mja hunena, **muungwana ni kitendo**
**2.** Avumae baharini papa**, na wengine wamo**
**3.** Furaha ya mwenye meno, **kibogoyo hashiriki**
**4.** Halali yako **haramu kwa mwenzako**
**5.** Hapana **siri ya watu wawili**
**6.** Heri kenda shika **kuliko kumi nenda rudi**
**7.** Ivumayo **haidumu**
**8.** Jembe halimtupi **mkulima**
**9.** Kata pua **uunge wajihı**
**10.** Kataa neno **usikatae wito**
**11.** Kauli ni bora **kuliko mali**
**12.** Heri umfadhili mbuzi **binadamu ataakuudhi**
**13.** Kipendacho roho, **hula nyama mbichi**
**14.** Kitanda usichokilalia **huwajui kunguni wake**
**15.** Kuishi kwingi ni **kuona mengi**
**16.** Kuku mgeni **hakosi kamba mguuni**
**17.** Kuteleza siyo **kuanguka**
18 Kuvuja kwa pakacha **nafuu kwa mchukuzi**
**19.** La kuvunda **halina ubani**
**20.** Leo ni leo asemaye **kesho ni mwongo**
**21.** Macho **hayana pazia**
**22.** Maji **hufuata mkondo**
**23.** Mali bila **daftan hupotea bda habarr**
**24.** Manahodha wengi **chombo huenda mrama**
**25.** Mbio za sakafuni **huishia ukingoni**
**26.** Mkataa pema **pabaya panamuita**
**27.** Mkono **mtupu haulambwi**
**28.** Mla mla leo **mla jana kala**

MWL

**nini MAZOEZI YA LUGHA**

**Kanusha sentensi zifuatazo**

1. Fundi huyu ameshona nguo zangu vibaya
    - Fundi huyu hajashona nguo zangu vibaya

2. Kiranja amewahi shuleni
    - Kiranja hajawahi shuleni

3. Kiatu hiki ni kipya
    - Kiatu hiki si kipya

4. Shule ina upungufu wa samanı
    - Shule haina upungufu wa samani

5. Shambani kwetu ni mbalı na mjini
    - Shambani kwetu si mbali na mjini

6. Kutembea gizani ni kuzuri
    - Kutembea gizani si kuzuri

7. Shule yetu ina maktaba kubwa
    - Shule yetu haina maktaba kubwa

8. Huyu ni daktari bingwa
    - Huyu si daktari bingwa

9 Kazi ya kulima ina changamoto kubwa
    - Kazi ya kulima haina changamoto kubwa.

10. Mwajuma m mtoro
    - Mwajuma si mtoro

MWL.

11. Mtoto mkorofi hupendwa na mwalimu
    - Mtoto mkorofi hapendwi na mwalimu

12. Salumu aliishia darasa la sita
    - Salumu hakuishia darasa la sita

13. Rushwa huwaathiri watu wenye fedha tuu
    - Rushwa haiwaathiri watu wenye fedha tuu

14. Kwetu kuna milima mingi

- Kwetu hakuna milima mingi

**ANDIKA SENTENSI ZIFUATAZO KATIKA WINGI**

1. Mshahara wa mfanyakazi umechelewa
   Mishahara ya wafanyakazi
   imechelewa
2. Fundi alipanda juu ya nyumba kuezeka bati
   Mafundi walipanda juu ya nyumba kuezeka
   mabati
3. Kiongozi anayeogopa mtu hawezi kuongoza
   Viongozi wanaoogopa watu hawawezi
   kuongoza
4. Mwandishi wa kitabu kile anaishi mwenge
   Waandishi wa vitabu vile wanaishi
   mwenge
5. Pazia la dirishi limechakaa sana
   Mapazia ya madirisha yamechakaa
   sana
6. Samaki aliyechina hafai kuliwa
   Samaki waliochina hawafai
   kuliwa
7. Gurudumu la gari limepata pancha
   Magurudumu ya magari yamepata
   pancha
8. Mlio wa bunduki ulisikika kutoka
   mbali Milio ya bunduki ilisikika kutoka
   mbali

**Tunga sentensi kwa kutumia nahau**

i. **Angua kilio**
   Shangazi alipoibiwa mkoba wake aliangua kilio
ii. **Chimba dawa**
   Tulipokua tunasafiri kuelekea Bukoba katıkati ya safari abiria walimwomba kondakta kuchimba dawa.
iii. **Fura kichwa**
   Asha aliposhika namba moja alifura kichwa
iv. **Jogoo la pili**
   Siku ya mtihani wa Taifa baba alituamsha jogoo la pili
v. **Kufumba na kufumbua**
   Tuliposatirı kwa ndege kufumba nakufumbua tulifika mwisho wa safari

MWL

**B. Kubaini Miundo Katika Sentensi Wakati Wa Mazungumzo**

Muundo wa sentensi ni sehemu ya sentensi isiyokamilisha sentensi, ili iweze kukamılisha sentensi lazima iongezewe maneno mengi

Mfano

- Japokua……………………..
- ………………kinaganaga………………….
- ………………pasi na……………………….

**Miundo Hukamilishwa Na Kua**

a) Japokua hatukua na pesa za kutosha, tulichangishana mpaka tukaweza kumsaidıa
b) Tulimweleza kinaganaga kuwa tabia yake ya wizi si nzuri
c) Fatuma alingia pasi na kupiga hodi

**Soma Habari Ifuatayo**

Maisha ya utotoni ya Ana kabla kuwa mtu mzima, hayakua mazuri Baada ya kuzaliwa aliishi maisha ya tabu sana. Kabla ya hapo baba yake hakua na kazi ya maana Aliambulia kazi ya kijungu jiko tu. Mama yake alijitahidı ili aweze kumsomesha mwanae. Mara aoke mikate, mara akaange maandazi, mara akaange mihogo ilimradi tu wapate riziki na malezi ya ana yaende vizurı.

Baada ya kufika umri wa kwenda shule. Ana alipelekwa shule kusoma. Ana alikuwa na tabia ya kuwaaga wazazi wake kabla ya kwenda shuleni, baada ya kurudi alımsaidıa mama yake kazı za nyumbanı.

Alijitahıdi kusoma kwa bidu na baada ya kumaliza darasa la saba alichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza huko nako alisoma kwa bidii. Baada ya kumaliza kidato cha nne alifaulu kupata daraja la kwanza, na kuwa mwanafunzi bora nchi nzima. Ama kweli Mungu hamtupi mja wake.

**UFAHAMU**

1. Maisha ya Ana kabla ya kuwa mtu mzima yalikuaje?
   - Maisha ya Ana kabla ya kuwa mtu mzima yalıkua ya taabu sana.

2. Baba yake Ana alikuwa na kazi gani?
   - Baba yake Ana hakua na kazi ya maana aliambulia kazi ya kijungu jiko tu.

3. Mama yake Ana alijishughulisha na shughuli gani hadi akaweza kumsomesha Ana?
   - Mama yake Ana alijishughulisha na shughuli za kukaanga mandazi, mihogo na kuoka mikate.

4. Ana alikua na tabia gani kabla ya kwenda shule
   - Ana alikuwa na tabia ya kuwaaga wazazi wake kabla ya kwenda shule.

5. Ana aliporudi shule alifanya nini
   - Ana alıporudi shule alimsaidia mama yake kazi za nyumbani

MWL.

6. Baada ya kumalıza darasa la saba Ana alichaguliwa kwenda wapi?
   - Baada ya kumaliza darasa la saba Ana alichaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza

7. Ana alipata daraja la ngapi alipohitimu kidato cha nne
   - Ana alıpata daraja la kwanza na kuwa mwanafunzi bora nchi nzima

**MIUNDO**

**Bainisha miundo inayotumika katika habari kisha itungie sentensi**

1. ……………………kabla ya…………………………………………
   - Alikunywa chai kabla ya kunawa uso

2. Baada ya………………………………………………………….
   - Baada ya kumaliza darasa la saba alijiunga na kidato cha kwanza

3. Alijitahidi…………………………………………………………….
   - Alijitahidi kuandika haraka

4. ………………….ilimradi………………………………………….
   - Alisoma ilimradi amridhishe baba yake

5. ……………………….alikuwa………………………………………
   - Sifuni alikuwa na tabia ya uvivu

6. …………………..kwa bidii…………………………………………..
   - Alisoma kwa hidu ili afaulu.mithani yake

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Panga herufi zilizochanganywa ili kuunda neno sahihi**

i. Lemui – elimu
ii. Kiof- kifo
iii. Ng maob - ng'ambo
iv. Omeng- ngome
v. V. Niami - amini
vi. Bututhu - thubutu
vii. Ifna – fani
viii. Matachu - chutama
ix. Mwaek - mwake/ mweka
x. Jumihi- Jihimu
xi. Rikithi -kithiri

MWL

**Pigia Mstari Vivumishi Katika Sentensi Zifuatazo**

1. Baba amenunua kiatu kipya

2. Mkwezi hodari ni

Juma 3 Mtoto

weturamepotea-

4. Mboga zote zimeungua

5. Kijana mrefu ameanguka

**Panga maneno katika sentensi ili yalete maana**

1. Sherehe ni sana chakula cha kitamu
2. Chakula cha sherehe ni kitamu sana
3. Abushiri Bahati pete na hokotwa na mte
4. Pete ya mtemi Abushiri iliokotwa na Bahati
5. Shule mdogo awali ya wangu anasoma
6. Mdogo wangu anasoma shule ya awali
7. Lugha letu la Kiswahili Taifa ni ya
8. Kiswahili ni lugha ya Taifa letu
9. Sana vizuri mwalimu anatufundisha wetu
10. Mwalimu wetu anatufundisha vizuri sana
11. Kijijini likizo nitamtembelea wa bibi wakati
12. Wakati wa likizo nitamtembelea bibi kijijini
13. Kulipa kukopa matanga harusi
14. Kukopa harusi kulipa matanga
15. Ya tulitembelea Taifa sisi maktaba
16. Sisi tulitembelea maktaba ya Taifa
17. Amefaulu wake Hadija mtihani wake vizuri sana
18. Hadija amefaulu mtihani wake vizuri sana
19. Baba mkononi juzi na niliongea simu ya kutumia
20. Juzi niliongea na baba kwa kutumia simu ya mkononi

MWL.

**C. Kubaini Mawazo Makuu Katika Risala**

**Risala;** Ni taarifa fupi inayosomwa mbele ya kiongozi mgeni rasmi kwa niaba ya kundı fulanı la watu ilı kutoa maelezo au kuonesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi. Ni aina ya taarifa ambayo hupelekwa kwa mtu au watu fulani inayoeleza haja inayotakiwa.

**MUUNDO WA RISALA**

Risala imegawanyika katika sehemu tatu

**MWANZO**
Hapa panahusu sana salamu, ukaribisho na lengo la risala

**KATI**
Hapa ndipo kiini cha risala ambacho huonesha mafanikio, matatizo, mapendekezo nk

**MWISHO**
Hueleza msisitizo au shukrani

**SOMA RISALA IFUATAYO KISHA JIBU MASWALI**
**RISALA YA WANAFUNZI WA SHULE YA MSINGI FUKA KWA MGENI RASMI JUU YA SHUGHULI ZA UZALISHAJI MALI**
Ndugu mgeni rasmi, wazazi, walimu na wanafunzi.
Tunayo furaha kubwa kukukaribisha katika shule ya msingi Fuka, ili uweze kuona na kusikia shughuli za uzalishaji mali.

Ndugu mgeni rasmi shule yetu ina wanafunzi mia tao (500), wavulana mia mbili na hamsini (250) na wasichana mia mbili na hamsini (250). Walimu ishirini pamoja na shughuli za kitaalamu, shughuli za uzalishaji mali pia zinatiliwa mkazo.

Ndugu mgenicesmi shule-yetu ina miradi mbalimbali ambayo ni shamba la migomba na mboga za majani. Shamba la Migomba na mboga za majani kwa kipindi cha mwaka mmoja ziliingiza faida shilingi laki tano elfu ishirini.

Ndugu mgeni rasmi pamoja na mafanikio hayo tuna matatizo kadhaa yanayohusu shughuli za uzalishaji mali. Tuna tatizo la pembejeo, bado tunatumia majambe ya mkono katika ulimaji. Hi husababisha wanafunzi watumie muda mrefu.

Ndugu mgeni rasmi tatizo jingine ni tatizo la maji. Kutokana na tatizo hili, shule imeshindwa kupanua shamba la mboga za majani na kukosesha shule mapato.

Ndugu mgeni rasmi tunaomba wizara yako itusaidie ili tuweze kupata mkopo na hatimae tuweze kununua zana za kilimo zilizobora kama trekta na plau. Vilevile itusaidie kufikisha ombi letu la majt kwa Wizara husika ili tuweze kupata maji.

Ndugu mgeni rasmi, tunatumaini utapeleka maombi yetu kunakohusika. Asante.

UFAHAMU

1. Risala hii ilisomwa na wanafunzi wa shule gani?
   Risala hii ilisomwa na wanafunzi wa shule ya msingi Fuka
2. Shule hiyo ina walimu
   wangapi? Shule hiyo ina
   walimu ishirini
3. Shule hiyo inajishughulisha na shughuli zipi za uzalishaji mali
   Shule hiyo inajishughulisha na kilmo cha migomba na mboga za majani
4. Katilka kipindecha mwaka mojaid
   Katika kipindi cha mwaka mmoja miradi yao iliingiza faida ya shilingi laki tano na elfu ishirini
5. Ni changamoto gani shule inapitia katika shughuli za uzalishaji mali
   Changamoto wanazozipata ni ukosefu wa maji pamoja na zana bora za kilimo.

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua neno sahihi kutoka kwenye mabano**

1. Halima alikuwa**_______**bustanini (wanalima, wakulima, wamelima, analima)
   Halıma alikwa **analima** bustanini
**2.** Ndugu wa kiume wa damu moja ni**_____**(rafiki, kaka, dada, mjomba, mwalimu)
   Ndugu wa kiume wa damu moja ni **kaka**
3. Kuku**________**mayai (huzaa, hutaga, hujifungua)
   Kuku **hutaga** mayai
**4.** Hutembea kwa maringo_**_____**(nyoka, kuku, nyuki, kinyonga)
   Hutembea kwva maringo **kinyonga**
5. Mimi**______**mtoto mkubwa kwenye familia yetu (ndiyo, ndiye, ndie )
   Mimi **ndiye** mtoto mkubwa kwenye familia yetu
6. Juma**________________**mpira kila siku (atacheza, hucheza, amecheza)
   Juma **hucheza** mpira kila siku
7. Jana baada ya timu yetu kushinda**_____________**kwa furaha (tutashangilia, tunashangilia, tulishangilia)
   Jana baada ya timu yetu kushinda **tulishangilia** kwa furaha

8. Ni aina mojawapo ya samaki (mamba, bata, perege)
   **Perege** ni aina mojawapo ya samak

MWL.

**Badili sentensi zifuatazo kuwa kauli taarifa**

1. "Mtoto anaimba vizur1 dada amesema
   - Dada amesema kwamba mtoto anaimba vizuri
2. Baba ametuambia "kaka amepewa zawadi baada ya kushinda mbio za marathoni
   - Baba ametuambia kwamba kaka amepewa zawadi baada ya kushinda mbio za marathoni
3. "Nitasafiri kesho asubuhi" mama alisisitiza

- ❖ Mama alisisitiza kuwa atasafiri kesho asubuhi

4. "Mwaka huu nitavuna mazao mengi Mjomba amesema
   - ❖ Mjomba amesema kwamba mwaka huu atavuna mazao mengi
5. Mwalimu alitueleza, "Kiswahili kinafundishwa hadi nje ya nchi yetu
   - ❖ Mwalimu alitueleza kwamba Kiswahili kinafundishwa hadi nje ya nchi yetu
6. "Karanga zote zimeisha shambani" bibi alisema
   - ❖ Bibi alisema kwamba karanga zote zimeisha shambani
7. Mimi nitachezea timu ya Taifa" mwanafunzi alisema
   - ❖ Mwanafunzi alisema kwamba atachezea timu ya Taifa
8. Dada aliniambia" Nitakuletea zawadi
   - ❖ Dada aliniambia kwamba ataniletea zawadi
9. Bibi alitueleza" sitahudhuria mkutano
   - ❖ Bibi alitueleza kwamba hatahudhuria mkutano
10. "Kesho tutakula pilau" Mama alisema
    - ❖ Mama alisema kwamba kesho tutakula pilau
11. "Nitafua kesbo jioni" Mtoto alisema
    - ❖ Mtoto alisema kwamba atafua kesho

jioni 12 Babu aliseE Mwaka-bau-kalme

- ❖ Babu alisema kwamba mwaka huu kilımo kimekubali sana

**D. Kubaini Na Kuchambua Hoja Kuu Zilizotolewa Katika Majadiliano Majadiliano - maana**

Majadiliano ni mazungumzo ya watu wawili au zaidı wanaobadilishana mawazo kuhusu mada fulani

Ni kichocheo cha udadisi na njia ya kuelimishana

Mjadala hufanywa kwa mashindano ambapo upande mmoja hutoa hoja za kutetea jambo linalozungumziwa na upande mwingine hutoa hoja za kupinga. Kila upande hujitahidi kutetea msimamo wao mpaka mwisho. Katika majadiliano kunaweza kuwapo na watu ambao hawafungamani na upande wowote. Hawa huweza kutetea upande fulani, wakati fulani na kuupinga upande huo huo mwingine

**SOMA MAJADILIANO YAFUATAYO KISHA JIBU MASWALI**

**MAISHA YA MJINI NI BORA KULIKO MAISHA YA KIJIJINI**

Vijana wengi wanaamini kwamba maisha ya mjini ni mazuri kuliko maisha ya kijijini. Hivyo hutamani sana kuja mjini ili wawe na maisha mazuri. Wengine hutoroka kutoka kijijini kuja mjini. Wanapofika mjini hukutana na maisha magumu. Hukosa sehemu za kulala, chakula ni shida, fedha wanakua hawana kwa ajili ya matumizi, hivyo hujutia
ELIZA: Habari yako Eva
EVA: Ni nzuri
ELIZA Mh! Eva kuna jambo nataka tujadili mimi na wewe sijui utakua radhi?
EVA: Haina shida Eliza wewe sema tuu
ELIZA HIvi wewe unaonaje hii tabia ya vijana walio wengi huku kijijini kutamani kwenda mjini wanasema eti maisha ya mjin ni mazuri kuliko ya kijijini

EVA Mimi naona hii ni imani potofu kabisa, kwani maisha ya mjini ni magumu mno. Kwanza mjini kila kitu ni lazima ununue hata maji ya kupigia mswaki, tofauti na huku kijijini. Kijijini chakula kipo cha kutosha tunalima wenyewe. Baadhi ya vitu tu ndio tunanunua kama sukari mafuta.

Pili mjini kuna msongamano mkubwa wa watu nyumba zao zipo karibu mno. Na hii hupelekea kuwa na joto kali. Kijijini hakuna msongamano nyumba zipo mbalimbali hivyo tunapata hewa safi na hakuna joto. Tatu mjini kuna kelele hakuna utulivu kama kijijini

ELIZA: Hata mimi naona maisha ya kijijini ni mazuri kuliko ya mjini. Serikali nayo imetukumbuka watu wa vijijini, kwani imetuletea umeme, maji safi ya bomba, zahanati za kisasa, huduma zote muhimu kijijini zinapatikana.

EVA Mimi nadhani vijana waache mawazo potofu ya kwamba maisha ya mjini ni bora kuliko ya kijijini. Wasikimbilie mjini wakumbuke wao ndio nguvu kazi. Wajikite kwenye shughuli za kilimo Kwani uchumi wa nchi yetu unategemea kilimo. Serikali inatoa mbegu, madawa mbolea kwa wakati ili wakulima wasipate shida.

**UFAHAMU**

1. Majadiliano haya yanahusu nini? Au yanazungumzia nini?
    - ❖ Majadiliano haya yanazungumzia maisha ya mjini ni bora kuliko maisha ya kijijini.
2. Ni watu gani wanaona kwamba maisha ya mjini ni bora?
    - ❖ Vijana wa kijijini ndio wanaona maisha ya mjini ni bora
3. Ni changamoto zipi wanazokutana nazo wanapotoka kijijini kuja mjini?
    - ❖ Changamoto wanazokutana nazo ni, kukosa sehemu ya kulala, kukosa fedha za matumizi, kwa ajili ya kununua chakula, maji.

4. Maisha ya mjini yana ugumu gani kulinganisha na maisha ya mjini

❖ Maisha ya mjını yana ugumu ukilinganisha na maisha ya mjini

- Mjini kila kitu ni cha kununua wakati kijijini ni baadhi ya vitu tu ndio hununuliwa
- Mjin-kune-msengamano-wa watu
- Mjini kuna kelele nyingi wakati kijijini kuna utulivu hakuna kelele

5. Serikali imeboresha huduma gani za kijamii huko vijijini
   - ❖ Serikali imeboresha huduma za jamii kama vile maji safi ya bomba, umeme, zahanati za kisasa
6. Wewe unafikiri maisha ya kijijini na ya mjini yapi bora?
   - ❖ Mimi ninafikiri maisha ya kijijini ni bora kuliko ya mjini kwani kijijini unaweza kujiajiri mwenyewe kwa kujikita kwenye kilimo tofauti na mjini.

**METHALI**

**Kamilısha methali zifuatazo**

1. Chanda chema
   - ❖ Chanda chema huvishwa pete
2. Asiye na bahati
   - ❖ Asiye na bahati habahatiki
3. Asiyekubali kushindwa
   - ❖ Asiyekubali kushindwa si mshindani
4. _______________mguu huota tende
   - ❖ Mdharau mwiba mguu huota tende
5. Mfa maji
   - ❖ Mfa maji haachi

kutapatapa 6.___mwenyeji apone

❖ Mgeni aje mwenyeji apone

7. Mkono mmoja___________
   - ❖ Mkono mmoia haulei mwana
8. Nyumbani ni nyumbani______________

Nyumbani ni nyumbani hata pawe shimoni

9. Pilipili usiyoila
   - ❖ Pilipili usiyoila yakuwashia nini?
10. Polepole
    - ❖ Polepole ndio mwendo
11. Polepole ya kobe
    - ❖ Polepole ya kobe humfikisha mbali
12. Radhi za wazee,
    - ❖ Radhi za wazee ni fimbo

maishani 13 Sikio la kufa

❖ Sikio la kufa halisikii dawa

14. Usitukane wakunga
    - ❖ Usitukane wakunga na uzazi ungalipo

**MAZOEZI YA LUGHA**
**Unda maneno kwa njia ya kujirudiarudia**
**Mfano**
**Nane-nanenane**

1. Taka - takataka
2. Pole- polepole
3. Bara - barabara
4. Pili - pilipili
5. Hovyo – hovyo hovyo
6. Piki – pikipiki
7. Upande-upandeupande

**Tunga sentensi mbili zenye maana tofauti kwa kutumia maneno yafuatayo**
**i. Paa**
- ❖ Paa la nyumbe yetu limeehakaa
- ❖ Dada yangu alipaa samaki
- ❖ Ndege ya abiria ilipaa angani kwa kasi

**ii. Meza**
- ❖ Mtoto anameza maziwa kwa shida
- ❖ Meza yetu imetengenezwa kwa kioo

**iii. Mbuzi**
- ❖ Mbuzi wetu ana rangi nyeusi
- ❖ Mama alinunua mbuzi ya kukunia nazı

**iv. Jua**
- ❖ Mama anajua kupika biriani
- ❖ Jaua jua hitkua kalr sana

**V. Paka**
- ❖ Mwajuma anapenda kupaka kucha zake rangi
- ❖ Paka wetu aliua panya watatu

**Andika herufi ya jibu sahihi**

1. Mzee Jongo alitaka kutupatia mwanga wa jambo lile. Nahau ipi ingefaa kutumika hapa?

a. Kututaka radhi
b. Kutuchemsha bongo
c. Kutufungua njia
d. Kututia moyo
e. Kutupa ndimi kali

2. Alivishwa kilemba cha ukoka. Maana ya maneno kilemba cha ukoka ni_
__ a Alinivisha ukoka
b. Alisifiwa mno
C. Alikashifiwa sana
d. Alivishwa kilemba safi
e. Alisifiwa kinafiki

3. Kufuja mali maana yake ni
__ a Kuhifadhi
b. Kuiba mali
C. Kutafuta mali
d. Kutumia mali ovyo
e. Kutumia kwa ubahili

4. Methali ipi inafanana na methali ifuatayo?
Kuku mgeni hakosi kamba mguuni
a. Mcheza kwao hutunzwa
b. Kanguru nwoga Iukimbiza-ubawa
c. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
d. Jogoo wa shamba hawiki mjini
e. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu

5. Alipotaka kuzunguka mbuyu ni_________-
a Kutoroka
b. Kujificha
c. Kuponyoka
d. Kutoa rushwa
e. Kukimbia

6. Itabidi uwaangukie wazazi wako kutokana na mambo uliyowafanyia.
Kuwaangukia wazazi ni_--
a. Kuwadondokea
b. Kuwasamehe

c. Kuwapa zawadi
d. Kuwapiga ngwala
e. Kuwaomba msamaha

7. Malizia methalı ifuatayo, mpofuka ukongweni
a. Haoni ya mbeleni
b. Hasahau yaliyopita
c. Hapati njia
d. Hujua faida
e. Hukumbuk ya ujanani

**MAJIBU**

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| C | E | D | D | D | E | C |

**Badili sentensi zifuatazo kuwa katika halı ya uyakınishi**

1. Mama na baba hawakuamka asubuhi kunisindikiza shuleni
   - ❖ Mama na baba waliamka asubuhi kunisindikiza shuleni
2. Fundi mwashi hakuja kwa wakati
   - ❖ Fundi mwashi alikuja kwa wakati
3. Hazifanyı kazı zake kwa umakini mkubwa
   - ❖ Huzifanya kazi zake kwa umakini mkubwa
4. Banda halıtatosha kuku wote
   - ❖ Banda litatosha kuku wote
5. Mahindi hayakusagwa vizuri
   - ❖ Mahindi yalisagwa vizuri
6. Mtoto hatafuni chakula kwa urahisi
   - ❖ Mtoto hutafuna chakula kwa urahisi

7. Jiko lote-hahkujaa moshi kwa ajili ya kuni
   - ❖ Jiko lote lilijaa moshi kwa ajili ya kuni
8. Hatukupalilia karanga zetu mapema mwaka huu
   - ❖ Tulipalilia karanga zetu mapema mwaka

huu 9 Baba na mama hawakusafiri wakati wa likizo
   - ❖ Baba na mama walisafiri wakati wa likizo

10. Barabara zote hapa kijijini kwetu hazipitiki kwa urahisi
   - ❖ Barabara zote hapa kijijini kwetu zinapitika kwa urahisi
11. Mtoto huyu si mtulivu
   - ❖ Mtoto huyu ni mtulivu
12. Bibi na babu hawakulima mtama
   - ❖ Bibi na babu walilima mtama

13. Gari halikuondoka kituoni mapema

❖ Gari liliondoka kituoni mapema.

**2.2 KUSOMA KWA UFASAHA NA KUONESHA UELEWA WA MATINI MBALIMBALI**

**A. KUSOMA METHALI MBALIMBALI KATIKA KIFUNGU CHA HABARI NA KUELEZA MAANA ZAKE**

**METHALI**

Methalı mi usemi mfupi wa mapokeo wenye mpangılio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jamii husika

Ni kauli fupi yenye pande mbili za fikra ambazo upande wa kwanza huanza na upande wa pili humaliza.

**Mfano**

- ❖ Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

**Maana**

- ❖ Asiyefuata ushauri wa wakuuu wake mabaya humpata

Alıye juu mngoje chini

**Maana**

Anayejitapa ameshafaulu maishani punde atafeli

MWL.

**Soma Habarn Iluatayo Kısha Jibu Maswali**

Mzee Jangala ni mwenyekiti wa kijiji cha samaki maini. Wananchi wa kijiji cha samaki maini ni walevi kupindukia na hawapendi kufanya kazi kwa bidii. Pia hawana ushirikiano katika kazi za kijamii kama vile kutengeneza barabara, kuchimba mtaro.

Siku moja mzee Jangala aliita mkutano wa kijiji Mungu si athumani wanakijiji walijitokeza kwa wingi. Mzee Jangala alianza kwa kuwasalimu wanakijiji wenzake kisha akawaambia. Wanakijiji wenzangu msema kweli ni mpenzi wa Mungu na mficha uchi hazai hivyo lazima niwaeleze ukweli juu ya hiki. Kijiji chetu hakina maendeleo nahii ni kwasababu hatuna ushirikiano.

Tukikubaliana kufanya jambo wanaojitokeza huwa ni wachache sana. Mrtasahau kwamba umoja ni nguvu utengano ni udhaifu. Kama tungejitokeza wote na kushirikiana wote barabara yetu ya kwenda hospitali tungemaliza kuitengeneza Na ni barabara muhimu sana.
Mzee Jangala aliendelea kuwaambia wanakijiji wenzake kwamba. Kijiji chetu wananchi hamfanyi kazı kwa bidii.

Na hii inapelekea badhi ya kaya kushindwa kuhudumia kaya zao kwa kuzipatia mahitaji muhimu kama vile chakula, hata wazee wa zamani walisema mgaa gaa na upwa hali wali mkavu na mkono mtupu haulambwi. Hivyo basi kama kila mtu atajishughulisha kwa bidii watoto hawatakufa njaa. Hivyo wanakijiji wenzangu amkeni mfanye kazi kwa bidii.

Pia tabia ya ulevi wa kupindukia imekithirı sana hapa kijijini. Unakutana na mtu saa mbili asubuhi amelewa chakari. Hivi tunawafundisha nini watoto wetu ambao ni Taifa la kesho? Watoto wetu wataiga ulevi Maana mtoto wa nyoka ni nyoka na pia mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Hivi na hao watoto wakija kuwa walevi tutamlaumu nani? Jamani wanakijiji wenzangu tusiwalee watoto wetu kwenye misingi mibovu ya ulevi kupındukia.

Baada ya kusema hayo mwenyekiti aliwauliza wananchi wa kijiji cha samaki maini kama wana jambo la kuchangia. Mzee Juma alisimama na kuanza kumshukuru mwenyekiti wa kijjı kwa kuandaa mkutano. Alisema ni kweli kijiji chetu kinaongoza kwa ufukara. Na hili tatizo tumechangia sisi wenyewe kwani mchimba kisima hutumbukia mwenyewe.

Kuanzia sasa tutafanya kazi kwa bidii hasa kazi zetu za kilimo kwani jembe halimtupi mkulima. Tabia za ulevi nazo tutaziache. Mambo yote yanayopelekea kijiji chetu kuwa fukara tutayaache. Kwani mdharau mwiba mguu huota tende. Hatutakunywa pombe kwa kificho saa za kazi. Tunakuomba ndugu mwenyekiti wenye kuuza pombe wasiuze saa za kazi. Na kila mtu awe mlinzi wa mwenzie asitokee mtu yeyote atakayekunywa pombe wakati wa saa za kazi. Maana mficha maradhi kifo humuumbua
Mwenyekiti wa kijiji alıfurahi kusikia kwamba wananchi wake watajirekebisha. Aliwaaga kwa kuwaambia asiyesikia la mkuu huvunjika guu. Hivyo kila mtu akatekeleze majukumu yake jinsi tulivyokubaliana ili kijiji chetu kiondokane na ufukara.

**Jibu maswali yafuatayo**
**UFAHAMU**
1. Mzee Jangala ni mwenyekiti wa kijiji gani?
   - ❖ Mzee langala-nimwenyekiti wa kijiji cha samaki maini

2. Wananchi wa kijiji hicho walikua na tabia gani?

- Wananchi wa kijiji hicho walikua na tabia ya ulevi kupindukia hawapendi kufanya kazi kwa bidii na hawakua na ushirikiano katika kazi za kijamii.

3. Ni nani aliyesimama na kuchangia hoja baada ya mwenyekiti wa kijiji kuwaambia kama kuna mtu anataka kuchangia hoja?

- Aliyesimama na kuchangia hoja ni Mzee Juma

4. Orodhesha methali zote zilizopo kwenye habari hii

i. Mficha uchi hazai
ii. Mungu si athumani
iii. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
iv. Mgaa gaa na upwa halı wali mkavu
v. Mtoto wa nyoka ni nyoka
vi. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo
vii. Mchimba kisima hutumbukia mwenyewe
viii. Jembe halimtupi mkulima
ix. Mficha maradhi kifo humuumbua
x. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu

5. Toa maana ya methali hizo

**i. Mficha uchi hazai**

- Aonaye haya kufanya jambo hakika hawezi kulitekeleza, hivyo hatalifaidi, Au anayeona aibu kueleza shida udhaifu au dosari zake hawezi kupewa msaada.

**ii. Mungu si athumani**

- Mungu si binadamu ukadhani atashindwa, yeye anaweza yote, hata yaliyowashinda wanadamu.

**iii. Mgaa gaa na upwa hali wali mkavu**

- Anayejibidısha au kujishughulisha kutafuta hakika hatakosa kupata kitakachomfaa

**iv. Mkono mtupu haulambwi**

- Asiyeweza kuwafaa wengine hawezi kutegemewa kwa msaada wala kupewa heshima.

MWL

**v. Mtoto wa nyoka ni nyoka**

- Mtu hufuata tabia za wazazi au walezi wake

**vi. Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo**

- Mtoto huwa mwema au mtukutu kulingana na malezi anayopatiwa, yakiwa mazuri mtoto huwa mwema yakiwa mabaya mtoto huwa mtukutu

**vii. Mficha maradhi kifo humuumbua**

- Anayeona haya kusema yanayomsibu ili kupata ufumbuzi huridhika na hali iwapo mbaya.

viii. Mchimba kisima hutumbukia mwenyewe

- ❖ Anayepangia watu wengine ubaya si ajabu akajikuta yeye mwenyewe akidhuriwa nao.

ix. **Jembe halimtupi mkulima**

- ❖ Anayejibidisha katika kazi daima hakosi kupata ujira wake

x. **Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu**
Ushirikiano katika kufanya jambo una uaIO

xi. **Asiyesikia la mkuu huvunjika guu**
Anayekataa makanyo ama mafundisho apewayo na wakubwa zake huishia kufikwa na mabaya ambayo angesikiliza pengine angeyaepuka.

**Andika Sentensi Zifuatazo Katika Hali Ya Kutendewa**

1. Baba amechonga kiti kizuri
   - Baba amechongewa kiti kizuri
2. Timu ilifunga goli la kwanza kwa penalti
   - Timu ilifungiwa goli la kwanza kwa penalti
3. Bibi amepasua kuni zote
   - Bibi amapasuliwa kuni zote
4. Baba anapika viazi kwa kutumia jiko la gesi
   - Baba anapikiwa viazi kwa kutumia jiko

la 5 Msanii ameandika barua
   - Msanii ameandikiwa barua

6. Musa alichota maji ya kuoga
   - Musa alichotewa maji ya kuoga
7. Mama amepika ugali mtamu sana
   - Mama amepikiwa ugali mtamu sana
8. Shangazi alifua nguo zote
   - Shangazi alifuliwa nguo zote
9. Baba alichinja ng ombe wawili
   - Baba alichinjiwa ng ombe wawili
10. Kijana atachcza mpira vizuri
   - Kijana atachezewa mpira vizuri

**Tegua Vitendawili Vifuatavyo**

1. Abiria wote wamelipa isipokua hawa weusi
   - Nzi
2. Akikuandama hupendwi
   - Ukoma au ugonjwa wa ngozi
3. Ba funua Ba funika
   - Unyayo utembeapo
4. Baba kanipa sanduku funguo hakunipa
   - Tumbo
5. Bwana mkubwa kaanguka na mikoti koti yake

MWL.

- Mgomba

6. Cha ndani hakitoki nje, cha nje hakiingii ndani
   - Nyama ya mfupa
7. Dume la paa lina pembe mbili
   - Kıpepeo
8. Fimbo ya babu ina mafundo
   - Muwa

**B. Kusoma Na Kubaini Mnethali Zinazofanana**

Methalı ni usemi mfupi wa mapokeo wenye mpangilio maalumu wa maneno unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yatokanayo na uzoefu wa maisha ya jamin husika.

Ni kauli fupi yenye pande mbili za fikra ambazo upande wa kwanza huanza na upande wa pili humalizia

**Mfano**

i. Usimhukumu dobi, kaniki ndiyo rangi yake
ii. Tumikia kafiri, upate mradi wako
iii. Mpanda ovyo, hula ovyo
iv. Aliyekupa wewe kiti ndiye alıyenipa mimi kumbi

Baadhi ya methali huwa na maana zinazofanana, yaani hutoa ujumbe unaofanana

**Mfano**

a) Hasira za mkizi tijara ya mvuvi ina ujumbe unaofanana na ule wa methali ya "Vita vya panzi furaha ya kunguru. Methali hizi zinatuonya tuangalie matendo au uamuzi wetu usije ukatutia hasara na ukawanufaisha wengine.
b) Ndondodo si chururu ina ujumbe unaofanana na ule wa methali ya "haba na haba hujaza kibaba" Methali hizi zina maana kwamba juhudi katika kutimiza kitu hata kama ni kidogo mwishowe huzaa matunda makubwa

c) Hakuna kama mama methali hii ina maana sawa na methali "Titi la mama litamu hata likiwa kama la mbwa.

**Andika methali nyingine zenye maana sawa na hizı zifuatazo**

i. Heri kenda shika kuliko kumi nenda rudi
   - Moja shika si kenda nenda urudi

ii. Jana hairudi tena
   - Ujana ni moshi, uendapo haurud

iii. Jembe halimtupi mkulima

- Mgaagaa na upwa hali wali mkavu

iv. Jifya moja halinjiki chungu
- Kidole kimoja hakivunji chawa

v. Kanzu ya kuazıma usuvae ijumaa
- Nguo ya kuazima haisitiri mataka

vi. "Ndondondo si chururu
- Haba na haba hujaza kibaba
- Kidogokidogo ndio mwendo
- Papo kwa papo kamba hukata jiwe
- Polepole ya kobe humfikisha mbali

vii. Udongo uwahi ungali maji
- Usipoziba ufa utajenga ukuta
- Mtoto mkanye angali mdogo
- Samaki mkunje angali mbichi

viii. Mchimba kisima huingia mwenyewe
- Sheria ni msumeno
- Kupanda mchongoma kushuka ndio ngoma

ix. Kinyozi hajinyoi na akijinyoa hujikata
- Milima haikutani lakini bınadamu hukutana

x. Mdharau mwiba mguu huota tende
- Mchelea hak hatendi ukweli

xi. Kidole kimoja hakivunji chawa
Umoja ni nguvu utengani ni udhaifu

xii. Fimbo va mbali hatui nyoka
Kamba ya mbali haifungi kuni

MWL

**KUBAINI MAKOSA YA KIUANDISHI KATIKA MATINI ANUAI**

Lugha ndicho chombo kikuu cha mawasiliano baina ya watu. Hivyo ili watu waitumie lugha kwa kuelewana lazima itumike kwa usahihi. Mzungumzaji akikiuka kanuni za lugha, huzungumza lugha potofu Upotoshaji huu hujitokeza katika sarufi na kwenye mantiki. Makosa katika sehemu zote mbili husababisha kukatika kwa mawasiliano au kutoa ujumbe uliokusudiwa.

**Soma habari ifuatayo kisha onesha maneno yenye makosa**

Furaha ni madini ya samani sana. Furaha ingaliuzwa ingalikua gali mno, kwani ingalipatikana kwa lahisi ingalipoteza samani yake.

Binadamu huanza kuonesha furaha tokea utotoni kwa kutabasamu na kucheka. Furaha ya kudumu haitokani na nasaba bora, elimu kubwa au mali nyingi, bali inatokana na mtu kuishi na wenzake kwa kujiamini, kufanya kazi kwa bidii na kulizika

Chozi lilivyokua na samani kubwa limegawanyika tu kwa mtu kufiwa na wazazi, lakini humwagwa pia katika furaha. Dunia ingalikua nzuri zaidi walimwengu wangelitumia nia njema, maarifa na juhudi kutokomeza chuki, zuluma, ziki, na ubaguzi, wakajenga na kuimarisha udugu, haki na usawa.

**MANENO YENYE MAKOSA**

i. Samani - thamani
ii. Gali- ghali
iii. Lahisi- rahisi \
iv. Zuluma - dhuluma
v. Ziki- dhiki
vi. Kulizika -kuridhika

**UFAHAMU**

1. Mwandishi anasema furaha ni kitu gani?
    - Mwandishi anasema furaha ni madini ya samanı sana

2. Mwandishi anaeleza kama furaha ingalikua rahisi ingalipotea nini?
    - Mwandishi anaeleza kama furaha ingalıkua rahisi ingalipoteza thamani yake.

3. Binadamu huanza kuonesha furaha wakati gani?
    - Binadamu huanza kuonesha furaha toka utotoni kwa kutabasamu na kucheka

4. Mwandishi anaeleza furaha inatokana na nini
    - Mwandishi anaeleza furaha inatokana na
    - Mtu kuishi na wenzake kwa kujiamini
    - Kufanya kazi kwa bidii na kuridhika

MWL

**MSAMIATI**

**Toa maana ya msamiati kisha tunga sentensi**

**i) Furaha**

a. Ukunjufu wa moyo, uchangamfu
b. Hali ya kuridhika

**Sentensi**

- Dada alipohitimu elimu ya juu alikua na furaha sana

**ii) Nasaba**

a) Uhusrano wakizazr baina ya watu, uhusiano kutoka katıka mlango au ukoo mmoja

**Sentensi**

- Baba alituambia watu wa nasaba moja hawana budi kuheshimiana

**iii) Kazi**

b) Shughuli anayofanya mtu kama vile kulima,
kufundisha Sentensi

- Baba yangu anafanya kazi ya kuvua samaki

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi**

1.Mazao yamejaa wingi darını
- Mazao yamejaa kwa wingı darını

2. Nta wananata sana
- Nta manata sana

3. Nywele wamekua ndefu
- Nywele zimekua ndefu

4. Funua ukurasa wa kitabu vyako
- Funua ukurasa wa kitabu chako

5. Nyota imetanda anga yote
- Nyota zimetanda anga lote

6. Treni la mzigo
- Treni ya mizigo imedondoka limedondoka

7. Ndugu yangu unaitwa nini
- Ndugu yangu unaitwa nani.

8 Sisi sote afanye kazi kwa bidii
Sisı sote tufanye kazı kwa bidii

9. Macho ina kope
- Macho yana kope

MWL

**Pigia mstari viwakilishi katika sentensı zifuatazo**

1. **Wale** ndiyo waliofanikiwa kurudi na medali katıka mashindano ya mbio za marathoni
2. **Mimi** ndiye ninayefua nguo za bibi
3. Wao wanalima mazao ya biashara
4. Yule ni mchezaji hodari wa mpira wa kikapu
5. **Sisi** na wao tutakwenda kuwinda
6. **Wewe** ndiye uliyechora picha nzuri

**D. Kusoma Matangazo Na Kubaini Taarifa Muhimu**

**Tangazo** ni taarifa inayotolewa hadharani ili ipate kuwafikia watu wanaohusika na taarifa hiyo. Taarifa inaweza kuwa ya mkutano, semina, msiba, masomo, nafasi za kazi, onyo au biasara. Taarifa huweza kutolewa kwenye vyombo vya habari kama vile redio, televisheni (luninga) Magazeti. Pia kwenye mabango

MAMBO YA KUZINGATIA KATIKA UANDISHI WA MATANGAZO

1. Kutumia lugha inayoeleweka
2. Kutumia maandishi yanayosomeka vizuri
3. Kutumia picha na michoro inapowezekana
4. Kutoa maelezo yanayojitosheleza ili tangazo lipate kueleweka
5. Kama tangazo linatokea redioni au kwenye televisheni litolewe kwa kutumia sauti inayosikika vizuri

**Soma Matangazo Yafuatayo Kisha Jibu Maswali**

**NAFASI ZA KAZI**

Mbuyeku limited ni kampuni inayojishughulisha na uuzaji na usambazaji wa vifaa vya ujenzi kama vile mabati, simenti, nondo n.k. Kampuni inazo nafasi mbili za kazi

Mhasibu na katıbu muhtasi

**1. MHASIBU**

Majukumu ya mhasıbu ni kusimamia mahesabu ya kampuni, kuandaa ripoti za fedha, kufuatilia masuala ya kodi na kubuni mikakati ya kutumia vizuri rasilimali za kampuni

**ELIMU NA UZOEFU**

1. Shahada ya ACCA /CPA na hali ya uthibitisho ya NBAA
2. Ujuzi wa kanuni mbalimbali na sheria zinazohusiana na taaluma ya uhasibu
3. Ujuzi wa kutumia kompyuta ya kiuhasibu
4. Uzoefu wa miaka mitatu katika kusimamia mifumo ya uhasibu.
5. Uandaaji wa ripoti za uhasibu mahali pa kazi na shughuli nyingine za kitaaluma.

**2. KATIBU MUHTASI**

Mwombaji anatarajrwa kuisaidia menejimenti katika shughuli mbalimbali za utawala na uendeshaji wa kampuni ikrwemo kupokea na kusambaza taarifa, kushughulikia barua zinazoingia na kutoka, kuandan mikutano, kuweka mafailı katıka mıfumo na shughuli zingine na kiutawala.

**ELIMU NA UZOEFU**

1. Mafunzo ya usekretari kutoka chuo kinachotambulika
2. Ujuzi wa matumizi ya kompyuta
3. Ujuzi wa kanuni na uelewa wa kuendesha ofisi
4. Ujuzi na uzoefu wa mawasiliano na uandishi wa ripoti
5. vUzoefu wa kazi ya usekretari wa miaka miwili

**JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Waombaji waandike barua za maombi, waambatanishe na wasifu binafsi (CV) na nakala za vyeti, namba za simu na anwani za barua - pepe. Barua za maombi zinaweza kupelekwa jengo la Josam Mwenge, ofisi za Mbuyeku LTD au kutumwa kwa Meneja Mbuyeku LTD S.L.P 2502, Dar es salaam. Tarehe ya mwisho kupokea maombi ni tarehe 15.4.2020.

Watakaojibiwa ni wale tu watakaoorodheshwa kwa ajili ya kusailiwa

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Tangazo hili linahusu nini?
   - Tangazo hili linahusu nafasi za kazi ya uhasibu na katibu muhtasi.
2. Tangazo hili limetolewa na kampuni gani?
   - Tangazo hili limetolewa na kampuni ya Mbuyeku

LTD 3 Kampuni hiyo inajishughulisha na nini?
   - Kampuni hiyo inajishughulisha na uuzaji na usambazaji vifaa vya ujenzi

4. Barua za maombi zinatakiwa kutumwa kwa nani?
   - Barua za maombi zinatakiwa kutumwa kwa Meneja wa Mbuyeku limited.
5. Barua za maombi zinatakiwa ziambatanishwe na vitu gani?
   - Barua za maombi zinatakiwa ziambatanishwe na wasıfu binafsi (cv) na nakala za vyeti, namba za simu na anwani za barua pepe.
6. Lini ni mwisho wa kupokea maombi?
   - Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15.4.2020

**3. YANAHITAJIKA MAGARI YA KUSAFIRISHA KAHAWA**

Tunakaribisha maombi kusafirisha kahawa kutoka Moshi Kilimanjaro kwenda Congo. Magari yanayohitajika ni yale nyenye uwezo wa kuchukua kuanzia uzito wa tani kumi (10)

Malipo mazuri na ya kuvutia yatatolewa.

Kuhusu hati za maombi na maelezo zaidi mwone au mpigie simu

**Meneja mkuu**
**Mamlaka ya kahawa (KNCU)**
**S. L.P 21**
**MOSHI-KILIMANJARO**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15.4.2020.

**Jibu Maswali Yafuatayo**

1. Tangazo hili linahusu nini
   - Tangazo hili linahusu maombi ya kusafirisha kahawa
2. Kahawa zinatakiwa kusafirishwa kutoka wapi kwenda wapi?
   - Kahawa zinatakiwa kusafirishwa kutoka Moshi Kilimanjaro kwenda Congo
3. Magari yanayohitajika yanatakiwa yawe na sifa zipi?
   - Magari yanayohitajika yanatakiwa yawe na uwezo wa kuchukua uzito kuanzia tani kumi.
4. Maombi yanatakiwa kupelekwa kwa nani?
   - Maombi yanatakiwa kupelekwa kwa Meneja mkuu mamlaka ya kahawa KNCU

**e. Kusoma hadithi za kubuni kwa burudani na kwa kuzingatia alama za uandishi**
**HADITHI - maana**

Hadithi ni masimulizi yenye kusimulia habari fulani

Ni masimulizi yanayotumia lugha ya mjazo au nathari na mtiririko wake huwa mwepesi au sahili. Zipo hadithi za kubuni na zingine za kihistoria.

**SOMA HADITHI IFUATAYO, KISHA JIBU MASWALI**
**SUNGURA NA NGIRI**

MWL

Hapo zamani za kale Sungura na ngiri walikua marafiki wakubwa. Walikua wakitembea pamoja na kufanya shughuli zao pamoja. Siku moja walipanga kwenda safari ya mbali. Basi siku ilipowadia, walifunga safari bila hata kuchukua chakula na fedha. Ngiri alimweleza rafiki yake hakuna haja ya kubeba chakula kwani chakula kingi kipo njiani. Hivyo asiwe na wasiwasi. Baada ya kutembea kitambo kidogo, ngiri alimwambia rafiki yake, "Iwapo utaanza kuona chochote kile kinacholiwa utakula peke yako".

Baada ya mwendo mfupi, Sungura akaona maembe, kabla ngiri hajayaona. Akamwambia ngiri, Nimeyaona maembe, hivyo nitakula peke yangu. Ngiri akamjibu maembe yale ni yangu mimi ndiye niliyeanza kuyaona ndio maana ninayachekelea. Au unajifanya

hunioni ninavyoyachekelea? Sungura alistaajabu na kujisemea kimoyomoyo, "Meno ya ngiri wakati wote yako nje na si kwamba anacheka. Sasa iweje adai eti anachekelea maembe? Hata hivyo, kwa kuwa hakuwa na nguvu kama ngiri, alimwacha ale yale maembe.

Alipomaliza waliendelea na safari mbele kidogo, Sungura aliona mapapai. Basi mara akamuuliza ngiri, "Je umeona chochote? Kwa kuwa ngiri haoni mbali alijibu, "sijaona chochote. Kwani wewe umeona nini? Hapo Sungura alipata faraja akamwambia ngiri nimeona mapapai hivyo nitakula peke yangu" ngiri aliposikia hivyo alisema kwa ukali, "Mapapai hayo ni ya kwangu, nami niliyaona tangu mbali ndiyo maana nilikua nayachekelea. Niliposema sijaona kitu nilikuwa nakudhihaki tu".

Ngiri alikula mapapai yote peke yake. Sungura alipoona mambo yanazidi kuwa magumu, alichelea kufa kwa njaa kwani rafiki yake alikua anamdhulumu kila alichokiona. Sungura alijiona yupo kwenye ukingo wa kaburi kwani angeweza kufa wakati wowote kutokana na njaa.

Safari iliendelea lakini Sungura aliwaza namna ya kumtelekeza ngiri ili asife njaa. Mara walifika kwenye msonobari. Nyuma ya msonobari walimsikia simba akikoroma. Sungura alijisemea, "sasa wakati wangu wa kulipa kisasi umefika". Basi Sungura alianza kupiga kelele na kucheka ovyo. Ngiri alikua haelewi kwanini Sungura anafanya vile. Hatimae kicheko kilimwamsha simba. Simba aliuliza, "Nani anapiga kelela eamna hii wakati mimi nimejipumzisha? Ngiri alijibu, Sungura ndiye anayecheka hovyo". Sungura alijibu kwa unyenyekevu, "Hapana si mimi, mfalme wangu mtukufu. Ngiri ndiye aliyekua anacheka hovyo, unamwona anaendelea kucheka?" ngiri alijitetea, "Haya ni maumbile yangu tu.

Meno yangu yako nje wakati wote na sio nakucheka", Sungura alizidi kumkandamiza, "Anakudanganya huyo, mfalme. Mwangalie, hadi sasa meno yake bado yako nje, anaendelea kukucheka. Anasema eti una nywele mpaka machoni. Ngiri alijitahidi kukataa na kujitetea lakini maneno yake hayakufua dafu mbele ya hasira za simba. Simba alimrukia na kumrarua, kisha akamla Wakati simba aliposhiba, alilala usingizi mzito. Sungura

alijizoazoa kwa tabu na njaa yake na kurudi nyumbani. Ama kweli shibe mwana malevya na njaa ni mwana malegeza.

**UFAHAMU**

**Jibu maswali yafuatayo.**

1. Sungura na ngiri walipanga kufanya nini?
    - Sungura na ngiri walipanga kwenda safari ya mbali
2. Kwanini Sungura na ngiri hawakuchukua chakula?

- Sungura na ngiri hawakuchukua chakula kwa sababu ngiri alımwambia njiani kuna chakula kingi

3. Sungura na ngiri walikubaliana nini
   - Sungura na ngiri walıkubaliana atakaye kuwa wa kwanza kuona chochote kile kinacholiwa atakula peke yake.
4. Ni nani aliona chakula njiani?
   - Sungura aliona chakula njiani.
5. Na ahkua hakula chaula hiehe
   - Ngiri ndiye aliyekua anakula chakula hicho
6. Kwanini simba aliamka?
   - Simba aliamka kwa sababu alisikia kelele na kicheko cha Sungura akicheka hovyo.
7. Simba alifanya nini baada ya kusikia maelezo ya Sungura?
   - Simba alimrukia na kumrarua kisha akamla ngiri
8. Ngiri ameonesha tabia gani?
   - Ngiri ameonesha tabia ya ubinafsi
9. Je, tabia hiyo ni nzuri au mbaya?
   - Tabia hiyo ni mbaya
10. Taja methalı iliyotumika katika hadithi hii
    - Methali iliyotumika katika hadithi hii ni Shibe mwana malevya na njaa mwana malegeza

**2.3. KUTUMIA MSAMIATI KATIKA KUSOMA ILI KUCHANGANUA MAWAZO YALIYOWASILISHWA KATIKA MATINI MBALIMBALI**

**A. Kusoma Matinı Na Kubainı Mapya Na Kueleza Maana Zake Soma habarı ifuatayo kisha jibu maswali**

Wamasai ni kabila pekee lenye kutunza mila zao na destur zao. Kabila hili ni maarufu kwa shughuli za ufugaji. Wao huishi kwa kutegemea wanyama. Wamasar hujulikana kırahisı kutokana na utamaduni wao kuwa wakapekee Vizi lae berubern.mtutobo. menit Wamasai huishi kwa kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho kwa ajin ya mifugo yao. Ufugaji wa kimasai ni wa kizamani kwani hufuga idadi kubwa ya mifugo. Ufugaji wa kisasa unalenga kutuga idadı ndogo ya mifugo kwa njia za kitaalamu.

Mifugo ifugwayo na wamasai ni ile yenye kustahimili uhamiaji. Mifugo hiyo ni kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda. Wanyama hawa huwapatia maziwa, nyama, ngozi na pesa wauzwapo. Punda huwasaidia kubeba mizigo. Wamasai pia hufuga mbwa kwa ajili ya ulinzi. Wamasai hutumia akıli zao na muda wao mwingi kulinda mifugo yao dhidi ya maadui. Kundi maalumu la vijana wa kimasai liitwalo morani hulinda mifugo. Wanyama waishio porini kama simba, chu, fisi na nyoka ni hatari kwa mifugo yao. Hivyo wamasai

hubeba silaha za kiulinzi ili kukabiliana na wanyama hao wa porini. benga mkononi na mimmni ni alama zinazotambulishawamasa

**UFAHAMU**

1 Wamasai ni kabila pekee lenye kutunza nini?
- Wamasai ni kabila pekee lenye kutunza mila na desturi zao

2. Kabila hili ni maarufu kwa shughuli gani?
- Kabıla hili ni maarufu kwa shughuli za ufugaji

3. Vazi la kimasai linaitwaje?
- Vazi la kimasai linaitwa rubega.

4. Wamasai hutambulika kwa alama zipi?
- Wamasai hutambulika kwa vazi lao la rubega, kutoboa masikio na uvaaji wa shanga kiunoni na miguuni

5. Kwanini wamasai huishi kwa kuhamahama?
- Wamasai huishi kwa kuhamahama kwa ajili ya kutafuta malisho ya mifugo yao

6. Faida hupata wamasai kutokana na mifugo yao?
- Wamasai hupata nyama, maziwa, ngozi na fedha wanapouza mifugo yao.

7. Punda huwasaidia nini wamasai?
- Punda huwasaidia kubeba mizigo.

8 Wato gani hulinda mifugo?
- Watu wanaolsnda mifugo nı vijana waitwao morani.

**MSAMIATI**

**Toa maana ya msamiati na kisha tunga sentensi**

**i) Mila**
- Mambo yanayofanywa na jamii fulani ambayo yanalingana na asili, mazingira na nyendo za jamii.

**Sentensi**
- Babu alitumbia mila zao ni kutambika kwenye mti mrefu katikati ya msitu.

MWL

**ii) Kabila**
- Kikundi cha watu wanaohusiana kwa lugha, mila, desturi na utamaduni
- Jamii ya watu au vitu vya aina moja

**Sentensi**
- Mwalimu wa historia alituambia kabila la wagogo linapatikana mkoani Dodoma.

**iii) Utamaduni**
- Mila, asrh, jadr, na desturi za kundi la jamii fulani

**Sentensi**
- Ukarımu ni utamaduni wa watanzania

**iv) Malisho**

- Chakula cha wanyama kama vile majani au maganda
- Ulishaji wa wanyama

**Sentensi**

- Bwana shamba aliwaambia wanakijiji wafuge mifugo yao kulingana na eneo la malisho.

**v) Stahimili**

- Chukua mambo mazito bila ya kulalamika, kuwa na uwezo wa moyo wa kuchukua yalıyo mazito

**Sentensi**

- Mama alıpanda mbegu za mahindi zinazostahimili ukame.

**B. KUSOMA MATINI MBALIMBALI YANAYOELEZEA HALI YA HEWVA NA KUBAINI MAJIRA YAKE.**

**<u>HALI YA HEWA</u>**

Halı ya hewa ni jumla ya hali tofauti zinazomzunguka mwanadamu katıka mazingira yake. Mfano upepo, baridi, joto, kipupwe, mvua n.k. kila halı ya hewa huweza kuoneshwa kwa dalih ambazo huleta athari fulani katika mazingira. Miongoni mwa hali hizo za hewa ni ukungu, upepo, joto, baridi na mvua

Shughuli za binadamu zinategemea hali ya hewa ya mahali Kila kipengele cha hewa ni muhimu katika shughuli za binadamu. Vipengele vya hali ya hewa vinatakiwa viwe na uwiano sawa

**Soma habari ifuatayo kısha jibu maswali**

Mwalimu Ana anatufundisha somo la jiografia darasa la sita katika shule ya msingi uswaa huko mkoani Kilimanjaro. Siku moja alitufundisha juu ya hali ya hewa na majira ya hali hızo za bewa Ahanra kwa kusema
Aina za majira ya mwaka hapa kwetu Tanzania ziko nne, kuna majira ya mvua za vuli, majira ya mvua za mwaka, majira ya baridi na majura ya joto.

Majira haya hutofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu mbalimbali. Baadhi ya sababu hizo ni umbalı kutoka usawa wa bahari, mwinuko kutoka usawa wa bahari na kuwapo kwa milima misitu au majangwa.

Majira ya mvua yako ya aina mbili. Mvua za mwaka na mvua za vuli. Si kila sehemu nchini hupata aina zote mbili za majira ya mvua.

Majira ya joto hujulikana kama kiangazi. Mvua huadimika kabisa na ardhi inakuwa kame. Ni wakati ambapo vyito vya muda na visima vifupi hukauka na uhaba mkubwa wa maji hutokea.

Majira ya kipupwe ni kipindi cha baridi. Sehemu za pwani huwa na baridi kiasi lakini milimanı huwa na baridi kali. Watu huvaa nguo nzito na usiku hujifunika gubigubi.
Faida za kuwa na majira mbalimbali ya mwaka ni nyingi. Wakati wa mvua watu hupanda mazao ya chakula na biashara. Wakati wa joto, watu hufanya kazi za ujenzi. Wakati wa baridi ni wakati wa kupata hewa nzuri

**Jibu maswali yafuatayo**

1. Nini maana ya hali ya hewa
   - Hali ya hewa ni jumla ya hali tofauti zinazomzunguka mwanadamu katıka mazingira yake mfano upepo, baridi, joto, kipupwe, mvua n.k.

2. Taja aina kuu nne za majira ya hali ya hewa Aina za majira ya hali ya hewa ni
   a) Mvua za vuli
   b) Mvua za mwaka (masika)
   c) Kıpupwe
   d) Kiangazi (joto)

3. Wakati wa kiangazi (joto) hali ya hewa inakuaje?
   - Wakati wa kiangazi hali ya hewa inakua ni joto na kunakua na ukame na pia kuna kua na uhaba wa maji.

4. Wakati wa kipupwe hali ya hewa inakuaje?
   - Wakati wa kipupwe hali ya hewa inakua ya baridi kali.

5. Faida za kujua /kufahamu majira ya mwaka ni zipi?
   - Kujua majira husaidia watu kujua kipindi gani wafanye shughuli zipi. Mfano kipindi cha mvua ni kipindi cha kuotesha mazao ya biashara na chakula.

MWL

**C. Kusoma kifungu cha habari na kubaini maneno mapya yenye maana zaidi ya moja**

Baadhi ya maneno ya Kiswahili yana maana zaidi ya moja kutegemeana na jinsi neno lilivyotumika au lilivyotamkwa. Maneno yenye maana zaidi ya moja huitwa maneno tata. Utata katika mawasiliano hutokea pale uto anapotumia maneno yenye maana zaidi. Utata hutegemea muktadha mbalimbali pamoja na matamshi au hata mazingira ya neno linalohusika. Utata unaweza kujitokeza katıka neno na wakati mwingine katika sentensi

**Mfano**

**Kaa - neno hili lina maana zifuatazo**

i) Kaa la moto

**Sentensi**

- Mtoto amekalia kaa la moto

ii) Kuweka makalio chini/kitini

**Sentensi**

- Wanafunzi wote wanatakiwwa kukaa chini

iii) Mnyama wa majini

**Sentensi**

- Tulipokwenda mtoni kuteka maji tulimwona kaa

**Soma habari ifuatayo kisha ibu maswali**

Siku moja dada alimwomba mama amfundishe kupika samaki mbichi wa kuchemsha. Mama alimkubalia ombi lake. Alimwanmbia atamfundisha siku inayofuata.

Muda ulipowadia, mama alimwita dada ili amfundishe kupika samaki mbichi wa kuchemsha. Dada alikaa kwenye mkeka kisha akamsikiliza mama kwa makini.

Mama alimwambia, unachukua samaki na kumpaa. Unahakikisha magamba yote yametoka kisha unamwosha kwa maji safi, ukimalıza kumwosha unamwacha achuruzike majt Baada ya hapo unampaka viungo kama vile chumvi, ndmu, kitunguu swaumu na tangawizi. Viungo husaidia kuondoa shombo na pia humfanya samaki awe na ladha nzuri.

Baada ya hapo unachukua mbuzi na kukuna nazi, kisha unachuja nazi. Tui zito la kwanza unaloweka pembeni kwani tui hili hutumika mwishoni pale samaki anapokua amekaribia kuiva Unachuja tena jepesi na kuliweka kwenye sufuria ya kupikia samaki. Kisha unachukua karoti na vitunguu maji na kuvikata vipande vidogovidogo.

Bandika sufuria lenye tui jepesi jikoni na kisha weka karoti na vitunguu na ongeza chumvi kidogo. Acha tui jepesi lichemke kwa dakıka tano kisha tumbukiza samaki mbichi. Mwache achemke akikanba kuiva weka tui zito. Acha lichemke kwa dakika nane, tui litakua limeiva na samaki atakua ameiva. Ila unatakiwa kuangalia samaki asirojeke. Baada ya hapo epua samak atakua tayari kwa kuliwa.

Samakı wa kuchemsha anaweza kuliwa na ugali, wali au chapati. Pia samaki hutupa protini ambayo ni muhimu katika miili yetu.

**UFAHAMU**

1. Dada alimwomba nini mama?
   - Dada alimwomba mama arnfundishe kupika samaki wa kuchemsha
2. Samaki wa kuchemsha ana faida
   - Samaki wa kuchemsha anatupatia protini ambayo hutusaida kujenga mwili gani mwilini
3. Taja maneno yenye maana zaidi ya moja yaliyotumika katika habari hii
   a) Kaa
   b) Mbuzi
   c) Kata
   d) Paa

4. Toa maana za maneno hayo

**Kaa**

a) Kaa la moto
b) Kuweka makalio chinikitini
c) Mnyama wa majini

**Mbuzi**

a) Kifaa cha kukunia nazi
b) Mnyama wa kufugwa

**Kata**

a) Ni chombo cha kutekea maji kutoka mtoni au mtungını
b) Kutenganisha kitu kwa kutumia kitu kikali kama vile kisu, shoka, panga au jembe

**Paa**

a) Sehemu ya juu ya nyumba
b) Enda juu
c) Mnyama anayefanana na mbuzi

MWL.

**MAZOEZI YA LUGHA**

**Oanisha kifungu A na B ili kupata maana**

| | A | | B |
|---|---|---|---|
| 1 | Kupalia mkaa | A | Mchoyo |
| 2 | Kupiga chuku | B | . Pata nafuu |
| 3 | Mkono wa birika | C | Kutia chumvi |
| 4 | Pata ahueni | D | Kujitia matatizoni |
| 5 | Unga mkono | E | Kufukuzwa kazi |
| 6 | Kibarua kimeota nyası | F | Kubaliana naye |

MAJIBU
1.D
2. C
3. A
4. B
5. F
6. E

**Bainisha aina za sentensi hizi**
1. Baba anafua nguo zake
   - Sentensi sahili
2. Mlinzi alifungua mlango lakini dereva hakupita
   - Sentensi ambatano
3. Akıja anioni
   - Sentensi shurutia
4. Mtoto aliyekuja jana ameondoka
   - Sentensi changamano

**Kamilisha sentensi kwa kujaza vielezi sahihi**
1. Mshtakiwa aliapa kutorudia jambo hilo
   - Mshtakiwa aliapa kutorudia jambo hilo kamwe._______(kamwe, vibaya)
2. Kazi yake nzuri_____ilipendeza (hivi sana)
   - Kazı yake nzuri sana ilipendeza.
3. Dira hiyo ilimuongoza kwenda___(popote, yeyote)
   - Dira hiyo ilimuongoza kwenda popote
4. Rehema aliyauza maembe hayo_____(kabla ya, kwa mafungu)
   - Rehema aliyauza maembe hayo kwa mafungu.

MWL.